# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MBILI

## Kikao cha Tisa – Tarehe 6 Septemba, 2013

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alikalia Kiti*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 106

### Usafi wa Barabara Pale tu Viongozi Wanapotembelea Maeneo

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC** aliuliza:-

Kumekuwa na kawaida Viongozi wa Wilaya hapa nchini kuagiza usafi na kurekebisha barabara mbovu mara tu wanaposikia Viongozi wakubwa wa Serikali nchini wanatembelea:-

Je, Serikali sasa inatoa tamko gani kwa udanganyifu huo unaofanywa na Viongozi wa Halmashauri zetu mahali pengi nchini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri nchini zinatekeleza jukumu la kusimamia usafi wa mazingira kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 , Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009, Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya Na. 7 na Mji Na. 8 za mwaka 1982 na Sheria Ndogo za Halmashauri. Vilevile matengenezo na ujenzi wa barabara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa huongozwa na Sheria ya Barabara Na. 13 ya Mwaka 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matengenezo ya barabara zilizosajiliwa kwa mujibu wa Sheria hufanywa mara kwa mara kulingana na upatikanaji wa fedha kutoka katika Mfuko wa Barabara. Lengo likiwa ni kuziwezesha barabara hizo kupitika wakati wote wa mwaka. Kutokana na upatikanaji wa fedha barabara hufanyiwa matengenezo katika maeneo korofi, matengenezo ya kawaida, matengenezo maalum, ujenzi wa madaraja na makalvati. *(Makofi)*

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwa kuwa, suala hili kwanza lipo wazi wazi na linaonekana wazi na mifano mingi imekuwa ikionekana katika Mikoa mingi. Swali langu ni kwamba kwa kuwa, Miji mingi unakuta ipo imechoka, barabara ni mibovu za Mitaani, misingi haijajengwa na kisingizio kikubwa katika Halmashauri inakuwa kwamba fungu la fedha hawana. Inapotokea ujio wa kiongozi tu au Mbio za Mwenge tayari Viongozi wa Halmashauri wanaanza kuhimiza sasa usafi wa barabara, kujenga barabara zile mbovu hata kurekebisha misingi ya barabara katika Mitaa.

Je, Serikali haioni kwamba hawa viongozi wa Halmashauri wanatumia udanganyifu wa kuwadanganya Viongozi Wakuu pamoja na wananchi ambao ndiyo walipa kodi. Kama kuna viongozi wanaotumia udanganyifu huo Serikali inawachukulia hatua gani ya kinidhamu na ya kiuongozi?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa AnnaMarystella, Mheshimiwa Waziri majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida usafi unatakiwa ufanywe kwa Mujibu wa Sheria ambazo nimezitaja na unatakiwa ufanywe mara kwa mara. Sasa kama yapo maeneo ambayo wanasubiri mpaka Viongozi wafike

nadhani hilo ni tatizo ambalo Mheshimiwa Mbunge kama linatokea katika maeneo yake basi inatakiwa pale wanapofika viongozi awaeleze kwamba usafi huo umefanyika kwa Mujibu wa wao kufika ili waweze kuchukuliwa hatua. *(Makofi)*

Katika hali ya kawaida hata nyumbani kwako unaweza ukawa unafanya usafi kila siku, lakini anapokuja mgeni ni lazima wewe mwenyewe ukajiridhishe hiyo yote ni kuonesha heshima ya mgeni anayekuja. *(Makofi)*

Na. 107

**Kutokamilika kwa Wakati Miradi ya *BFFS***

**MHE. OMARY A. BADWEL** aliuliza:-

Wilaya ya Bahi ni moja ya Wilaya inayotekeleza miradi inayopewa fedha na *BFFS* kwa takriban miaka mitano sasa. Miradi imekuwa kero kwa wnaanchi kutokana na kutokukamilika kwa wakati licha ya wananchi kutimiza wajibu wao wa kuchangia miradi hiyo:-

(a) Je, Serikali inajua lolote juu ya sababu za mchakato mrefu unaotumiwa wa *BFFS* katika utekelezaji wa miradi yake?

(b) Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wananchi kuwa Serikali itashirikiana na *BFFS* ili kupunguza urasimu na kusimamia miradi hiyo ikamilike?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omary Ahmed Badwel, Mbunge wa Bahi, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi mradi wa *BFFS* ni wa miaka sita na ulianza kutekelezwa mwishoni mwa mwaka wa fedha 2008/2009 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2014. Katika Wilaya ya Bahi mradi huu unatekelezwa katika vijiji tisa ambavyo ni Chali, Makulu, Chali Isangha, Chali Igongo, Bahi Makulu, Zanka, Nholi Mindola Ilindi na Mpamatwa.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi zilizotekelezwa na kukamilika ni usanifu na kuandaa michoro imefanyika na kukamilika katika vijiji vitano vilivyopata maji, ujenzi na usambazaji wa maji katika vijiji vyote vitano iko katika hatua mbalimbali. Ujenzi wa mradi na usambazaji maji katika kijiji cha Chali Makulu umekamilika na wananchi wanapata huduma ya maji safi. Kijiji cha Chali Isangha usambazaji uko katika hatua za mwisho na ujenzi utakamilika ifikapo mwishoni mwa mwezi Septemba, 2013. Usambazaji wa maji katika vijiji vitatu vilivyobaki vya Nholi, Zanka na Minola inategemea kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2013. Hata hivyo, vijiji viwili vya Ilindi na Mpamatwa vilipata maji kidogo hivyo havikuendelezwa.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikisha Bunge lako Tukufu na wananchi kuwa tangu mwanzo Serikali imekuwa ikishirikiana na wadau wote katika miradi ya *BFFS*, hivyo itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha kuwa miradi iliyokusudiwa inakamilika ndani ya muda uliopangwa yaani mwaka 2014. *(Makofi)*

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwanza, kwa kuwa katika Bunge lililopita Wabunge wengi walilalamika kuchelewa kwa miradi hii mbalimbali na inatokana na hii habari ya kusema tunasubiri *no objection* kutoka kwa wafadhili au wahisani. Kwa kuwa katika Bunge hilo lililopita Mheshimiwa Waziri wa Maji alitoa tamko la kusitisha hizo *no objection* zote na kutaka miradi yote iendelee nchi nzima. Kwa bahati mbaya Waziri hakutoa taarifa yoyote ya maandishi kwa watekelezaji kule Halmashauri ili waweze kutekeleza miradi ile pamoja na fedha zilizokuwa kwenye akaunti bila kusubiri hiyo *no objection*.

Je, Serikali ipo tayari sasa kupeleka hizo taarifa kwa maandishi ili ile miradi iliyokuwa inazuiliwa na *no objection* iendelee kufanya kazi?

(ii) Kwa kuwa urasimu mkubwa unaochelewesha miradi hii unatokana na utaratibu wa ubadilishanaji wa

taarifa na hivyo kuchukua muda mrefu wa kuwapa taarifa na wao kujibu au kutoa taarifa na wale kujibu.

Je, Serikali ipo tayari kuangalia utaratibu mzuri wa upashanaji na ubadilishanaji wa taarifa ili usaidie kupunguza urasimu na miradi iweze kutekelezwa kwa wakati?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Waziri wa Maji alisema kwamba sasa hivi hatuhitaji tena ule utaratibu wa kuomba *no objection* kutoka Wizara ya Maji. Siyo Waziri tu, hata tulivyokutana na Wawakilishi wa Benki ya Dunia walisema huo utaratibu siyo wao bali walikuwa wanasema ni utaratibu wa Wizara ya Maji. Mheshimiwa Waziri wa Maji wakati anatoa kauli hiyo aliitolea Arusha ambapo mimi nilikuwepo, Makatibu Wakuu wa Wizara, Wizara zote mbili za Maji na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI tulikuwepo, Wakurugenzi walikuwepo, Wahandisi wa Maji walikuwepo na wote katika maeneo mengine waliendelea na utaratibu wa kutokufuata *no objection.* Sasa kama Bahi wanasubiri mpaka waletewe maandishi nadhani wana matatizo ya ziada ambayo tunahitaji kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kubadilisha utaratibu ili kuondoa urasimu, nadhani mojawapo ni hiyo ya kusema kwamba sasa hivi hatuhitaji *no objection*. Kwa Miradi ya Maji tulivyokuwa Arusha Wakurugenzi, Wahandisi wa Maji walisaini jinsi watakavyotekeleza ule mradi na wameapa kwamba

miradi itatekelezwa na itakamilika kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuandikiana Serikali muda wote inakwenda kwa maandishi. Isipokuwa tutajitahidi kama alivyopendekeza kwamba hayo maandishi basi tuwe tunapeana majibu kwa wakati muafaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma Nkamia, swali la nyongeza la mwisho.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nipate kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa miradi inayotekelezwa na Halmashauri Mama imekuwa ikisusua, hasa kutokana na hizi Halmashauri mpya zilizoanzishwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Nchemba; miradi mingi ambayo inatekelezwa na Halmashauri ya Kondoa haiendi kwa sababu ipo Wilaya Nchemba. Kwa mfano, Mradi wa Ntomoko, wamepata hela toka mwezi Mei, 2013 lakini hakuna kinachoendelea mpaka sasa.

Je, Serikali ipo tayari sasa kuhakikisha kwamba miradi hiyo inasimamiwa na Wilaya Nchemba badala ya kusimamiwa na Wilaya ya Kondoa?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Majibu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI, Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni tatizo kwa Halmashauri ambazo tayari zimeshagawanyika na zina watendaji wake wote wamekamilika miradi yao kuitekeleza wenyewe. Pale ambapo bado Halmashauri mpya haijapata watumishi wa kutosha bado nashauri waendelee kushirikiana na Halmashauri Mama ili kuhakikisha kwamba utekelezaji unaenda vizuri na pale watakapokwama basi wasisitize kuishirikisha Ofisi ya Waziri Mkuu - *TAMISEMI* ili kuondoa ile misuguano isiyokuwa ya lazima katika zile Halmashauri zilizogawanyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ahsante. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigangwalla, Mbunge wa Nzega.

Na. 108

**Kukamilisha kwa Mradi wa Umeme wa kwenda Ndala**

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA** aliuliza:-

(a) Je, Mradi wa Umeme kwenda Ndala utakamilika lini?

(b) Je, ni kwa nini shule zote za Msingi na Sekondari pamoja na Zahanati na Vituo vya Afya visiwekewe umeme kwenye mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *TANESCO* ilianza kutekeleza Mradi wa Umeme kwenda Ndala mwezi Oktoba, 2010. Mradi huu unahusisha Vijiji vya Ndala, Shabela na Kilimi na unategemewa kukamilika tarehe 30 Septemba, 2013. Gharama ya mradi huu ni jumla ya Dola za Marekani milioni 15.1 na kazi zilizofanyika ni:-

(i) Ujenzi wa njia ya umeme wa Msongo wa *KV 33* umbali wa kilomita 21.4;

(ii) Ujenzi wa njia ya umeme wa Msongo *KV 0.4* umbali wa kilomita 28.66;

(iii) Ufungaji wa transfoma 4 zenye uwezo wa *KVA 100;*

(iv) Ufungaji wa transfoma 4 zenye uwezo wa *KVA 200*; na

(v) Kuunganisha wateja wa awali 133.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaweka kipaumbele katika kupeleka umeme katika Vituo vya Jamii ambavyo ni pamoja na shule za msingi na sekondari; Zahanati, Hospitali, Vituo vya Afya, Mahakama, Vituo vya Polisi, Magereza, Pampu za Maji na Taasisi nyingine za Serikali. Utekelezaji wa kupeleka umeme katika vituo hivyo vya jamii utaanza mwaka huu wa 2013, katika maeneo yatakayopitiwa na Mpango Kabambe wa Usambazaji Umeme Vijijini Awamu ya Pili unaofadhiliwa na Wakala wa Nishati Vijijini.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Dkt. Hamisi Kigwangalla.

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa nini Serikali isitanue utekelezaji wa mradi huu ili kuhusisha Vijiji vya Eni-Inangana mpaka Miramboitobo?

(ii) Kwa nini Serikali isitekeleze mradi huu kwa gharama zilezile za awali za kufungiwa umeme ambazo ni nafuu kwa wananchi hawa wa vijijini ili katanua wigo wa wananchi wengi zaidi kufaidika na miradi hii ya umeme vijijini?

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Dkt. Hamisi Kigwangalla, kwa maswali mafupi kabisa lakini yenye kueleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hili la ku-*extend* huu mradi ambao unakamilika kuelekea njia ya Usangara, Kaloleni hadi mwisho. Mheshimiwa Mbunge tulikwishawasiliana na nikupongeze kwamba unafuatilia sana miradi ya umeme ya Jimboni kwako na kwamba tumeweka katika *REA Phase two* itatekelezwa miradi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuhusiana na gharama tutaendelea kuwa na gharama hizi ambazo tulizitoa za nafuu ambayo ni kiasi cha shilingi 177,000 kwa mahali tu pasipokuwa na umbali usiozidi mita 30 kwa maana mahali ambapo hapahitaji nguzo na pale ambapo panahitaji nguzo moja basi ni kitu kama laki tatu na sabini na kitu. Fedha hizi tunaamini kwamba wananchi wa kijijini wanaweza kumudu, lakini pia kuna uwezekano wa kuwaruhusu kulipia kwa awamu. Kwa hiyo, imani yetu kubwa ni kwamba wananchi wengi wataweza kuunganisha umeme kwa sababu gharama hizi zinawezekanika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Moshi Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii. Kwa kuwa azma ya Serikali ni kuhakikisha inapeleka umeme vijijini; na Serikali iliahidi kupeleka umeme katika Vijiji vya Kabungu, Mchamchaka, Ifukutwa na Majalira hasa katika maeneo ya shule ya sekondari ya Kabungu na shule ya sekondari ya Kata ya Mpandandogo.

Je, ni lini umeme huo utafika katika vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)**: Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vya Kabungu hadi Majalira na maeneo mengine yanayokwenda na *line* ile hivi vyote vitatekelezwa katika miradi ya umeme ya *REA phase two.*

**MWENYEKITI:** Swali la mwisho la nyongeza Mchungaji Natse.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Naomba niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* imeahidi kupeleka umeme maeneo ya Karatu, Endamalalie wananchi wamejitolea kusimamisha nguzo, nyaya zimewekwa na ahadi ya Serikali imekuwa baada ya wiki mbili umeme utakuwa tayari.

Sasa niulize ni lini umeme Endamalalie utakuwa tayari?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli ziko baadhi ya shughuli ambazo zilianza kufanyika katika mradi huo kutoka Karatu kwenda Endamalalie lakini bado mpaka sasa haujakamilika. Nitajaribu kufuatilia nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge

na wananchi wa Endamalalie, shemeji zangu wale nitajitahidi kufuatilia nione nini kinasababisha kukwama huko. *(Makofi)*

Na. 109

**Hitaji la Umeme Kata za Itezi na Iduda – Mbeya**

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA** aliuliza:-

Katika Kata ya Itezi Mtaa wa Gombe Kaskazini na mitaa mitatu miongoni mwa mitaa minne iliyoko Kata ya Iduda haina umeme licha ya kuwepo katika Jiji la Mbeya.

Je, ni kitu gani kinachopelekea mitaa hiyo kutokuwa na umeme hadi leo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshmiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwa na umeme kwa muda mrefu katika maeneo anayouliza Mheshimiwa Mbunge kumesababishwa na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya umeme. Hata hivyo, kwa sasa tayari tathmini ya gharama za kupeleka umeme kwenye mitaa hiyo imefanyika na mitaa husika imewekwa kwenye Bajeti

ya *TANESCO* kwa mwaka huu wa fedha wa 2013/2014. Mradi huu unategemewa kuanza mwishoni mwa mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za mradi wa kupeleka umeme Gombe Kaskazini zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 161.3. Kazi za mradi huo zitahusisha:-

(i) Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa *kV 0.4* umbali wa Km 5.58;

(ii) Ufungaji wa *transfoma* moja ya *kVA 200;* na

(iii) Kuunganisha wateja wa awali 195.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za mradi wa kupeleka umeme katika mitaa mitatu ya Kata ya Iduda zinakadiriwa kuwa shilingi milioni 224.6. Kazi za mradi huo zitahusisha:-

(i) Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa *kV 33* umbali wa Km 1.5;

(ii) Ujenzi wa njia ya umeme msongo wa *kV 0.4* umbali wa Km 6;

(iii) Ufungaji wa transfoma moja (1) ya *kVA 200;* na

(iv) Kuunganisha wateja wa awali 175.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nilikuwa na maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Kata hizi zilizotajwa Kata ya Itezi mtaa wa Gombe Kaskazini, pamoja na Kata ya Iduda katika hiyo mitaa mitatu. Kata hizi mbili zote zimezungukwa. Sasa nilikuwa namwomba na ninamtaka Mheshimiwa Naibu Waziri, atupe majibu ni kitu gani kinachopelekea kwa Kata hizi ambazo zimezingirwa na umeme zisiwe na umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kama tunavyoelewa hizi Kata zote ziko katika Jiji la Mbeya na mimi nilifanya ziara katika Kata zote na huo sio umeme wa *REA.* Sasa nilikuwa nataka kujua Kata. Kwa mfano kama Kata ya Iganzo, Tembela, Mwasanga, Nzovye, Isalaga, Iziwa, Nonde, Nzoho zote hizi hazina umeme na ziko Jiji la Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Waziri angetueleza ni kitu gani kinachosababisha Kata zote hizi ambazo ziko Jiji la Mbeya kwa muda mrefu zisiwe na umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Dkt. Mwanjelwa, kwa namna anavyofuatilia miradi ya umeme Mbeya Mjini. Amekuwa akinifuatilia sana lakini

Dkt. Mwanjelwa anajua jitihada ambazo mimi na yeye tumekubaliana na tumefanya na hatua ambazo tumefikia kwamba mara kupatikana kwa fedha hizi ambazo tumezitenga, nikiri kabisa ni jitihada ya Dkt. Mary Mwanjelwa.

Nataka nikuhakikishie kwamba natambua Kata ya Itezi na Iduda zimezungukwa na umeme na tutajitahidi kuhakikisha kwamba fedha hizi zinapatikana kutoka kwenye Bajeti ya *TANESCO* na umeme unaenea katika maeneo yote ya Kata hizi.

Vilevile ni kweli kabisa Kata za Iganzo, Tembela, Nzovye na maeneo yanayozunguka Kata hizo kwa maana ya mitaa ile ya Mbeya na kwamba katika sera au sheria ya *REA* mitaa iliyoko mijini inahesabika kwamba ni mji. Kwa hiyo, haiwezi kushughulikiwa na *REA.*

Mheshimiwa Waziri aliwahi kutoa kauli hapa kwamba yako baadhi ya maeneo ambayo itabidi tuyaangalie kwa jicho tofauti kutokukumbwa na mfumo huo ambao kwa hakika zitakuja kupata umeme baadaye sana. Unaweza kukuta vijiji vya mbali vimepata umeme lakini mitaa iliyopo karibu na mjini haikupata umeme. Hili tunaliangalia tuonane Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa tuweze kuona namna gani tunaweza tukafanya katika eneo hili.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matatizo ya umeme yako makubwa sana ndani ya Wilaya ya Kilombero ambapo ni Wilaya yenye uzalishaji mkubwa wa umeme Kihansi na Kidatu. Kata mbalimbali za Wilaya ya Kilombero hazina umeme kabisa. Cha kushangaza hivi juzi tu pale Kata ya Kibaoni Makao Makuu ya Wilaya pamoja na kuwa kuna umeme, lakini ikaonekana kwamba wanaongeza mashimo mengine kuchimba waweke umeme wakati vijiji vya jirani kama Mlabani, Katitindiuka na maeneo mengine hakuna kabisa umeme.

Je, ni lini Serikali itawawezesha wananchi wa Wilaya ya Kilombero kupata umeme unaostahili ingawa ina mitambo miwili ya kuzalisha umeme ndani ya Wilaya hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunapata umeme katika Gridi ya Taifa na chanzo ni Kihansi na Kidatu. Ni kweli pia kwamba baadhi ya maeneo yaliyoko karibu kabisa na vyanzo hivi hayana umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tumeweka mpango wa kwanza ambao unahusisha Wilaya ya Mbozi na Wilaya ya Kilombero ni mpango maalum ambao tumefanya ni kama eneo la majaribio ambao unaweka umeme katika maeneo ya vijiji hivi vyote mpaka Kibaoni ambako anazungumzia Mheshimiwa Mbunge na tulishatoa majibu haya wakati wa Bunge la Bajeti na tulimpatia Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la

Kilombero ambaye nadhani mkiwasiliana kwa sababu mnahudumia wananchi mnaweza mkatupa mawazo yenu kama mnayo mawazo ya tofauti na hivyo.

**MHE. VITA R. M. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. Kwa kuwa tatizo hili la umeme kutofika katika baadhi ya maeneo ya mji linafanana na mji wa Namtumbo ambao umepata umeme, tunaishukuru sana Serikali. Kuna vijiji vinavyozunguka vya Libango, Minazini vya Luwinga na maeneo ya Namtumbo mjini nayo hayajapata umeme.

Je, Serikali inawahakikishia nao pia *TANESCO* watasambaza umeme katika vijiji hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli baadhi ya maeneo ya Namtumbo ikiwemo Lubambo na Luwinga yapo katika programu ambazo tunafikiria kwa sasa zinaweza zikatusaidia ikiwemo ni ya kupeleka umeme Namtumbo. Hata kama katika programu hiyo itakuwa imeshindikana, tunayo *REA PHASE III* ambayo inakuja, tunaamini kabisa tutaweka. Nikuhakikishie kwamba Lubambo na Luwinga ipo katika *REA PHASE II* na umeme wananchi watawekewa.

Na. 110

## Punguzo la Nguzo za Umeme

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA** aliuliza:-

Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ilitangaza punguzo kwenye nguzo za umeme:-

Je, utekelezaji wa punguzo hilo umefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotangazwa na Serikali ni punguzo la bei ya kuunganisha umeme na sio punguzo kwenye nguzo. Vifaa vinavyohusika katika kumpatia umeme mteja ni pamoja na nguzo, waya, mita ya umeme na vifaa vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, punguzo la gharama la kuunganishia umeme wateja lilianza kutekelezwa mwezi Januari, 2013 kama ilivyotangazwa.

Kwa mfano gharama ya kuunganisha umeme kwa umbali usiozidi mita 30 njia moja (*single phase*) bila kuhitaji nguzo, imeshuka kutoka shilingi 455,108 hadi shilingi 320,960 kwa mijini. Aidha, kwa wateja

wanaohitaji nguzo moja kuunganishiwa umeme, gharama imeshuka kutoka shilingi 1,351,884 hadi shilingi 337,740 kwa vijijini na shilingi 515,618 kwa mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini inawahamasisha wananchi, hasa wa maeneo ya vijijini, kutumia fursa hii muhimu kuunganishiwa huduma ya umeme na kuutumia kwa shughuli za kimaendeleo. *(Makofi)*

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Napenda kumwuliza Naibu Waziri masuala madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa baada ya punguzo hili kuna baadhi ya wananchi wanalalamika kwamba tangu walipie yapata miezi mitatu na zaidi hayajapata huduma hii ya kufungiwa umeme. Ningependa kujua tangu mtu alipie mpaka apate nguzo hiyo ni muda gani halisi unaotakiwa ili aweze kuendana na malipo sahihi? *(Makofi)*

(ii) Kwa kuwa Shirika la *TANESCO* kupitia Wizara ya Nishati na Madini linajiendesha kibiashara; na kwa kuwa mwananchi anapolipia gharama za umeme nia yake ni kupata umeme; na kwa kuwa Shirika hili linajiendesha kibiashara linapopata fedha kutoka kwa mwananchi anayelipia umeme tayari linajiendesha kwa shughuli zingine za uzalishaji. Ningependa kujua pale mwananchi anapocheleweshewa kufungiwa umeme na tayari ameshalipia pesa yake Serikali haioni

kuna haja sasa mwananchi huyo anapopata huduma ile kwa kuchelewa ili aweze kulipwa?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mteja anapolipia mpaka kuwekewa umeme hakupaswi kupita muda mkubwa sana kama ukizidi sana katika taratibu isiwe zaidi hata ya wiki mbili kwa sababu ya zile *logistics* na mambo mengine.

Kinachopelekea hapa ni kwamba tumekuwa na mafanikio makubwa sana katika kuwaunganisha umeme wananchi toka tulipotangaza kushusha kwa bei hizi. *Target* yetu ukiangalia toka mwezi Januari tulipotangaza hadi sasa tumeweza kuwafungia wateja zaidi ya 150,000 idadi hii ni kubwa ni tofauti kabisa na *targets* zilizokuwa zimewekwa. Tulichofanya sasa tume-*update* zile *target* na tumeagiza vifaa vya kutosha, sababu kubwa hapa ni vifaa ambavyo mchakato wake wa manunuzi na hili ni Shirika la Umma unatakiwa kwenda kwa mujibu wa sheria yetu ya Manunuzi.

Sasa kwa kuwa Shirika walikuwa wame-*target* kutokana na *policy* yake lilikuwa lime-*target* kiasi ambacho kimekuja kuwa zaidi sana. Kwa hiyo, kuanza tena mchakato wa manunuzi ilituchukua muda lakini nataka niwahakikishie kwamba baada ya muda tatizo hili litapungua kwa kiasi kikubwa sana.

La pili ni suala la kwamba wananchi *I mean* wateja wakishalipia na wakawa wamecheleweshewa

huduma hii je baada ya kuunganishiwa wanapata gawio lolote kutoka kwenye fedha walizoweka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ni kwamba biashara ya kisasa na kwa sababu umesema Mheshimiwa Mbunge kwamba *TANESCO* inafanya kazi kibiashara iko mikataba na mikataba. Sasa hapa kuna mkataba kati ya mteja na *TANESCO.* Katika mikataba hiyo hiki kipengele hakisemwi. Kwa hiyo niseme tu *position* ya sasa ni kwamba changamoto zitaendelea kuwepo tutachelewa kidogo na wateja wetu watuvumilie kwa sababu tuna nia njema kabisa ya kuhakikishwa kutoa huduma nzuri. Maana tumeji-*commit* kwenda kwa kiwango hicho. Shirika la *TANESCO* niseme tu kwamba ni Shirika linalofanya kazi kibiashara na sisi kama Serikali kazi yetu ni kulilea ili liweze kutimiza malengo yake. Tumefanya kazi hiyo na kwa hakika nawahakikishia kwamba ucheleweshaji mkubwa baada ya muda huu hautakuwepo. *(Makofi)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa fursa ya kuuliza swali la ziada.

Ningependa tu kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba katika Jimbo langu la Hai tatizo la umeme lina sura tofauti kidogo. Miundombinu ya umeme iliyopo imechakaa sana na kwa maana hiyo kuna maeneo ambayo nguzo za umeme zimeoza zinalazimika kukatwa na kuchimbiwa tena, zinakatwa na kuchimbiwa tena hadi kimo chake kimekuwa kifupi sana hali ambayo inahatarisha usalama wa raia.

Aidha, kwa upande mwingine kuna vitongoji vingi na vijiji vingi ambavyo havina umeme lakini katika sura ya kawaida inaonekana Wilaya nzima ya Hai ina umeme.

Mheshimiwa Waziri tatizo hili ni kubwa sana kiasi kwamba nikianza kuzungumza kijiji kimoja kimoja itakuwa ni kirefu sana. Ombi langu Mheshimiwa Waziri, utakuwa tayari kuja Wilayani Hai ili tukae na wahusika wote tuweze kuangalia namna ya kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli maeneo yaliyopata umeme miaka mingi iliyopita ni dhahiri kabisa vifaa vile vinatia changamoto ya wengine ambao hawajawahi kuwa na huo umeme. Kwa hivyo lazima tu-*balance interests*. Hata hivyo, nikubaliane na wewe kwamba kuna jambo linatakiwa kufanyika katika ku-*raise situation* ya sasa ya maeneo ambayo nguzo na vifaa vingi vinavyosafirisha umeme vimechakaa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutajaribu kuona ni namna gani tunaweza tukafanya na nikuhakikishie tu kwamba mimi kwangu hainipi tatizo lolote kuja nitakuja na ninaamini kabisa haya marekebisho tunayoyazungumza na maombi yako Mheshimiwa Mbowe Serikali ya CCM haina choyo inajua ina wajibu wa kutawala na unapotawala lazima uhakikishe kwamba unawahudumia wananchi na tunaendelea kufanya kazi hiyo kwa uaminifu mkubwa na tunaamini wananchi wanatuelewa. Mheshimiwa Mbowe

nitakuhudumia pamoja na Wananchi wa Hai kwa sababu ni jukumu la Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM). (*Makofi)*

Na. 111

## Kuyapima Maeneo ya Jeshi Yenye Migogoro

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM** aliuliza:-

Kwa muda mrefu Serikali iliahidi kuyapima maeneo ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) ambayo yana migogoro na wananchi kwa lengo la kutathmini na kutoa fidia kwa Wananchi waliochukuliwa maeneo hayo:-

Je, ni kwa nini utaratibu huo haukutekelezwa?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdalla Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwa muda mrefu Serikali iliahidi kuyapima maeneo ya Jeshi la Wananchi na Jeshi la Kujenga Taifa ambayo yana migogoro na wananchi ili kujua mipaka ya maeneo ya Jeshi na kiwango cha fidia kwa wananchi wanaomiliki maeneo yao.

Wizara yangu inahitaji shilingi milioni 526 kupima maeneo 80 na shilingi bilioni 85 kwa ajili ya kulipa fidia. Kutokana na ufinyu wa Bajeti zoezi hili limekuwa likitekelezwa awamu kwa awamu. Iwapo Wizara yangu itapatiwa fedha hizo maeneo yote ya Jeshi yenye migogoro yatapimwa na wananchi wanaomiliki maeneo hayo watalipwa fidia kama inavyostahili. *(Makofi)*

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Taarifa ya Ahadi za Serikali Bungeni ni ya mwaka 2007 Januari, ni miaka saba sasa Serikali iliahidi kuyapima maeneo mbalimbali kutathmini na kutoa fidia kwa wananchi waliochukuliwa maeneo haya. Sasa ni miaka saba na nimekuwa nikiulizia suala hili muda mrefu na mwaka 2008 Serikali ilisema kuwa, suala hili litakuwa ni historia na kuwa ndani ya mwaka 2009 maeneo hayo yatapimwa na fidia italipwa kwa wananchi.

Huu ulikuwa ni uongo kwa mujibu wa taarifa wa utekelezaji wa ahadi ya Serikali Bungeni. Kwa kuwa baadhi ya maeneo ambayo Serikali iliahidi kuyapima ni JKT Makutopora Dodoma, Rankoma JKT Mara, Chita JKT Morogoro, Tunduru *TPDF* Ruvuma, Biharamulo na Kagera. Mheshimiwa Waziri ninaomba uniambie, tabia hii ya Serikali kulidanganya Bunge na kutoa muda kuwa suala hili litatekelezwa kwa muda maalumu ni lini Serikali itaacha?

Katika majibu ya msingi yanasema kuwa Serikali inahitaji shilingi milioni mia tano ishirini na sita kuyapima maeneo na bilioni themanini na tano kwa kuwa mimi ni Mjumbe toka kipindi cha mwaka 2005 hadi leo na Serikali bado inaendelea kuyapima maeneo mapya tofauti na yale ambayo Serikali iliyaahidi.

(i) Je, kwa kuwa baadhi yawananchi waliochukuliwa maeneo yao wameshakufa; Serikali ina mkakati gani wa ziada?

(ii) Serikali ina kauli gani juu ya kuyapima maeneo yale ambayo walisema zamani na wanaendelea kuyapima maeneo mapya? Ninaomba majibu, ahsante sana.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza siyo nia wala siyo dhamira ya Serikali kuendelea kuwadanganya wananchi na kulidanganya Bunge. Ninakubali kuwa toka mwaka 2007, kama ulivyosema Serikali imekuwa ikitoa ahadi hiyo lakini kama nilivyosema tatizo kubwa siyo kutokuwepo kwa dhamira na nia ya kulipa na kutatua migogoro hii ya wananchi.

Tatizo kubwa tunalokabiliana nalo ni ufinyu wa Bajeti; kama nilivyosema, tunahitaji karibu milioni 86 hivi kwa ajili ya kupima na kwa ajili ya kulipa fidia kwa bahati nzuri sana Mheshimiwa Masoud wewe ni Mjumbe wa Kamati ya kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama.

Unajua kiasi cha fedha kilichotengwa ni bilioni tatu kiasi hicho bila shaka itakuwa ni kazi kubwa sana inahitaji weledi wa kiuchumi wa hali ya juu sana unapohitaji bilioni 86 ukapata bilioni tatu na ukaweza kutatua migogoro hiyo. Kama nilivyosema kupanga ni kuchagua mimi kama Waziri ninachokifanya kutokana na ufinyu huu wa Bajeti na kiwango kidogo hiki ni kuamua na kutatua migogoro hii awamu kwa awamu.

Mheshimiwa Mbunge, suala la pili kama ulivyosema hata pale ambapo wako baadhi ya wananchi ambao wanadai fidia na kwa bahati mbaya sana wamekwenda mbele ya haki, ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa haki yao haitapotea kwa sababu wanao warithi pale tathmini itakapofanyika bila shaka warithi wao watapewa haki hiyo, haki yao bila shaka haitapotea.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nilikuona ulikuwa umesimama Mheshimiwa Telele wengine wote wamesimama sasa hivi kwa hiyo utauliza Mheshimiwa Telele.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo vizuri wananchi kuendelea kuwa na migogoro na wanajeshi, wawe Jeshi la Kujenga Taifa au Jeshi la Wananchi ambao ni walinzi wa Taifa letu.

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kutafuta maeneo mengine na hasa katika Wilaya za mpakani ili kuwahamishia hawa wanajeshi na shughuli zao ili huko wanakopelekwa waende kuimarisha ulinzi

na usalama katika Wilaya za mpakani kama Ngorongoro?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Jeshi linapoamua kuchukua maeneo fulani kwa ajili ya shughuli za ulinzi na usalama wa nchi yetu wanafanya kazi hiyo kwa weledi na utaalamu. Pendekezo la Mheshimiwa Mbunge kuwa Jeshi liko kwenye maeneo fulani ambayo yameteuliwa kwa sababu hizo za mkakati halafu unapopendekeza wahame waende kwenye maeneo mengine ninadhani siyo suala la busara sana lakini ombi lake tunapaswa kulifanyia kazi.

Pale tutakapodhani kuwa kuna sababu ya kufanya hivyo tutafanya hivyo, pale ambapo hakutakuwa na sababu ya maana ya kufanya hiyo tutaendelea kubaki na kama kuna wananchi itabidi walipwe haki inayostahili kama nilivyosema kuwa dhamira ipo, nia ipo ya kuwalipa wananchi fidia stahiki. *(Makofi)*

Na. 112

**Serikali Kusaidia Shule za Wafugaji – Arumeru Mashariki**

**MHE. JOSHUA S. NASSARI** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikisaidia shule za jamii ya wafugaji katika maeneo ya Longido:-

Je, ni lini Serikali itaanza kusaidia shule zilizopo katika maeneo ya wafugaji wa Arumeru Mashariki?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba Waziri ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Joshua Nassari, Mbunge wa Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali imekuwa ikisaidia shule zilizopo katika jamii ya wafugaji ikiwemo Halmashauri ya Longido. Aina ya Msaada unaotolewa na Serikali katika shule za jamii ya wafugaji walioko katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido ni ujenzi wa mabweni na kutoa chakula kwa wanafunzi wa shule za sekondari kupitia fedha zinazotengwa kupitia Serikali Kuu. Wanafunzi wa shule za msingi katika Halmashauri hiyo wanapata chakula cha mchana kupitia Programu ya Chakula Shuleni inayotekelezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na *World Food Programme (WFP).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Meru inayojumuisha majimbo ya uchaguzi ya Arumeru Mashariki na Magharibi ina jumla ya shule za msingi 137 kati ya hizo shule za Serikali ni 111 na zisizo za Serikali ni 26. Halmashauri hii ina jumla ya shule 55 za sekondari kati ya hizo 29 ni za Serikali na 26 ni za binafsi. Aidha, shule 24 kati ya shule kati ya shule 137 za msingi na shule 6 kati ya 55 za sekondari za ziko kwenye

maeneo ya wafugaji katika kata za Ngarenanyuki, Mbughuni, Maroroni, Makiba na Songoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa elimu Bora inatolewa katika maeneo ya wafugaji wa Kata hizo tano, kati ya mwaka 2012 hadi 2013, Serikali imeajiri jumla ya walimu wa shule za msingi 73 na walimu 49 wa sekondari. Aidha, hata hivyo Serikali imejenga vyumba na madarasa 220 katika shule za msingi na vyumba 97 vya madarasa ya shule za sekondari kwenye maeneo ya wafugaji hao. Vilevile Serikali imejenga nyumba za walimu 73 kwa ajili ya walimu wa shule za msingi na nyumba 17 kwa ajili ya walimu wa sekondari. Sambamba na jitihada hizo katika kipindi cha Julai 2012 hadi Juni, 2013, Fedha za ruzuku ya uendeshaji wa shule *(Capitation Grant)* kiasi cha shilingi 108,986,445.01 zilitolewa kwa shule za msingi na shilingi 100,783,584 zilitolewa kama ruzuku ya uendeshaji kwa shule za sekondari. Vilevile jumla ya vitabu 6,883 vikiwemo vya Sayansi na Hisabati vimesambazwa kwenye shule za sekondari tangu mwaka 2011 hadi 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada hizi za Serikali katika kusaidia jamii ya wafugaji waliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru, kumekuwepo na Mashirika na Taasisi binafsi ambazo zimekuwa zikitoa misaada ya kuendeleza elimu katika shule za msingi na sekondari katika maeneo yafuatayo:-

Ujenzi wa vyumba vya madarasa, maktaba ya vyumba vya walimu, huduma ya maji, kutoa semina na

masomo, chakula kwa wanafunzi, sare za shule, malezi kwa watoto, matibabu kwa wanafunzi, sare za shule, vifaa vya shule, malezi ya watoto, matibabu kwa wanafunzi, wanaotoka kwenye mazingira magumu, kompyuta mpakato na *printer,* kugharamia ada za wanafunzi wenye mazingira magumu, kuweka umeme wa jua na wa upepo pamoja na ununuzi wa vitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mnamo tarehe 16 Mei, 2012 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi kwa kushirikiana na *WFP* na Halmashauri ya Wilaya ya Meru walitoa mafunzo ya uendeshaji wa mpango wa chakula cha mchana katika shule za msingi kwa uongozi wa Halmashauri, Waratibu Elimu Kata na Walimu Wakuu. Katika mpango huu shule 97 za msingi ya 111 zimenufaika kwa michango ya vyakula toka kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko katika mchakato wa kuanzisha Mpango wa Taifa wa Chakula cha mchana shuleni. Mpango huu utasaidia kuongeza uandikishaji, kupunguza mdondoko na kuongeza ufaulu hasa maeneo ya wafugaji pamoja na maeneo yenye ukame nchini.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, ningependa kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza:-

Mosi, kwa muda mrefu sasa tumekuwa tukiwekeza nguvu nyingi na tumehimiza wananchi kujenga shule

kwenye maeneo yote hususani jamii za wafugaji ambazo zinaoekana zilikuwa nyuma sana kielimu, wananchi wamejenga shule lakini kumekuwa na changamoto kubwa ya suala zima la chakula mashuleni tukizingatia kuwa hizi shule ni za jamii ya wafugaji na siyo za wakulima. Halmashauri imeshafanya *training* ya huu mpango wa utoaji chakula mashuleni lakini bado shule zangu zilizoko katika jamii ya wafugaji hazijanufaika na mpango huu. Wilaya ya Longido ambayo inapakana karibu kabisa na Wilaya ya Ngarananyuki wote ni wafugaji kwa maana ya Wamasai na Wameru ni watu ambao wana share kila kitu na *culture* zinafanana, sasa hawa wa Longido wanapewa chakula lakini hawa wa pembeni wa Arumeru hawapewi chakula ninaiomba Serikali kuwa ione kuna umuhimu wa kusaidia shule hizi ambazo ziko katika jamii ya wafugaji kwa sababu wafugaji wameamua kuuza mifugo na kupeleka watoto shule badala ya kuwapeleka machungani.

Swali la pili, shule ya Sekondari Kisimiri ambayo iko katika Kata ya Ngarananyuki ina kidato cha kwanza mpaka cha sita na ni shule ambayo iko katika jamii ya wafugaji kwa 100% na shule hii wazazi wamejitahidi wamepeleka watoto shule wamewa-*equip* na kwa mwaka juzi shule ilikuwa ni ya tatu kitaifa kwa shule za Serikali kwenye matokeo ya kidato cha sita. Shule hii iko mbali sana kutoka kwenye huduma kwa sababu iko ng'ambo ya pili ya upande wa pili wa *Arusha National Park*, yaani upande wa pili wa Hifadhi ya Taifa ya Arusha na Mlima Meru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanapata matatizo usiku endapo watoto wakiugua na kuna kidato cha kwanza mpaka cha sita.

**MWENYEKITI:** *Order, order.*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Anaamshwa *DMO* anapaswa kusafiri na gari lake la Idara ya Elimu, takribani kilomita 80 angalau kwenda kum-*rescue* mtoto kumpeleka hospitali kwa maana ya kumleta huku chini. Ninaiomba Serikali angalau gari moja au mawili kwenye hizi shule ambazo ziko kwenye jamii ya wafugaji ambazo ziko mbali na huduma ili wanapopata matatizo angalau waweze kufikia huduma kama Shule ya Kisimiri Juu?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza alielekeza kuwa Serikali inaonaje kusaidia masuala ya chakula cha mchana kwa watoto wa shule za msingi na sekondari, kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi ni kwamba Wilaya ya Arumeru tayari walimu na Waratibu Kata walishapewa semina ya namna ambavyo shirika hili la *WFP* tutakapokuwa tayari tumesharidhiana na Wizara ya Elimu tutaanza kutoa chakula cha mchana katika Halmashauri yake, kwa hiyo, kwa suala hili asiwe na wasiwasi.

Mwezi huu tarehe 16 - 20 Halmashauri yake ni moja kati ya zile Halmashauri ambazo waliomba wakaendelee kupewa maelekezo zaidi na kujifunza namna ya kushirikiana na hili shirika kutoa chakula, kwa

sababu ni lazima jamii husika waweze kuona namna ya kupata kuni, namna ya kujenga majiko, namna ya kulipa fedha za walinzi kwa sababu lile shirika linatoa chakula tu na siyo Halmashauri hizo tu ni pamoja na Halmashauri zote za Mkoa wa Arusha kwa ajili ya wafugaji na Mikoa kama ya Dodoma na Singida ambayo ni Mikoa inayotambulika nchini kama ni Mikoa yenye ukame. Kwa hiyo tutatoa semina hiyo halafu tutaanza kupata chakula.

Swali lake la pili kuhusu Shule ya Kisimiri ambayo iko Kata ya Ngarananyuki kwa ajili ya umbali wa shule, Mheshimiwa Mbunge ninataka kusema kuwa sina majibu ya moja kwa moja kuwa Serikali itaahidi hapa kuleta gari kwa sababu tulipoazimia kujenga shule za Kata hata mimi Jimboni kwangu ukienda kule Chunya kuna Kata inaitwa Ngwala. Kwa hiyo, kutoka Ngwala mpaka kuja Mjini Chunya ni karibia kilomita 250 ukizingatia na hiyo shule yako ambayo iko karinia kilomita mia moja na kitu. Kwa hiyo kwa ujumla hili ni suala la kitaifa kwamba Serikali ina shule karibia 4,600 tusingeweza kutoa magari kwenye shule zote kama ilivyokuwa zamani shule zilikuwa 500 ni chache sana tuliweza kuwapatia magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni changamoto ya Kitaifa ambayo tunaenda nayo lakini katika miaka inayokuja tutaendelea kuangalia changamoto na kutatua kwenye masuala yetu ya kielimu. Mheshimiwa Mbunge, nisingesita hapa kukupongeza kwa juhudi unazozifanya kwenye Jimbo lako. Mimi nimefika Shule ya Msingi Ngaboku mwaka jana, ni mbali sana kwa

wafugaji tulikuwa na shirika kutoka nchi ya Australia na Mheshimiwa Mbunge tulikuwa wote pale na ukaahidi kuwa utafanya Harambee kwa ajili kujenga shule ya sekondari kwa wafugaji.

Taarifa nilizonazo kutoka kwa Afisa ya Elimu ni kwamba umeshafanya Harambee na tayari shule hiyo inaendelea kujengwa kule Ngaboku. Mimi nikupongeze na uendelee hivyo hivyo na pia kuwahamasisha wafugaji wa maeneo yako kule waweze kujenga shule na waweze kupokea huu mradi wa chakula utakaokuja katika Jimbo lako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza la mwisho linatoka kwa mfugaji mwingine Ole-Sendeka.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa sababu ya msingi ya kufanya shule za wafugaji ziweze kupata huduma maalumu ya Serikali ni kutokana na jiografia ya umbali wanakoishi wafugaji na mahali shule zilipo; na kwa kuwa wafugaji wa maeneo hayo ya wafugaji kama ilivyo, Longido, Simanjiro, Monduli, Ngorongoro na maeneo mengine yanayofanana na hayo yakiwemo baadhi ya maeneo kama alivyosema Mheshimiwa Nassari kulikojengwa sekindari 16, lakini umbali kutoka shule hadi mahali wanapoishi wananchi ni zaidi ya kilomita 100.

Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuendelea na dhamira yake hiyo iliyoanza kwenye shule za msingi kusaidia baadhi ya shule za wafugaji ili gharama ipungue kwa wazazi wale ambao sasa wanabeba mzigo mkubwa wa gharama za mabweni katika hosteli hizo 16 za Wilaya ya Simanjiro?

**MWENYEKITI:** Ahsante majibu kwa wafugaji wengine wa Simanjiro.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninakubaliana na Mheshimiwa Ole-Sendeka lakini nimesema kwamba tarehe16 - tarehe 20 mwezi huu wa tisa hata Halmashauri yake ya Simanjiro ni miongoni mwa Halmashauri ambazo zitapokea semina kutoka kwa maafisa wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na hawa Shirika la *WFP* ili tuweze kupanga mkakati wa namna gani tunaendesha zoezi la kuwapatia watoto chakula kwenye shule za msingi na sekondari pia, lakini kuhusu Longido ni kama ni *unique* kwa sababu Mheshimiwa Rais alipotembelea Longido aliahidi kuwa tuwape chakula shule za sekondari na msingi kutokana na eneo lenyewe lilivyokuwa limekaa.

Sasa kama na maeneo mengine ya Simanjiro, Longido na Wilaya zingine ziko kama Longido ni suala la tu la Serikali kupokea ushauri na tuweze kuona kama tunaweza kufanya katika Wilaya zingine.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea tunahama kutoka kwa wafugaji na sasa

tunakwenda kwa wakulima. Swali namba 113 linaulizwa na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, kwa niaba yake ni Mheshimiwa Mchungaji Mwanjale, kutoka Mbeya hukohuko.

Na. 113

**Muswada wa Kudurusu Sheria ya Tumbaku**

**MHE. LUCKSON N. MWANJALE (K.n.y. MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA)** aliuliza:-

Je, Serikali italeta lini Bungeni Muswada wa kudurusu Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2001?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mbunge wa Lupa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kumi na Saba wa Bunge mwezi Novemba, 2009, Wizara yangu iliwasilisha marekebisho ya Sheria za Mazao Na. 20 ya mwaka 2009 *(Crop Laws (Miscellaneous Amendments) Act of 2009)* ili kutekeleza kikamilifu maamuzi ya Serikali kuhusu urasimishaji wa miundo, majukumu na ugharamiaji wa Bodi za Mazao nchini kwa kuzingatia maoni ya wadau wa tasnia ya tumbaku. Miongoni mwa Sheria zilizofanyiwa

marekebisho ni Sheria ya Tasnia ya Tumbaku ya mwaka 2001.

Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho katika Sheria hizo yalilenga kuwezesha wadau kushiriki kikamilifu katika kuendeleza mazao makuu ya asili, kwa maana ya *traditional crops,* likiwemo Zao la Tumbaku, kwa kutenganisha majukumu baina ya wadau ambayo ni majukumu ya usimamizi na uratibu wa zao, *regulatory functions,* yatakayotekelezwa moja kwa moja na Bodi na kugharamiwa kupitia Bajeti za Serikali na kutenganisha upande wa pili majukumu ya pamoja *(shared functions)*, yatakayotekelezwa na kugharamiwa na wadau wote ikiwemo Serikali yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa kurekebisha au kutunga sheria, unahusisha upatikanaji wa maoni ya wadau wa sekta au tasnia husika. Aidha, kwa sasa Wizara haijapokea mapendekezo ya wadau wa tasnia ya tumbaku kwa ajili ya kufanya marekebisho ya sheria hiyo. Serikali itakuwa tayari kuleta Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Tumbaku ya mwaka 2001 hapa Bungeni pale itakapopata mapendekezo ya wadau wenyewe na kuwepo kwa mazingira ya kufanya hivyo.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa jibu zuri la Serikali, lakini nina swali moja la nyongeza.

Kumekuwa na matatizo makubwa hasa kuhusu uteuzi wa Tumbaku pindi inapopelekwa katika masoko na kuwaletea usumbufu mkubwa sana wakulima wa zao hilo. Je, Serikali itaisaidia vipi Bodi ya Pareto ili iweze kuwaajiri *classifiers* wa Tumbaku?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri kutoka Tumbaku sasa kwenda kwenye Pareto. Haya ndiyo kilimo hicho hicho.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson Mwanjale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *problems* ya hawa *classifiers* ni jambo ambalo tumelizungumza mara kwa mara na nawashukuru Wabunge wanaotoka Mikoa inayolima Tumbaku, akina Mheshimiwa Vita Kawawa, akina Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Mwambalaswa na wengine, wamelizungumza. Tatizo ni kwamba, kwa sasa hivi *classifiers* tuliokuwa nao ni 20, mahitaji ya nchi nzima ni *classifiers* 40. Wakaguzi wa Tumbaku hawapatikani kirahisi rahisi. Wanatakiwa kukaa pale na kufanyakazi, nadhani kama miaka mitatu, minne, ili waweze ku-*qualify* kwamba ni *classifiers*. Kwa hiyo, tumekubaliana na Bodi kwamba, twende kwa awamu na ikiwezekana tuondokane na utaratibu wa kwamba wapitie kwenye Sheria za Utumishi ili tuwapate kwa haraka, kwa sababu wakulima wengi pamoja na kwako kule Mheshimiwa

Mwenyekiti, wanaumizwa kwa kukosekana kwa *classifier* wa kutosha.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Tanzania ni moja ya nchi ambazo zimepitisha Azimio la Kuridhia *WHO Framework Convention Tobacco Control* mwaka 2007; je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba yale Maazimio ambayo yapo katika Mkataba huu ambayo nchi yetu imeridhia yanatekelezwa nchini Tanzania?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa ufupi, Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ndugulile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni lazima tuseme ukweli; huu ni mgogoro unaotokana na Maazimio yaliyofikiwa na Wizara ya Afya na malengo ya Wizara ya Kilimo, kwa hiyo, inaonekana hapo palikuwa na mgogoro wakati hili jambo linasainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema kwamba, Zao la Tumbaku kwa hivi sasa ndiyo zao namba moja Tanzania, linaingiza dola milioni 250. Kweli tunatambua kwamba, Zao la Tumbaku lina mgogoro kidogo katika masuala ya afya. Kwanza, tukubaliane kwamba,

Watanzania siyo watumiaji wakubwa wa fegi kwa maana ya sigara. Kwa hiyo, sisi tuna-*export,* Wachina na Wajapani, wanaitaka tumbaku yetu, sisi tunakataa na hatujui familia 90,000 zinazolima tumbaku tutawapeleka wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema, wakati tunaangalia utaratibu wa kupata zao mbadala, haya tutakwenda tukiangalia, lakini kwa sasa hili ni zao ambalo linapeleka watoto shule na linalisha watu. Mimi nadhani kwa sasa pamoja na kwamba tumesaini huo Mkataba, lakini tuwafikirie zaidi wale wakulima 90,000.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata, linaulizwa na Mheshimiwa Halima Mdee, kwa niaba yake Mheshimiwa Silinde.

Na. 114

**Wadau Wanaoshiriki Mpango wa Kilimo Kwanza**

**MHE. DAVID E. SILINDE (K.n.y. MHE. HALIMA J. MDEE)** aliuliza:-

Serikali inao wadau mbalimbali wanaoshiriki katika mkakati wa Mapinduzi ya Kijani “KILIMO KWANZA”:-

(a) Je, ni vigezo gani vilitumika kuwapata wadau hao na kuingia makubaliano nao?

(b) Mmoja wa wadau wakubwa wa mkakati huu ni Kampuni ya Kimarekani ijulikanayo kama Monsanto.

Je, ni fedha kiasi gani Kampuni hiyo imewekeza katika mkakati huu na Kampuni ina jukumu gani mahususi katika mkakati wa KILIMO KWANZA?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vikubwa vya ushiriki katika ubia huu wa KILIMO KWANZA ni pamoja na kukubali kufanya jitihada katika kuongeza tija na uwekezaji katika kilimo. Mbili, kuzalisha kwa kutumia mbinu endelevu *(sustainable practices)* na kuwashirikisha Wananchi hususan Wakulima wadogo katika uzalishaji ili kutoa ajira na kupambana na umaskini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukubwa wa biashara zinazofanywa na Kampuni ya Monsanto hapa nchini, ni vigumu kufahamu moja kwa moja kiwango cha uwekezaji wa Kampuni hii katika utekelezaji wa azma ya KILIMO KWANZA. Hata hivyo, Kampuni hiyo ina mpango wa kuwekeza kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 50, ambapo kupitia Mpango wa Kuimarisha uwezo wa Wasambazaji wa Pembejeo, itatoa mafunzo kwa wataalam 600 wa kampuni binafsi katika Wilaya za Iringa, Kilolo, Njombe na Songea, miongoni mwa mambo mengine.

Kampuni hiyo pia itashirikiana na taasisi za kifedha ili kwezesha upatikanaji wa mikopo kwa Wakulima wadogo zaidi ya 200,000. Mikopo hii ni kwa ajili ya kuwasaidia katika uzalishaji na matumizi ya teknolojia bora za kilimo. Aidha, itasaidia kutoa mafunzo kwa Maafisa Ugani na Wakulima kuhusu hifadhi bora ya udongo *(Soil Conservation)* na mazingira. Hivyo, kwa mtazamo huu utaona kwamba, majukumu ya kampuni hii hayana tofauti na makampuni mengine yanayoshiriki katika utekelezaji wa KILIMO KWANZA.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Katika swali tumeuliza kuhusiana na vigezo vya Kampuni ya Monsanto. Tunataka tufahamu, Monsanto ni moja ya Kampuni ambayo inashiriki katika ubia wa *SAGCOT* lakini inapigwa vita sana Duniani kwa kuzalisha mbegu zenye sumu ambazo zina athari katika ardhi na kwa binadamu:-

(i) Je, sasa ni kwa nini Serikali iliingia ubia na kampuni hii haikuyaona hayo?

(ii) Kwa kuwa pamekuwepo na wadau mbalimbali ambao wanawekeza katika KILIMO KWANZA; je, ni kwa nini Sera ya KILIMO KWANZA mpaka sasa bado inasuasua?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa David Silinde, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako unisamehe, lakini kule Marekani, Dunia ya Wakubwa, kuna Jarida linaitwa *FORBES,* ambalo ndiyo linabaini makampuni makubwa Duniani. Mwaka 2009 *FORBES* ilii-*declare* Monsanto kuwa *company of the year*. Katika Makampuni makubwa Duniani kuna Monsanto, Unilever, Amagro, Syngenta, SAB MILLER, Diajo na Dumpot. Hao wote kwa kuitikia azma ya Mheshimiwa Jakaya Kikwete, wamekuja wamejiunga na *SAGCOT and these are the biggest companies in the world*. Sasa ukisimama ukisema wanapigwa vita; wanapigwa vita wanafanya biashara na nani? Isipokuwa kuna masuala ya uanaharakati, hiyo ni kweli kama katika *everything* kuna uanaharakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie kwamba, hapa Tanzania hivi sasa tuna mbegu za mahindi, pamba, mbegu za mafuta, matunda na mbogamboga, ambazo zinatokana na Kampuni hii ya Monsanto *today*. Sasa tunachofanya ni kwamba, wewe unachanganya vitu, kwa sababu hapa unazungumzia *genetically modified crops,* hilo ni suala lingine; lakini *as we speak,* tuna hizi *high value crops* ambazo mbegu zake zinatokana na Monsanto na haya makampuni mengine, maana kuna Syngenta ambao nao wanafanya kazi kama Monsanto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge aelewe kwamba, hawa Monsanto na wengine niliowataja, *these are multinationals*, ndiyo utaratibu wa kawaida, wanafanya huku wanapigwa vita na nini. Ukisema

wanapigwa vita Duniani, haiwezekani wakapigwa vita halafu wakawa na biashara hizi kubwa Duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la pili, nataka kusema kwamba, suala la Sera ya KILIMO KWANZA kusuasua labda tunalitazama kwa macho tofauti, lakini katika miaka mitano au miaka minne iliyopita, tangu Mheshimiwa Rais amezindua Mpango wa KILIMO KWANZA, hakuna zao hata moja ambalo halijaongezeka mara dufu. Tulikuwa tunalima mahindi tani milioni tatu, sasa hivi tunalima tani milioni tano, lengo ni kufika tani milioni saba. Tulikuwa tunalima tumbaku tani elfu hamsini sasa tunalima tani laki moja na thelathini na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo KILIMO KWANZA, kwamba, hatujafikia malengo makubwa hapana, tunakwenda mbele zaidi pamoja na kuwawezesha Wakulima wa Tanzania kuongeza tija, matrekta, matumizi bora ya mbegu na kadhalika. Hilo ni jambo ambalo mbali ya kuibeza Serikali, mimi nadhani ungeipongeza kwa sababu mafanikio ni makubwa sana.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Katika Sera ya KILIMO KWANZA, mojawapo ya vitu ambavyo vimebainishwa kama vipaumbele ni suala la upatikanaji wa soko la uhakika kwa wakulima. Katika msimu wa mwaka huu, Wakulima wa Zao la Mpunga

wameathirika sana na bei ndogo ya mpunga. Sasa hivi bei ya gunia moja la kilo mia moja linauzwa shilingi 25,000 wakati kuzalisha gunia hilo linamgharimu mkulima kati ya shilingi 30,000 mpaka 35,000. Je, Serikali wana mikakati gani ya makusudi na dhamira mahususi za kutatua tatizo hili haraka iwezekanavyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Haji Mponda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa anavyosema Mheshimiwa Dkt. Mponda hasa kwa wale Wakulima wa Ifakara, Mheshimiwa Susan Kiwanga amekuwa analisema, lakini Wabunge wa Bahi, Mheshimiwa Badwel na maeneo ya Shinyanga kwa Mheshimiwa Azza. Mpunga mwaka huu tumepata *a bumper harvest*, uzalishaji mwaka huu umekuwa mzuri kidogo. Jambo ambalo tunafahamu ni kwamba, uzalishaji wa mpunga wote unavunwa kwa wakati mmoja kwa maana ya Julai, Agosti na Septemba.

Sasa unapovuna mpunga wakulima wanakuwa wanao, kinachogomba ni hii *structure* ya ulanguzi, wanakwenda kununua mpunga kwa shilingi 25,000 au 30,000 ili mwezi Novemba, utakapokuwa umepungua wauze kwa shilingi 80,000 hadi 90,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulichosema ni kwamba, Serikali tumejitoa kwenye kupanga bei, lakini inabidi tuangalie tena mkakati huu na ninyi Wabunge

tutawaletea mridhie mkubali Serikali iingie kwenye maeneo fulani kumhami Mkulima. Bei ambayo inamfaa Mkulima naomba niseme na Watanzania wananisikiliza, ni kiasi cha shilingi 45,000 kwenda mbele, hiyo inakwenda kwa maana hata kwa vigezo vya *supply and demand*, hii shilingi 25,000 ni kuwanyonga Wakulima. Tunawaomba pia Wakuu wa Wilaya kwenye maeneo yale, waangalie uwezekano wa kudhibiti *entry* ya ulanguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Wakulima wenyewe nao waangalie, saa nyingine kwa sababu ya hali ya maisha na kadhalika, wanalazimika kuuza mpunga kwa bei hiyo. Nadhani tunatengeneza mkakati kwa Wizara mbalimbali pamoja na TAMISEMI ili kudhibiti hawa walanguzi wanapoingia wajulikane, wabainike na tujue kwamba, wananunua mpunga kwa bei hiyo, kwa sababu kwenye mahindi mwaka huu tumeweza, kwa hiyo, natarajia mfumo huo huo tutautumia kwenye mpunga. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Felister Aloyce Bura; Mheshimiwa Bwanausi kwa niaba yake!

Na. 115

## Kuandaa Utaratibu Unaofanana wa Ukokotoaji wa Hesabu za Mafao ya Wastaafu

**MHE. JEROME D. BWANAUSI (K.n.y. MHE. FELISTER A. BURA)** aliuliza:-

Kila Mfuko wa Hifadhi ya Jamii una utaratibu wake wa ukokotoaji wa hesabu za wastaafu, hali inayosababisha tofauti ya malipo kwa wastaafu waliokuwa wanalipwa mishahara inayolingana katika kipindi cha utumishi wao:-

Je, kuna utaratibu wowote unaoandaliwa na Serikali kuhakikisha kuwa ukokotoaji wa hesabu za wastaafu hao hautofautiani sana kutoka katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko ya Jamii inayohusika na ukokotoaji wa hesabu za wastaafu ni Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Umma (*PSPF)*, Mfuko wa Pensheni kwa Watumishi wa Serikali za Mitaa (*LAPF)*, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (*PPF)*, Mfuko wa Akiba kwa Watumishi wa Serikali

(*GEPF)* na Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*. Kila moja ya Mifuko hii ilianzishwa kwa Sheria yake na katika Sheria husika kuna Kanuni *(formula)* ya kukokotoa mafao ya mstaafu. Kwa kuwa kanuni za ukokotoaji hutofautiana kati ya Mfuko na Mfuko, hapana shaka hata mafao pia hutofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeunda Mamlaka ya Usimamizi wa Mifuko *(The Social Security Regulatory Authority - SSRA)*, ambayo katika majukumu yake ya jumla ya usimamizi wa Mifuko, hujumuisha pia uhuishaji wa uwiano wa ukokotoaji wa hesabu za mafao. Suala hili limefanyiwa kazi na *SSRA* na mapendekezo yake yamefikishwa Serikalini na linasubiri kibali cha Baraza la Mawaziri. Baada ya idhini ya Baraza la Mawaziri kupatikana, Serikali italeta Muswada Bungeni wa kufanyia marekebisho Sheria za Mifuko ili kukidhi hoja hiyo ya uwiano. Ahsante.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa ukokotoaji huu wa uwiano unasubiriwa kwa hamu sana ili uweze kutoa uwiano wa pamoja; je, Mheshimiwa Waziri anadhani mchakato huu ambao ameueleza utachukua muda gani ili huu Muswada uweze kuletwa na hatimaye Bunge liweze kuidhinisha?

(ii) Kwa kuwa wastaafu wengi wana maisha magumu sana kutokana na hali ya kipato chao cha posho kuwa ndogo sana, ikiwa ni pamoja na wazee ambao wanaishi katika mazingira magumu. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha inaongeza mafao haya ya wastaafu pamoja na wazee ambao wanaishi katika mazingira magumu?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bwanausi, kama ifuatavyo:-

Kuhusiana na ni lini mchakato huu utamalizika ili uletwe Bungeni, ningependa kurudia jibu nililolitoa nilipojibu swali la msingi kuwa, andiko la mapendekezo ya kuhusisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii limeshawasilishwa kwenye *Cabinet Secretariat* kwa majadiliano. Ninaamini haitachukua muda mrefu sana kabla halijafikishwa mbele ya Bunge kwa ajili ya kupitiwa. Kwa hiyo, nawaomba Wabunge na Wananchi wote kuwa na subira kwa sababu limeshafikia hatua nzuri kumalizika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na wastaafu pamoja na wazee wanaoishi katika mazingira magumu, tunatambua kwamba, kuna ugumu unaotokana na viwango vya pensheni inayotolewa sasa hivi. Kama mnavyojua, pensheni inatokana vilevile na uwezo wa Serikali kuongeza, kwa sababu tunapofanya hivyo inabidi pia tuwe tuna mapato ya kutosha kuongeza pensheni hiyo. Suala hili linaigusa

Serikali na tunaendelea kulifanyia kazi, jinsi gani tunaweza kuboresha hali hii. Kwa sababu hata hivyo, vyombo vilivyopo sasa hivi viliongezwa muda si mrefu sana. Tunalitambua hilo tatizo ni kubwa na tunaendelea kufikiria jinsi ya kulifanyia kazi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Marais Wastaafu na Mawaziri Wakuu, wao wanalipwa pensheni nzuri ndiyo maana hata Mheshimiwa Mrema sasa hivi anajikomba kwa Serikali ili na yeye aweze kulipwa pensheni nzuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, hebu rekebisha hayo maneno yako na uende kwenye hoja.

*(Hapa Wabunge fulani walipiga kelele)*

**MWENYEKITI:** *Order, order!*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namaanisha kwamba, anaeleza ili na yeye sasa aweze …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkosamali, naomba ukae kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu ndani ya Bunge. Swali lililopo hapa halihusiani na Mbunge mwenzako unayemtaja, naomba ujielekeze kwenye swali na siyo hayo unayoyasema.

*Order, order* ndani ya Bunge na ninaomba *Hansard* kwa mamlaka ya Kiti, huyo Mbunge aliyetajwa na maneno yaliyotajwa yafutwe kwa mamlaka yangu na ninaomba Mkosamali ujikite kwenye swali lako la msingi. *(Makofi)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Kwa kuwa Viongozi niliowasema wanalipwa vizuri. Sasa kwa nini Serikali isiboreshe pensheni za watu wa kawaida isiwe inaangalia watu wa juu peke yao?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu. Mheshimiwa Waziri hajajibu swali, hayo makofi ni ya nini. Hebu mpeni nafasi Naibu Waziri ajibu swali. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkosamali, kama ifuatavyo:-

Viongozi Wakuu Wastaafu wanalipwa viwango vya juu zaidi ya viwango vya pensheni vya wastaafu wa kawaida, kwa sababu kwanza ni mujibu wa Sheria tuliyoikubali sisi wenyewe kuwa walipwe. Vilevile hawa ni Viongozi ambao kwa muda waliokuwa wakihudumia, walichukua *risk* kubwa katika maisha yao kujitoa kwa ajili ya nchi hii.

Ukisema kuwa na wastaafu wengine wote wa Tanzania walipwe viwango vile, Serikali bado ndugu zangu haina uwezo. Wale tunaowahesabu ni wachache na pia wadhifa wao unahitaji iwe hivyo. Hata hivi sasa Wabunge wengine mlioko huku ndani, viongoni wenu wana heshima fulani kubwa zaidi kuliko sisi wengine. Lazima tukubali hizo *hierarchy* jamani.

Hatuwezi kuacha kuwa Viongozi wanakuwa na heshima fulani kubwa zaidi kuliko sisi, wengine hata umri tu wenyewe jamani utoshe. Mkosamali wewe unamsema Mzee Mrema hapa, kwa kweli mimi nimeona aibu sana kutokana na hadhi yake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nilishasema hilo ni swali la nyongeza la mwisho na nadhani wote mnajua hilo na hamkusimama wakati wa swali la msingi. Kwa hiyo, kwa mujibu wa utaratibu wa uendeshaji wa shughuli za Bunge, tunaendelea na swali linalofuata. Linaulizwa na Mheshimiwa Dkt. Henry Daffa Shekifu, kwa niaba yake Mheshimiwa Nundu.

Na. 116

## Udhibiti wa Maduka ya Fedha za Kigeni

**MHE. OMARI R. NUNDU (K.n.y. MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU)** aliuliza:-

Benki Kuu ya Tanzania ndiyo msimamizi mkuu wa Taasisi za Fedha nchini yakiwemo maduka ya fedha za kigeni hapa nchini:-

(a) Je, kuna maduka mangapi ya fedha za kigeni hapa nchini?

(b) Je, kuna utaratibu gani wa kuyakagua, kuyasimamia na kuhakikisha kuwa hayawi vyanzo vya kutorosha fedha za kigeni?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Henry Daffa Shekifu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi Januari, 2013, kulikuwa na jumla ya maduka ya fedha za kigeni 223 nchini; kati ya hayo, maduka 194 yapo Tanzania Bara na maduka 29 yako Zanzibar.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, maduka ya fedha za kigeni yanaanzishwa na kuendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Kigeni ya mwaka 1992, ambayo imeipa Benki Kuu ya Tanzania jukumu la kutoa leseni na kusimamia uendeshaji wa maduka hayo. Kwa mujibu wa Kifungu cha 5(a) na 7(1) ya Sheria tajwa hapo juu, Benki Kuu imetoa Kanuni za Uanzishaji na Usimamizi wa Maduka ya Fedha za Kigeni ya mwaka 2008 *(Foreign Exchange Bureau de Change Regulations, 2008).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa maduka ya fedha za kigeni hayawi vyanzo vya

kutorosha fedha za kigeni, wamiliki wa maduka haya lazima wazingatie masharti yote yaliyomo kwenye kanuni. Miongoni mwa masharti hayo ni pamoja na maduka yote lazima yaanzishwe kama Kampuni; yamilikiwe na kuendeshwa na Watanzania; yaanze na mtaji usiopungua shilingi 40,000,000; hayaruhusiwi kusafirisha fedha nje ya nchi; wanahitajiwa kuweka kumbukumbu ya mauzo na manunuzi kwenye kompyuta na kutoa stakabadhi inayochapishwa kutoka kwenye kompyuta inayoonesha muda wa mauzo au manunuzi ya fedha; kuwasilisha Benki Kuu taarifa za bei, kuuza na kununua fedha za kigeni kila siku na kila mwezi; na mwisho kuwasilisha Benki Kuu hesabu zilizokaguliwa kila mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuweka sawa kumbukumbu za waendeshaji wa maduka na kutengeneza mazingira mazuri ya kazi zao, Benki Kuu inafanya yafuatayo:-

Kwa maombi mapya ya leseni, waombaji wanatakiwa kuleta maelezo yao binafsi *(CV),* vyanzo vya mitaji yao, pamoja na rekodi ya malipo ya kodi kwa kipindi cha miaka mitatu, hutoa mafunzo ya kanuni za uendeshaji wa maduka ya uuzaji na ununuzi wa fedha za kigeni na kuwafanyia usaili wakurugenzi na waendeshaji waandamizi kabla ya kutoa leseni mpya. Kuongeza muda wa leseni baada ya kujiridhisha kuwa duka husika limetimiza kanuni za uendeshaji. Pia Benki Kuu hutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kudai stakabadhi za ununuzi na uuzaji wa fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakaguzi hupitia maduka yote kuangalia na kukagua utekelezaji wa kanuni za kuendesha maduka. Zipo adhabu kwa wanaokiuka kanuni, miongoni mwa adhabu hizo ni pamoja na onyo kali, faini isiyopungua shilingi 2,500,000; kufungiwa biashara kwa muda wa miezi mitatu hadi sita na mwisho, kunyang'anywa leseni kwa mujibu wa sheria.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Pamoja na majibu mazuri ya kina ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu swali hili, nina swali la nyongeza.

Biashara hii ina sehemu mbili; sehemu ya watoa huduma na sehemu ya wapokeaji huduma. Kwa wale wapokeaji huduma hasa ukizingatia tatizo ambalo limeenea duniani sasa hivi la kusafirisha fedha chafu, ni taratibu zipi zinachukuliwa kuhakikisha kuwa suala kama hilo halijitokezi? Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri mwenyewe!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa Mbunge, anauliza kwamba, taratibu gani zinafanyika na Serikali ili kuzuia fedha chafu

ambazo zinazunguka Duniani na sisi tusiwe sehemu ya mtandao huo. Mheshimiwa Naibu Waziri, anapojibu swali la msingi ameeleza kanuni iliyotayarishwa na Benki Kuu, inaeleza mambo gani ambayo ni muhimu kwa kila *Bureau de Change* iweze ku-*comply* na ameeleza mambo manane. Kwanza, ni lazima duka lenyewe liwe limeandikishwa kama kampuni. Pili, liwe linamilikiwa na Mtanzania ili iwe rahisi sisi kuwa-*control.* Tatu, aanzishe kwa mtaji usiopungua shilingi milioni 40. Nne, asipeleke hela yoyote nje ya nchi kama benki. Kipengele namba nne ni kikubwa, ambacho kinaifanya Benki Kuu katika kudhibiti kuhakikisha kwamba maduka haya hayajiingizi katika utaratibu wa kupeleka *cash* nje ya nchi kama zilivyo benki ambazo zina leseni ya kufanya kazi hiyo. Lazima watoe risiti na mwisho ni lazima wapeleke *audited accounts* Benki Kuu kila mwisho wa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Waziri vilevile ameeleza na haya ni majibu sahihi kwa swali hili la pili kwamba, kuna adhabu zilizopangwa. La kwanza, akiharibu kwa mara ya kwanza kuna onyo kali. La pili, ni faini isiyopungua *2.5 million.* Adhabu ya tatu ni kuhakikisha kwamba, kwa uzito wa kosa atakalokuwa amelifanya, anapata adhabu ya kufungiwa miezi mitatu mpaka miezi sita. Mwisho ni kufutiwa leseni kwa mujibu wa Sheria. Kwa hali hiyo, katika taratibu zote ni dhahiri kabisa Serikali ina mkakati na utaratibu wa kuzuia fedha chafu zisiwe sehemu ya mtandao katika Tanzania.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Benki Kuu ndiyo msimamizi mkuu wa Taasisi za Fedha; na kwa kuwa mtu yeyote anapokwenda kununua fedha katika Benki kama za *NMB* na *CRDB* inakuwa ni ghali sana kuliko *Bureau de Change;* na kwa kuwa unapokwenda kuuza fedha katika Benki za *NMB* unapunjwa sana kuliko *Bureau de Change;* kwa maana nyingine ni kwamba ni bora ukimbilie kwenye *Bureau de Change* kuliko benki zetu za *NMB* na *CRDB.*

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa!

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Je, ni Sera ya Benki Kuu na Wizara ya Fedha kuzi-*promote* zaidi *Bureau de Change* kuliko Benki za *CRDB* na *NMB? (Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mnyaa, kama ifuatavyo:-

Biashara sasa hivi ya fedha au vitu vingine vyovyote ni huria na ndiyo maana kuna aina mbalimbali za masoko ya fedha na vitu vingine kwa ajili ya watu kuchagua. Serikali imetoa wigo mpana zaidi

kwa mtu kuchagua wapi anataka kufanya biashara na wapi atapata faida zaidi, anavyojionea mwenyewe. Benki biashara yake kubwa siyo kuuza *forex,* kazi yake ni kuweka amana, kutoa mikopo na vitu kama hivyo. Kuuza *forex* au kupokea *forex* ni mojawapo tu ya biashara ambayo siyo *core business. Bureau* kazi yake ni kubadilisha fedha na ilitengenezwa hivyo makusudi mwanzoni kuhakikisha kuwa, mtu anayekuwa na fedha zake za kigeni nje, anataka kuzileta nchini au anataka kufanya biashara inayohusiana na fedha za kigeni, asipate shida ya kulazimika kwenda benki.

Wananchi hawafungwi kuwa watumie fedha yao vipi au wakachenji hela yao vipi, mradi tu yeye mwenyewe aone kuwa masilahi yake yako wapi. Benki Kuu wala Serikali, hai-*promote* shirika lolote. Vyombo vyote hivyo vipo pale kwa ajili ya kuwahudumia Wananchi na Wananchi wana jukumu la kuamua wenyewe wapi wakienda kubadilisha kuwasaidia zaidi au wakienda kuweka itawasaidia zaidi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata, litaulizwa na Mheshimiwa Omar Rashid Nundu!

**MHE. OMAR RASHID NUNDU:** Ahsante. Kabla sijauliza swali la nyongeza, kwa faida tu, swali langu la pili lililopita lilikuwa ni kuhusu wale wanaopokea huduma kuwa wanaweza kwenda *Bureau de Change* moja wakabadilisha kiasi kikubwa cha pesa wakaenda na wakaenda kwenye *Bureau de Change* nyingine wakabadili tena.

Wale ambao wanatoa huduma, *Bureau de Change,* taratibu ambazo Serikali imeziweka zinaridhisha, lakini wanaokwenda kupata huduma hiyo, wanaweza wakaenda sehemu mbalimbali na kubadilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hivyo, naomba sasa swali langu namba 117 lipatiwe majibu.

Na. 117

**Vituo vya Polisi Kuzinduliwa na Kubaki Wazi Saa 24**

**MHE. OMARI RASHID NUNDU** aliuliza:-

Pamoja na Polisi kufanya doria saa 24 bado ulinzi huo hautoshelezi; aidha, kwa kutokuwepo kwa vituo vya polisi vidogo au kukosekana kwa askari vituoni nyakati za usiku kama ilivyo katika Vituo vya Usagara, Raskazone, Bombo, Barabara ya 8, Kwaminchi, Duga, Kange na Michukuuni Jijini Tanga ulinzi unakuwa hafifu:-

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha kuwa Vituo vya Polisi vinabaki wazi saa 24?

(b) Je, ni lini Kituo cha Polisi cha Mchukuuni Kata ya Tangasisi kilichojengwa zaidi ya miaka kumi iliyopita kitazinduliwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua juhudi za Wananchi katika kujenga Vituo Vidogo vya Polisi nchini vikiwemo alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge. Chini ya Mpango wa Maboresho, Jeshi la Polisi linakusudia kupeleka huduma za ulinzi na usalama katika ngazi za Kata au Shehia ambako baadhi ya vituo vilivyojengwa na Wananchi vitatumika kama Vituo vya Polisi, sambamba na Ofisi za Polisi Jamii kwa manufaa ya Wananchi wa eneo husika kwa saa 24.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi Mchukuuni kilicho mbali na makazi ya Wananchi kilianza kujengwa mwaka 2000 na hadi bado hakijakamilika. Uzinduzi wa Kituo hicho utafanyika mara tu baada ya ujenzi wake kukamilika. Nitumie nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Mbunge, ashirikiane na wadau welevu kukamilisha ujenzi wa kituo hiki haraka ili kizinduliwe.

**MHE. OMARI RASHID NUNDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipouliza swali hili ilikuwa Julai, 2012, takribani mwaka mmoja umepita. Kilichojitokeza katika kipindi hiki, vituo ambavyo vimejengwa na Wananchi, ambavyo havina askari

vimeongezeka; kuna Mabokweni na kuna Kwamichi. Ninachotaka kusema hapa ni kwamba, Wananchi wanajenga lakini vituo hivyo havipatiwi huduma ambazo zinatakiwa. Hiki cha Mchukuuni kilipojengwa kilibaki bila huduma mpaka kikaota nyasi. Sasa nina maswali mawili ya nyongeza, pamoja na jitihada za Wananchi alizoziongelea Mheshimiwa Naibu Waziri:-

(i) Kwa kuwa miji yetu kama vile Tanga inakua kwa kasi kubwa na sehemu za makazi zinaongezeka pande zote za miji; ni hatua zipi ambazo Serikali yenyewe inachukua kuhakikisha kuwa kuna Ofisi za Polisi za kutosha katika makao mapya hayo sambamba na kuwepo ulinzi wa kutosha usiku na mchana?

(ii) Polisi wanafanya kazi nzuri sana, lakini wanapata changamoto nyingi sana; changamoto ya kukosa vitendea kazi na kupigwa kama ambavyo tumeshuhudia jana hapa. Sasa Serikali inafanya nini kufanya maisha ya Polisi yawe mazuri hasa ukizingatia kuwa Askari wadogo hawaendi likizo mpaka baada ya miaka mitatu, wanaenda likizo miezi mitatu mfululizo. Serikali haioni kuwa taratibu kama hizi zimepitwa na wakati sasa Askari hao waweze kwenda likizo kila mwaka kama wafanyakazi wengine kwa ajili ya tija ya kazi zao na ongezeko la ulinzi? Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kwamba, naomba kupitia hadhara hii, niwashukuru sana

Wananchi ambao wanajitokeza kujenga vituo katika maeneo yao. Niwaombe na niwahakikishie pia kwamba, vituo watakavyovijenga vitakuwa vya manufaa kwa kuongeza hali ya ulinzi katika maeneo yao. Vituo ambavyo vimejengwa na bado havina wafanyakazi kwa maana ya askari vipo na hivi karibuni tumeanzisha utaratibu mwingine katika kuhakikisha ulinzi jirani, ulinzi wa familia, unaimarika, kwa kutenga baadhi ya Askari kuhakikisha kwamba, wanaenda maeneo zaidi ya kwenye Kata kuliko pengine *concentration* nyingine. Kubwa katika kuhakikisha kwamba wanafanya kwa saa ngapi, inategemea pia hali ya uhalifu katika maeneo yale.

Nasikitika kwamba, kituo hiki ambacho amekitaja Mheshimiwa Mbunge, kilipata matatizo kwa sababu ujenzi wake haukuwa na mashauriano mazuri. Ukweli ni kwamba, kituo kilichojengwa na Wananchi kikawa hakifai kwa ajili ya shughuli za kiulinzi. Hapa tunatafakari tuone tutafanya nini ili tuweze kuongeza vigezo kiweze kutumika kwa ajili ya kujengwa kwake.

Kuhusu hali ya Askari na taratibu ambazo tunatakiwa tufanye ni kwamba, lengo la Serikali ni kuhakikisha Askari wanaishi katika hali nzuri na likizo ni haki yao. Kama nilivyosema kwenye jibu lililopita ni kwamba, bado tuna uchache wa Askari na pengine tuna nusu tu ya Askari tunaowahitaji. Kubwa hapa ni kuhakikisha kila mmoja wetu ni sehemu ya ulinzi na si sehemu ya kuwapiga Askari.

Na. 118

## Matukio ya Viongozi Kumwagiwa Tindikali

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH** aliuliza:-

Matukio ya kumwagiwa tindikali watu au viongozi wa nyadhifa mbalimbali yametokea mara kwa mara huko Zanzibar, mbali na tukio la hivi karibuni la mwaka 2012 la kumwagiwa tindikali Katibu wa Mufti, Ndugu Fadhili Soraga, yapo matukio mengine ya nyuma ambapo Ndugu Masoud Mohamed Shambi, aliyekuwa Afisa wa Tume ya Uchaguzi Pemba alimwagiwa tindikali mwaka 2000 na Ndugu Rashid Ali Juma aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa Zanzibar naye alimwagiwa tindikali mwaka 2011:-

Je, Serikali inaweza kuwaeleza Watanzania wahalifu waliofanya vitendo hivyo na hatua zinazochukuliwa dhidi yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2000 hadi 2012 na hata hivi karibuni, yametokea matukio kadhaa ya watu kumwagiwa tindikali. Tarehe 13 Novemba, 2000 saa 2.00 usiku, Ndugu Masoud

Mohamed Shambi, alimwagiwa tindikali kupitia dirishani akiwa nyumbani kwake eneo la Kisiwani kwa Binti Abeid, Wilaya ya Wete, Mkoa wa Kaskazini Pemba. Tarehe 17 Februari, 2011 saa 2.00 usiku, maeneo ya Uwanja wa Amani, Ndugu Rashid Ali Juma naye alimwagiwa tindikali. Aidha, tarehe 6 Novemba, 2012 majira ya saa 11.20 alfajiri, Barabara ya Msumbiji Mabata, Sheikh Fadhili Suleiman Soraga, Katibu wa Mufti wa Zanzibar naye alimwagiwa tindikali. Mara tu baada ya kupata taarifa za matukio haya, upelelezi ulianza na watuhumiwa wapatao 16 walikamatwa na hatua za kisheria kuchukuliwa.

Mheheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuanza kushamiri kwa matukio haya, Serikali imeanza kuchukua hatua madhubuti za kuhakikisha kwamba, tunayadhibiti. Wadau wa Jukwaa la Haki Jinai, walikutana na kuweka mikakati ya pamoja kupambana na matumizi haramu ya tindikali. Mikakati hiyo ina lengo la kudhibiti uagizaji, uhifadhi, uuzaji na usambazaji wa kemikali mbalimbali zikiwemo tindikali. Ni matumaini yetu kuwa, hatua hizi zitapunguza upatikanaji holela wa tindikali na kupunguza matukio ya kutumia tindikali kama silaha.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(i) Kwa kuwa malalamiko yaliyoko kwa Wananchi ni kwamba, uhalifu huu unatendeka, lakini

Vyombo vya Dola haviwakamati wahalifu na wala hawawafikishi katika Vyombo vya Sheria na kupatiwa adhabu mwafaka. Je, Serikali kwa kutumia dhana ileile ya uwazi na ukweli na kuongeza imani ya Wananchi kwa Vyombo vyao vya Dola, inaweza kuweka wazi watu hawa 16 ni akina nani na adhabu zipi za Kisheria wamepatiwa?

(ii) Baadhi ya watu waliomwagiwa tindikali ni Viongozi wa Serikali na Maafisa wa Chama cha Mapinduzi kwa upande wa kule Zanzibar; ni imani yangu kwamba, Vyombo vya Dola vinafanya utafiti wa kina wa matukio haya. Je, Serikali inaweza kueleza hapa ni nini sababu za uhalifu huu kuongezeka katika kipindi hiki?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba, Serikali inachukua hatua na imewakamata watu wote waliohusika na haya matukio ambayo yalitokea Zanzibar. Watuhumiwa sita walifikishwa Mahakamani katika tukio la Bwana Shambi na watuhumiwa wanne walihojiwa na kupelekwa kwa *DPP.* Aidha, tukio la Mheshimiwa Soraga, watuhumiwa wanne walifikishwa na jalada hilo bado liko kwa *DPP,* tunasubiri maelekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili kuhusu kiini; wahalifu wako *dynamic,* siyo teknolojia tu ambayo inabadilika, wahalifu nao wanabadilika na kwa bahati mbaya sana wamehisi pengine kwa kubeba silaha; panga, upinde, mshale, mkuki, ni rahisi kuonekana nia waliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya tindikali mpaka sasa yalikuwa ni silaha ambayo inafichwa na inafanywa kwa kificho kwenye vichochoro vya ajabu ajabu. Kwa hiyo, hii ndiyo sababu ya kuwa inaanza kutumika, lakini kwa nini inatumika, labda niseme kitu kimoja kwamba, inavyoonekana kuna mambo tofauti ambayo yanasababisha. Moja ni kwamba, kama hili suala la Ndugu Shambi, lilitokea wakati wa harakati za kisiasa na yeye alikuwa Mtumishi wa Tume ya Uchaguzi. Tunaamini kwamba, pengine suala lake lilihusika hivyo na hata upelelezi uliashiria kutokea hilo kwamba, pia tofauti za kisiasa zinatugawa na tunafanya mambo ambayo hayaeleweki.

Vilevile kuna matukio ya kawaida ya mahusiano ya watu kibiashara, kuna mahusiano ya kidini ambayo tumeshuhudia pia, baadhi ya watu wenye dini moja wanatofautiana kwenye baadhi ya mambo na wanahisi pengine wananyang'anywa Misikiti au Makanisa na haya ndiyo matatizo ambayo tunayaona yanachangia katika mambo haya.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda hauturuhusu, bado tuna maswali mawili. Tunaendela na swali linalofuata, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed!

Na. 119

## Kiwanda cha Urafiki

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Kumekuwa na viwanda na kampuni nyingi zimekuwepo hata kabla ya kuwepo kwa Sheria ya Ubia katika Sekta Binafsi, iliyopitishwa na Bunge Mwaka 2010, kikiwepo Kiwanda cha Urafiki:-

(a) Je, Serikali, haioni kuwa sasa ni muda mwafaka wa kubadilisha jina la Kiwanda cha Urafiki na kukiita Kiwanda cha Chuma Chakavu kwa sababu kilichobaki hapo ni *"Scrapers"* tu?

(b) Je, ni hasara kiasi gani Serikali inapata kwa Kiwanda hicho cha Urafiki?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haina mpango wa kubadilisha jina la Kiwanda cha Urafiki na kuitwa jina lingine. Aidha, siyo kweli kuwa kilichobaki Urafiki ni chuma chakavu, kwani Kiwanda hiki kinaendelea kuzalisha nguo kwa kutumia pamba

inayolimwa hapa nchini na kutoa ajira kwa wafanyakazi wapatao 851 hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2011 kiwanda kilizalisha nguo zenye mita za mraba milioni 1.904 na kupata jumla ya shilingi bilioni 4.823. Mwaka 2012 kiwanda kilizalisha mita za mraba milioni 3.9 na kuuza mita za mraba milioni 3.4 na kupata shilingi bilioni 6.7. Kuanzia mwezi Januari hadi Agosti mwaka huu wa 2013, jumla ya mita za mraba milioni 3.07 zilizalishwa na mauzo ya thamani ya shilingi bilioni 5.5 yamepatikana.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, hasara ambayo tunaweza kusema Serikali inapata ni kushindwa kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuongeza uzalishaji na ajira kutokana na kutokukamilika kwa sehemu ya pili ya usokotaji. Hata hivyo, juhudi zinaendelea za kuimarisha na kuendeleza uzalishaji, ambapo wanahisa, kwa maana ya Serikali ya Tanzania, pamoja na Serikali ya China, tumekubaliana kutafuta mwekezaji mwenye uwezo wa kimtaji, kiteknolojia na uzoefu katika sekta ya nguo na mavazi, ili aendeleze Kiwanda hiki cha Urafiki.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Kiwanda hiki kilikaa muda mrefu bila kufanya kazi, kuna taarifa kwamba, mashine za usokotaji za Kiwanda hiki ziliuzwa kama *scraper* bila utaratibu na hakuna hatua yoyote nyingine

iliyochukuliwa kwa kununua mashine nyingine. Je, Serikali ilichukua hatua gani dhidi ya wale wote waliohusika na uuzaji wa *scraper* hizi?

(ii) Kwa kuwa tatizo la kusuasua kwa uzalishaji katika Kiwanda cha Urafiki linajulikana; na kwa kuwa Serikali ina hisa kubwa katika kiwanda hiki. Je, ni kwa nini Serikali haiongezi nguvu kwa kuimarisha sehemu ya pili ya usokotaji, yaani *Spinning II,* ili kiwanda hiki kiweze kuongeza uzalishaji na ajira kwa vijana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, swali la kwanza analouliza Serikali imechukua hatua gani kwa waliouza mali hizo, nadhani chuma chakavu, za Kiwanda cha Urafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niwahakikishie Wabunge na Wananchi kwa ujumla kwamba, yule anayeuliza anataka kujua na mimi naomba nitoe taarifa hii sahihi ambayo ni nguvu kwa anayetaka kujua. Kwamba, Wizara yangu ilichukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kufuatilia uhalali wa kuuzwa kwa mitambo hii ambayo ilikuwa imekwishakuwa chakavu. Uuzwaji wa mitambo hiyo chakavu ulifanywa kwa njia ya mnada baada ya kupata ridhaa ya Bodi ya Kiwanda cha Urafiki. *Tender* ya kuuzwa kwa mitambo chakavu ilitangazwa kwenye magazeti tarehe tatu

mfululizo; tarehe 18 Agosti, tarehe 23 Agosti na mwisho ilikuwa tarehe 30 Agosti mwaka 2004. Mkataba wa Mauzo ulifanywa tarehe 6 Novemba, 2004 na mali ile iliuzwa. Fedha ambazo zilipatikana ziliingizwa kwenye akaunti ya kiwanda kwa matumizi ya kiwanda. Hata hivyo, ninasema kwamba, hiyo mali ambayo ilikuwepo imeshakuwa chakavu isingeweza tena kutumika, kwa sababu ya muda mrefu ambao ilitumika, ilikuwa haifai tena ndiyo maana ikauzwa kwa utaratibu ambao nimeshausema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuhusu kwa nini Serikali isiweke nguvu katika usokotaji ili kiwanda kiweze kuongeza uzalishaji na ajira. Napenda niseme kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, mkakati wa kuimarisha Kiwanda cha Urafiki unafanywa baina ya Serikali yetu ya Tanzania pamoja na Serikali ya Uchina. Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, juhudi zinaendelea za kuimarisha na kuendeleza uzalishaji, ambapo wanahisa wenyewe hawa wawili, Tanzania na China, tumekubaliana kutafuta mwekezaji mwenye uwezo wa kimtaji, kiteknolojia na uzoefu katika sekta ya nguo na mavazi, ili aweze kukiendeleza Kiwanda hiki cha Urafiki.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata na ndiyo la mwisho. Leo tunaahirisha Bunge ni bora tulimalizie swali la mwisho lililobaki. Mheshimiwa Kapt. Chiligati!

Na. 120

## Eneo la Mipaka ya Hifadhi – Wilaya ya Manyoni

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI** aliuliza:-

Kutokana na kuongezeka kwa wakazi kwenye Kata ya Chikola, Sasilo na Iseke, kulikosababishwa na wahamiaji wengi kutoka Mikoa ya Mwanza na Shinyanga, maeneo ya kilimo yamekuwa haba; na kwa vile asilimia 58 ya eneo la Wilaya ya Manyoni ni la Hifadhi (Lungwa, Muhesi na *Kizigo Game Reserves)*:-

(a) Je, Serikali iko tayari kurekebisha mipaka ya Hifadhi hiyo ili Wananchi wa Vijiji vya Imalampaka, Chisinjisa, Mpapa, Kitongoji cha Chilejeho, wapate eneo la kilimo na ufugaji?

(b) Askari wa Wanyamapori wamekuwa wakikamata mali zinazohisiwa kutoka kwenye maeneo ya hifadhi kama vile asali, mbao na kuwatoza faini wahusika, lakini hawatoi risiti; je, Serikali inasema nini kuhusu vitendo hivyo?

(c) Je, kwa nini Serikali haianzishi utaratibu wa kutenga maeneo ya Hifadhi Shirikishi *(WMAs),* kwenye Hifadhi za Wilaya ya Manyoni?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Captain John Zefania Chiligati, Mbunge wa Manyoni Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya Mapori ya Akiba ipo Kisheria na imezingatia mifumo ya kiikolojia. Idadi ya maombi ya wakazi kuongezewa ardhi hususan maeneo ya hifadhi, imeongezeka nchini kote. Hii inatokana na ukweli kwamba, wakazi wengi hasa wafugaji wamekuwa wakihamahama kwenda karibu na maeneo ya hifadhi ili kupata malisho ya mifugo na kilimo. Hii ni changamoto kubwa sana katika uhifadhi na imesababisha uharibifu mkubwa wa mazingira na migogoro mingi kati ya Hifadhi, Wafugaji na Wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia matakwa ya Sheria na kwa kuzingatia masilahi mapana ya uhifadhi endelevu nchini, Serikali inasisitiza kwamba, Wananchi wote wanapaswa kuheshimu mipaka ya maeneo yote ya hifadhi nchini na kwamba, ni marufuku kuvamia eneo lolote lililohifadhiwa Kisheria. Aidha, Serikali inasisitiza kwamba, Halmashauri zote nchini ni sharti kuwa na mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kukabiliana na changamoto za ongezeko la watu mijini na vijijini.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya mwaka 2009, utozaji wa faini yoyote unaofanywa na Askari wa Wanyamapori ni sharti uambatane na stakabadhi ya kukiri makosa. Aidha, Askari au Afisa Wanyamapori

anapotoza faini, anapaswa kutoa risiti kwa aliyelipa faini. Kila anayelipa faini ana haki na wajibu wa kudai risiti sahihi, ikionesha kiwango cha fedha ambacho amekilipa. Wizara yangu ina taarifa ya baadhi ya Askari Wanyamapori, ambao wamekuwa siyo waadilifu na hivyo kuikosesha Serikali mapato kwa kutoza faini mbalimbali bila kutoa risiti. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali itawatia nguvuni na kuwachukulia hatua za Kisheria Watumishi wake wote watakaopatikana na hatia hiyo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa ushirikishaji jamii katika uhifadhi wa wanyamapori, hususan uanzishwaji wa maeneo ya hifadhi ya wanyamapori *(Wildlife Management Areas)* katika vijiji ni moja ya utekelezaji wa Sera ya Wanyamapori ya mwaka 1998, kama ilivyokuwa *revised* mwaka 2007. Kwa mujibu wa Sera na Sheria ya Wanyamapori Namba 5 ya Mwaka 2009, *Wildlife Management Areas (WMAs),* huanzishwa katika maeneo ya ardhi za vijiji husika baada ya vijiji kufanya mpango wa matumizi bora ya ardhi na kutenga eneo ambalo watalitumia kwa ajili ya *WMAs.* Hatua za kufuata zimebainishwa katika Kanuni za *WMAs* za mwaka 2012, Kanuni ya 3 hadi ya 13. Aidha, Serikali ipo tayari kuwasaidia Wananchi wa Manyoni kwa kufuata hatua hizo ili waweze kuanzisha *WMAs* katika maeneo yao. Mwisho, Serikali inasisitiza kwamba, maeneo ya *WMAs* yanaanzishwa na ni sharti yaanzishwe katika ardhi za vijiji na si katika hifadhi zozote, ikiwa ni pamoja na *Game Reserve, National Park System* na *Game Controlled Area.*

**MHE. KAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Namshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa majibu yake, lakini nina swali moja dogo sana la nyongeza:-

Nakubaliana naye kwamba, Wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi siyo sahihi na haikubaliki. Kwa kuwa Wananchi katika Kata nilizozitaja wamekuwa wastaarabu, badala ya kuvamia wao wameomba, wameleta kilio chao kwa baba yao Serikali. Je, Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari baada ya Bunge hili kumalizika yeye na mimi twende katika maeneo hayo aone hali halisi na baadaye Serikali ichukue hatua kulingana na hali halisi?

**MWENYEKITI:** Majibu Naibu Waziri. Nadhani utafurahi kuongozana na Senetor Chiligati.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kapt. John Chiligati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, namshukuru sana kwa hizi jitihada anazofanya katika mazingira anayotoka na katika Jimbo ambalo lina eneo kubwa sana la uhifadhi, mapori ya akiba yale ambayo ameyataja. Tunafahamu changamoto ambazo zinatokana na ongezeko la ujangili na jinsi ambavyo ameshirikiana na wanakijiji wa maeneo haya na hasa wa Kata za Chikola, Sasilo na Iseke, katika kutusaidia

Serikali jitihada zetu za kupambana na ongezeko la ujangili. Changamoto ambazo zinatokana na ongezeko la watu, Serikali inazitambua na inaendelea na mashauriano ya namna kuliangalia kwa upana zaidi. Niseme tu kwamba, nitakuwa tayari kwenda katika Jimbo la Mheshimiwa Mbunge. Haitakuwa *immediately* baada ya Bunge hili, lakini nitahakikisha kwamba, tunapanga na yeye mapema iwezekanavyo na kwa vyovyote kabla ya Bunge linalofuata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, siwezi kuruhusu maswali ya nyongeza, muda umepita sana. Hata hivyo, kwa sababu leo ni siku ya mwisho, kwa kutumia mamlaka ya Kikanuni nikaona ni bora tumalize na hilo swali tusiliache.

Wageni waliofika Bungeni leo; Wanafunzi 67 kutoka Shule ya Sekondari ya *WAMA* Nakayama, iliyoko Nyamisati, Rufiji. Shule iliyoko chini ya Taasisi ya Wanawake na Maendeleo inayoongozwa na Mama Salma Kikwete, Mke wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Shule hii inachukua wanafunzi kutoka Tanzania nzima na gharama zote hutolewa na *WAMA.* Inasomesha watoto wa kike wanaoishi katika mazingira magumu. Wameongozwa na Mwalimu Ally na Mkuu wa Shule, Mama Mesa. Mama Mesa, tungeomba msimame na wanafunzi wote wa kutoka Sekondari hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mke wa Rais wetu, kwa kuona suala hili la kuwasaidia watoto wa kike na hasa walioko

kwenye mazingira magumu kwamba ni suala la kipaumbele. Tunawashukuru sana watoto wetu, jitahidini kusoma, maisha sasa hivi bila elimu hayana manufaa kwenu. *(Makofi)*

Wanafunzi 55 kutoka Shule ya Sekondari ya *Gift Skill,* Kibaha; ningeomba na wao wasimame. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hawa ni wanafunzi wetu wengine kutoka *Gift Skill* wamekaa katika pande tofauti ndani ya Ukumbi wetu wa Bunge. Kwa namna ya ajabu, hawa wanafunzi wote leo *uniform* zao ni nyekundu zinafanana na viti vya Ukumbi wa Bunge. Sasa sijui maana yake ni nini, lakini na ninyi karibuni sana. Wanafunzi wa *Gift Skill* Kibaha, kama nilivyosema jitahidini sana sana na elimu, hakuna jambo la msingi katika maisha yenu sasa hivi kama elimu, elimu ni ukombozi wenu. *(Makofi)*

Wanafunzi 100 kutoka Shule ya Msingi Amani Dodoma. Ningeomba na wao wasimame. Naona wameambatana na walimu wao, karibuni na ninyi pia. Bado mpo katika hatua ya mwanzo lakini tunamwomba Mungu awajalie afya njema, nguvu na uwezo muweze kufika na wengi wenu muweze kuwa Wabunge kama Wabunge mnaowashuhudia kwenye Bunge hili. Karibuni sana Wanafunzi wa Shule ya Msingi Amani Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pale kwenye *Gallery* ya Spika tuna wageni kutoka Chuo Kikuu ambacho kinaitwa *Barian Maritime University* cha Nchini China.

Hawa ni wageni wa Wizara ya Uchukuzi, wakiongozwa na Profesa Wang Zu; nadhani nimepatia hilo jina, ambaye ni Rais wa Chuo hicho Kikuu. Ningeomba Profesa asimame pamoja na wageni kutoka katika Chuo hicho Kikuu; *please, Professor could you raise up please* na wameambatana na ujumbe wa wenyeji wao ukiongozwa na Meja Jenerali Mstaafu Ligate Sande, ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya *Dar es Salaam Maritime Institute (DMI)* karibu sana. *(Makofi)*

Wageni kutoka Ubalozi wa Norway wako hapa nchini ambao ni Bi. Elizabeth Hansen, ameongozana na Bwana Alexander Mwalongo; karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni kumi na tano wa Mheshimiwa Kakoso kutoka Halmashauri ya Mpanda; karibuni sana ndugu zetu. Nafikiri hao ni Waheshimiwa Madiwani, basi tunawashukuru sana Waheshimiwa Madiwani, Mbunge wenu yuko imara ndani ya Ukumbi wa Bunge na ninaamini kazi hizo pia anazifanya vizuri akiwa huko Jimboni, mpeni ushirikiano wa kutosha kwa manufaa ya Wananchi wa Mpanda na kwa manufaa ya nchi yetu. *(Makofi)*

Wageni wanane kutoka Karagwe wakiongozwa na Ndugu Peter Kajura. Wageni kutoka Karagwe naona wao wapo katika Ukumbi wetu huo mwingine huko chini, kwa hiyo, tunawakaribisha sana. Naamini wananisikia na ni wageni wa Mheshimiwa Blandes hawa. Tunaomba mtambue uwepo wa Mheshimiwa

Blandes ndani ya Ukumbi wa Bunge na pia tunatambua kazi zake nzuri anazozifanya anapokuwa huko Jimboni. Tunawakaribisha tena siku nyingine muweze kuja kushirikiana nasi na salamu zao huko Karagwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dokta Khamis Kigwangalla, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa, leo tarehe 6 Septemba, 2013, saa saba mchana, kutakuwa na kikao katika Ukumbi wa chini ya Jengo la Ukumbi wa Bunge *(Basement)*. Kwa hiyo, Serikali za Mitaa mna kikao saa saba.

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya UKIMWI, naye anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane katika Ukumbi Namba 231, Ghorofa ya Pili. Mheshimiwa Mng'ong'o anaomba Wajumbe ya Kamati yake msikose kwenye kikao hicho.

Mheshimiwa Peter Msolwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo na Maji, anaomba Wajumbe wake wakutane saa saba. Naye anasema wakutane *Basement,* sasa kwa sababu Ukumbi ule ni mkubwa, mnaweza mkajipanga mkajua mnafanya kazi kwa utaratibu upi. Wajumbe wa Kamati hiyo na wao wahudhurie huko.

Mheshimiwa Bwanausi ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini

na yeye anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa saba katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge mliosimama, Mheshimiwa Said, Mheshimiwa Mnyaa, Mheshimiwa Chomboh, Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Mkosamali, Mheshimiwa Machali, Mheshimiwa Lissu, Mheshimiwa Mnyika, sawa nimewaona, Mheshimiwa Sendeka na Mheshimiwa Dokta Kigwangalla. Nimewaona wote nitawapa nafasi pale nitakapoona inafaa kuanza kuwasikiliza. Katibu tuendelee.

## KAULI ZA MAWAZARI

### Ukusanyaji wa Kodi za Magari kwa Kutumia Mfumo wa *MaxMalipo*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkutano wa Kumi na Mbili, tarehe 27 Agosti, 2013, katika kipindi cha maswali na majibu, ulitoa maelekezo kwa Wizara ya Fedha kuandaa Taarifa ya kina kuhusu hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Margaret Sitta, juu ya utaratibu, ufanisi na upungufu wa ukusanyaji wa kodi za magari kwa kutumia mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao ujulikanao kama *MaxMalipo.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni Taarifa ya Wizara ya Fedha kuhusu mfumo wa *MaxMalipo* pamoja na mifumo mingine inayotumika kukusanya ada za magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*, imeanzisha mfumo ambao umelenga katika kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ada za magari. Mfumo huu ulikuwa tayari tangu tarehe 9 Agosti, 2013 na ulianza kutumiwa rasmi na walipa kodi kuanzia tarehe 12 Agosti, 2013.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, endelea.

**MHE. TUNDU A. LISSU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna nakala, Kanuni zinataka tuwe na nakala.

**MWENYEKITI:** Nakala zinagawiwa, nimeshaletewa taarifa. Mheshimiwa Waziri, endelea!

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, malipo yote ya kodi za magari sasa yanafanywa kwa utaratibu wa mtandao kupitia njia mbalimbali. Njia hizi ni pamoja na simu za viganjani, Mabenki, Mawakala wa *MaxMalipo,* Tovuti ya Mamlaka ya Mapato *(Revenue Gateway System)* kama ilivyotangazwa kwenye Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha, pamoja na Ofisi za Shirika la Posta nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu mpya umeanzishwa kutokana na sababu mbalimbali kubwa ikiwa ni upungufu kwenye mfumo wa zamani wa kumbukumbu za taarifa za magari na malipo yake, lakini pia kero walizokuwa wanazipata walipakodi

wakati wa ulipaji wa ada hizi. Baadhi ya kero hizo ni kama ifuatavyo:-

(i) Msongamano mkubwa katika Ofisi za TRA ili kupata makadirio ya kiwango cha kodi kinachotakiwa kulipwa kwa chombo husika.

(ii) Msongamano mkubwa kwenye kaunta za benki kwa ajili ya kulipia ada ndogo ndogo za vyombo vya moto hivyo kusababisha walipa kodi wengi kutolipa ada hizo.

(iii) Kukosekana mfumo wa malipo ya mtandao hivyo kazi za uthibitishaji wa malipo kufanywa na watu walioajiriwa kwa ajili hiyo *(human intervention - manual work)* hivyo kusababisha hatari ya kufanyika makosa na upotevu wa mapato ya Serikali.

(iv) Kuibuka kwa matapeli wanaojifanya ni Wafanyakazi wa *TRA* (maarufu vishoka), waliotumia mwanya wa kukosekana mfumo madhubuti kuwalaghai na kuwaibia walipa kodi.

(v) Kero katika upatikanaji wa kadi za magari na vyombo vingine vya moto ambapo ilikuwa inachukua wastani wa siku saba kuzipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* ilifanya utafiti wa tatizo na changamoto za kulipa kodi hasa za magari na vyombo vya moto na kubuni mfumo wa kielektroniki ambao umelenga kutanua wigo wa njia za kulipia kodi, kwa

kuanzia na ada za magari. Hii inampa fursa mlipakodi kuchagua njia iliyo rahisi na nyepesi kutokana na mazingira atakayokuwa nayo kuweza kulipa ada yake. Mfumo huu sasa unamwezesha mlipa kodi kulipa ada ya gari bila kufika Ofisi za *TRA,* ambapo kwa sasa mlipakodi anaweza kutumia njia zifuatazo:-

(i) Simu za Viganjani *(M-Pesa, Tigo-Pesa, Airtel-Money, EazyPesa).*

(ii) Mabenki (Kwa sasa tuna *CRDB* na *NMB* wataanza hivi karibuni).

(iii) Mawakala wa *MaxMalipo.*

(iv) Ofisi zote za Shirika la Posta nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo huu mpya wa ulipaji ada za magari umethibitisha faida zifuatazo:-

(i) Mfumo huu ni rahisi kutumia na unapanua wigo wa kumwezesha mlipa kodi kulipa ada ya gari akiwa mahala popote nchini na wakati wowote, iwe usiku au mchana, kwa kutumia njia tofauti kama zilivyoainishwa hapo juu, hivyo unachochea makusanyo zaidi.

(ii) Utamwezesha mlipaji kuhakiki kiwango cha kodi anayotakiwa kulipa kwa kutumia simu yake ya mkononi, hivyo kupunguza mianya ya udanganyifu kutoka kwa watu wasio waaminifu.

(iii) Mfumo huu ni salama zaidi kwani taarifa za malipo zinatumwa kwenye Ofisi za *TRA* moja kwa moja *(Online)* na pia mlipa kodi anapelekewa ujumbe wa kuthibitisha kupokelewa kwa malipo aliyofanya kutoka *TRA.*

(iv) Mlipa kodi anaweza kulipa kodi yake kupitia njia mbalimbali mbadala kama vile kwenye mabenki, simu za mkononi, Mawakala wa *MaxMalipo* pamoja na Ofisi za Shirika la Posta nchi nzima.

(v) Mlipa kodi anakwenda kwenye Ofisi yoyote ya *TRA* kuchukua kadi yake, baada ya Ofisa wa *TRA* kuthibitisha malipo kwenye mfumo na kuangalia vitambulisho vya mhusika kama ndiyo mwenye gari.

(vi) Mfumo huu unaiwezesha Mamlaka ya Mapato kukusanya kodi kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha takribani wiki tatu, tangu mfumo mpya wa kodi za magari uanze rasmi tarehe 12 Agosti, 2013 mpaka kufikia tarehe 31 Agosti, 2013, yaani mwezi uliopita; kumekuwa na mafanikio mengi ya kujivunia ambayo matumizi ya teknolojia kwenye malipo na ukusanyaji wa aina mbalimbali za kodi umeleta ufanisi mkubwa. Mafanikio yafuatayo yamejidhihirisha:-

(i) Mfumo huu umeongeza wigo mpana wa ulipaji na urahisi wa kufanya malipo kwa walipa kodi. Kwa sasa njia mbalimbali za ulipaji wa kodi za magari kama nilivyoeleza, zinatumika ikiwa ni pamoja na *M-*

*PESA, AIRTEL MONEY, TIGO-PESA,* Benki ya *CRDB,* Wakala wote wa MAXMALIPO pamoja na Ofisi za Posta nchi nzima. Kwa kipimo cha muda wa majuma matatu, yaani tangu tarehe 12 Agosti, 2013 mpaka tarehe 31 Agosti, 2013 na ulinganifu wa kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha wa 2012/2013 (Wakati ukitumika mfumo wa zamani), mfumo huu umeongeza makusanyo kwa jumla ya Shilingi 1,016,232,109.05, ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 27 kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapa chini. Kwa kuwa Waheshimiwa Wabunge wana *details,* naomba uniruhusu niende ile inayofuata.

(ii) Mfumo huu, umepelekea idadi kubwa ya walipakodi kujitokeza kulipa kodi hii kwa hiyari ndani ya kipindi kifupi cha tathmini na hivyo kukuza tabia ya ulipaji kodi bila shuruti *(compliance level).*

(iii) Ukusanyaji mapato umeendelea kufanya vizuri na Jumla ya walipa kodi 23,680 walitumia mfumo huu na kiasi cha Shilingi 4,770,033,407 zimelipwa kupitia mfumo mpya kama inavyooneshwa na jedwali hapa chini kwa kuwa tena Waheshimiwa Wabunge wana jedwali hili, naomba uniruhusu niendelee namba tano.

(iv) Fedha hizi zinazokusanywa zinafika kwa wakati kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya matumizi maendeleo.

(v) Mfumo mpya umefanikisha ulinganifu na ukokotoaji *(reconciliation)* wa fedha za makusanyo kuwa mwepesi na hivyo kupelekea kuwapo kwa

usahihi wa mizania *(balancing)* ya fedha zinazokusanywa.

(vi) Mfumo umewaongezea wigo mpana wa sehemu za kuchukulia kadi, ambapo sasa walipa kodi wanaweza kuchukua kadi zao kwenye ofisi yoyote ya Mamlaka ya Mapato Tanzania tofauti na ilivyokuwa hapo awali.

(vii) Mfumo umewajengea walipakodi mazingira ya uaminifu mkubwa kwa malipo ya kodi kwani kwa sasa ulipaji unaweza kufanyika mtu akiwa popote bila mipaka na pia kwa muda wowote ambao mlipaji anauona utamletea ufanisi na wepesi katika ufuatiliaji. Hivyo, wale waliopo maeneo ambayo mabenki hayapo, bado wanaweza kulipia vyombo vyao na fedha kufika Serikalini kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kumekuwepo na changamoto za hapa na pale kama ifuatavyo:-

Changamoto ya kwanza, walipa kodi kutofahamu utaratibu sahihi wa kutumia njia mpya. Hatua ambazo *TRA* wamezichukua; *TRA* na makampuni ya simu wanafanya kampeni za elimu kwa walipa kodi kwa kutumia redio, runinga, magazeti, vipeperushi, michezo ya kuigiza na matangazo ya barabarani. Mamlaka ya Mapato inazungumza na makampuni ya simu ili kuweza kutumia ujumbe mfupi *(SMS)*, kwenda kwa watu wote wanaomiliki simu Tanzania kulezea taratibu

sahihi za mfumo mpya wa ulipaji ada za magari. *Vodacom* tayari wameanza kutoa matangazo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ni baadhi ya Mawakala wa *MaxMalipo* kwa wakati fulani kutokuwa na salio la kutosha kufanya malipo yanayohitajika. Hatua zinazochukuliwa na *TRA, MaxCom Africa Company* inayosimamia huduma za *MaxMalipo* imefanya zoezi la kuhamasisha mawakala wake hasa wale wanaotoa huduma hii kwa kiwango kikubwa kuongeza mtaji. *MaxMalipo* kwa kushirikiana na mabenki wameanza kutoa mikopo kwa mawakala ili pamoja na uhamasishaji kwa Mawakala kuwekeza zaidi. Kwa kuanzia, baadhi ya Mawakala wameanza kupatiwa salio la kutosha, yaani *float* kwa njia ya mkopo*. TRA* itaweka udhibiti na usimamizi kuhakikisha kunakuwepo na idadi sahihi ya mawakala ambao watavutiwa na kuwekeza zaidi katika biashara hii ili pia waweze kulipa kodi stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya tatu ni kuwa mfumo unatumia mawasiliano, wakati mwingine mitandao husika kutopatikana kwa walipa kodi. Hatua zinazochukuliwa kushughulikia changamoto hii, mazungumzo yamefanywa kwa watu, kwa watoa huduma za simu za viganjani kuboresha upatikanaji wa huduma hii. *TRA* imejizatiti hivyo kuweka mkakati wa kuingiza mabenki mengi zaidi kwenye mfumo mpya ili uwe mbadala pale panapokuwa na matatizo ya mitandao. Hivi sasa Benki ya *CRDB* imeshaunganishwa na matarajio ni kuiunganisha Benki ya *NMB* ifikapo

tarehe 16 Septemba, 2013. Hatua za awali za majaribio zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto namba nne, ni foleni ya kuchukua kadi kwenye ofisi za *TRA*. Kama nilivyosema *TRA* na Shirika la Posta Tanzania, wako kwenye mazungumzo ya kuweka mkakati wa kuwezesha mteja kuchukua kadi kwenye ofisi za Posta nchi nzima. Vile vile *TRA* itafungua vituo vyake vyoyr vya huduma nchi nzima yaani *Tax Service Centres* ili viweze kutoa huduma za kadi za magari. Hatua hizi zitapunguza msongamano kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Margaret Sitta alifika kwa mmoja wa Mawakala wa *MaxMalipo*, pale Mtaa wa Samora kwa huduma ya kulipia ada ya gari yake. Biashara ya Wakala huyo imesajiliwa kwa jina la *Dar News Stand,* ambaye anafanyia biashara zake Mtaa wa Samora karibu na ofisi za Mamlaka ya Mapato zinapofanyika shughuli za leseni za magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kuwa jirani na ofisi za Mamlaka, watu wengi wamekuwa wakienda kwake kwa malipo ya ada za magari pindi waambiwapo zinapokelewa na *MaxMalipo* pia. Mpaka tarehe 30 Agosti, 2013, yaani mwezi uliopita, yeye peke yake, yaani *Dar News Limited,* alikuwa ameshawahudumia walipa kodi 965 na thamani ya malipo aliyofanya ni sh. 148,095,600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichotokea wakati Mheshimiwa Margaret Sitta, anataka kutumia huduma hii ya *MaxMalipo* ni kwamba Wakala huyu *Dar News Stand* alikuwa yupo kwenye mchakato wa kuongeza *float* kwa njia ya benki kwa kuwa alikuwa ameishiwa baada ya mauzo mengi aliyokwishayafanya kabla ya hapo. Hivyo kupelekea kushindwa kumhudumia Mheshimiwa Sitta kwa wakati husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Mheshimiwa Margaret Sitta alishauriwa kutumia njia mbadala kwa maana ya *M-Pesa, Tigo Pesa, Airtel Money, CRDB Bank* au wakala mwingine wa *MaxMalipo*. Kwa hali hiyo, tunamwomba radhi Mheshimiwa Margaret Sitta na tunamhakikishia kwamba hatua zimechukuliwa kama tulivyoeleza hapo juu na hata pia hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na kampuni ya *MaxMalipo* ni pamoja na hizi zifuatazo:-

(i) Uongozi wa *MaxMalipo* umewatambua Mawakala na kutathimini biashara katika huduma ya kulipa kodi ya magari. Mpaka tarehe 30 Agosti, walikuwa wameanza kutoa huduma hiyo nchi nzima, kwa idadi walikuwa 323 mpaka tarehe tajwa hapo juu. Mawakala hawa wanatoka katika maeneo mbalimbali na mikoa tofauti ya Tanzania.

(ii) *MaxMalipo* imeanza kuwapa *float* ya biashara mkopo kwa wale ambao tathmini imeonesha wanahitaji kusaidiwa zaidi

kutokana na namna wanavyofanya biashara na kutoa huduma za ada za magari wakati mchakato wa kibenki ukiendelea.

(iii) Ni *Max Com* imeanza mazungumzo na benki mbalimbali ili ziweze kuwakopesha mitaji kwa ajili ya Mawakala wote wa malipo wanaoendesha biashara zilizosajiliwa kisheria.

(iv) *TRA, Max Com* na Kampuni za Simu wameanza kwa pamoja kutoa elimu zaidi kwa walipa kodi na jamii kwa ujumla kuwa, malipo ya kodi yanalipwa kwa kupitia njia mbalimbali zifuatazo: *M-Pesa, Airtel Money, Tigo Pesa, Ezy* Pesa, Benki, Mawakala wa *MaxMalipo* pamoja na ofisi zote za Shirika la Posta Tanzania.

(v) *MaxMalipo* baada ya tathmini itahakikisha huduma za Mawakala wake wote zinatolewa katika ofisi au maduka ya Mawakala ambayo ni rasmi kibiashara. *(Makofi)*

(vi) Max malipo itadhibiti mwenendo wa kifedha wa Mawakala wake hasa kwenye uwekezaji mtaji na utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni ya *MaxMalipo* ni kampuni ya Kitanzania iliyoanzishwa na vijana wa Kitanzania iliyopo chini ya mpango wa Serikali wa kukuza ubunifu na matumizi ya Sayansi na Teknolojia, yaani Dar es Salaam Teknohama *Business Incubator*

wenye mantiki wa kuendeleza nchi kwa kutumia teknolojia chini ya Tume ya Sayansi yaani *COSTECH*. Kampuni ya *MaxMalipo* imefanya vizuri toka kuanzishwa kwake. Baadhi ya mafanikio, naomba niyasema kama ifuatavyo:-

(i) Imeajiri wafanyakazi 85 moja kwa moja na 6,000 kupitia Uwakala. Malengo ni kutoa ajira zaidi ya 20,000 ifikapo 2014 yaani mwaka kesho kwa mtu mmoja mmoja na kwa vikundi vya wajasiriamali.

(ii) *MaxMalipo* imetengeneza mfumo madhubuti wa malipo ya *electronic* na inafanya kazi na Mashirika ya Serikali na Binafsi kama vile *TANESCO, TTCL, NSSF, DAWASCO, UWASA*, Wizara ya Ujenzi *(TEMESA), Ferry* ya Magogoni Kigamboni, Vodacom, *Airtel, Tigo, Zantel* na *DSTV* kwa uchache.

(iii) *MaxMalipo* imevuka mipaka na kwenda Rwanda na Burundi na inaendelea na nchi nyingine katika kupanua wigo na pia kuunga mkono juhudi za kuimarisha Jumuiya ya Afrika Mashariki.

(iv) *MaxMalipo* ilitambuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa Mkutano wa *SMART Partnership dialogue* iliyofanyika mwaka huu kwa ubunifu wao na ufanyaji kazi makini.

(v) Kwa kutumia mifumo yake imefanikiwa kuongeza makusanyo katika taasisi na mashirika yote inayofanya kazi nayo hasa kwa kupanua wigo wa makusanyo na malipo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni hii inaungana na Kamati ya Bunge ya kusimamia Mashirika na Taasisi za Umma, kuhusu matumizi ya mfumo wa *electronic* wa makusanyo na udhibiti wa makusanyo wa Wizara na Mashirika ya Umma katika kuzuia mianya ya upotevu na kuboresha makusanyo. Kampuni hii ya *MaxMalipo* imeshiriki katika maonyesho katika Viwanja vya Bunge mara mbili kuonesha mfumo wake wa kudhibiti mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa taasisi mbalimbali zimekuwa zikishirikiana kibiashara na *MaxMalipo* zile nilizozitaja na nimezirudia hapo chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa basi, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge waunge mkono juhudi za Mamlaka ya Mapato Tanzania kwenye maboresho ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali na kurahisisha namna za malipo kwa manufaa ya Taifa na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ningependa kutoa rai kwa Waheshimiwa Wabunge kuunga mkono na kuwapa moyo vijana wetu wa Kitanzania kama hawa wa *MaxMalipo* wanaojitokeza na kuonesha

juhudi katika kuleta ufumbuzi wa matatizo tuliyonayo bila kuwa na utegemezi wa wataalam kutoka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi!

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 2 Septemba, 2013, Kiti chako kiliiagiza Serikali itoe maelezo kuhusu mgomo wa wafanyakazi wa *TAZARA* ambao umedumu takribani kwa wiki mbili kuanzia Ijumaa tarehe 13 Agosti, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgomo huo wa wafanyakazi wa *TAZARA* uliitishwa na Chama cha Wafanyakazi wa Reli Tanzania *(TRAWU)*, kudai malimbikizo ya mishahara yao yote ya mwezi Mei, Juni, Julai na sasa Agosti, 2013. Mgomo huo unawahusu wafanyakazi wa *TAZARA* kwa ngazi isiyokuwa ya Menejimenti, aidha, hauwahusu wafanyakazi wa *TAZARA* upande wa Zambia, pamoja na kwamba hata wao wanadai malimbikizo ya mishahara kwa miezi niliyokwishataja, lakini wanafanya hivyo kwa njia ya majadiliano na menejimenti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba mgomo huo umefanyika nje ya taratibu za kisheria kwani hakukuwepo mazungumzo yoyote ya awali kati ya uongozi wa *TAZARA* na Chama cha Wafanyakazi

wa Reli Tanzania *(TRAWU)* na kutangazwa rasmi kwa mgogoro, Serikali iliyatambua maumivu ya wafanyakazi, hivyo kuagiza hatua zozote zile dhidi ya wafanyakazi waliogoma zisichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye Menejimenti ya *TAZARA* ikawasilisha kwa Serikali zote mbili za Zambia na Tanzania, taarifa ya hali halisi ya mamlaka hiyo, mahitaji yake ya dharura na ya vipindi vya muda mfupi, kati na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, picha halisi ambayo Serikali zote mbili zimeipata, ni kwamba, pamoja na ongezeko la kuridhisha la mzigo unaopitishwa kwenye reli hiyo sasa, bado mapato ya mamlaka ni madogo kuliko matumizi. Kwa mfano, katika miezi sita iliyopita, mapato ya mamlaka yalikuwa ya wastani wa dola za Kimarekani milioni 1.53 kwa mwezi, wakati matumizi yalikuwa wastani wa dola za Kimarekani milioni 2.5 kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ikumbukwe kwamba mishahara na mafuta peke yake vinachukua wastani wa dola za Kimarekani milioni 1.9 kwa mwezi na sehemu inayobaki ni matumizi mengine ya uendeshaji. Hivyo basi, pamoja na msukumo mkubwa wa Serikali zote mbili wa Menejimenti ya *TAZARA* kuongeza ufanisi na tija ndani ya mamlaka, bado umuhimu unajitokeza kwa Serikali zetu mbili kuiongezea *TAZARA* nguvu zaidi ya kifedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majadiliano ya muda mrefu na Waziri mwenzangu mwenye dhamana ya Uchukuzi wa Zambia, Mheshimiwa Yamfwa Mukanga, Serikali ya Zambia imeshatuma dola za Kimarekani milioni tano ambazo tayari zimeshapokelewa na Menejimenti ya *TAZARA*. Aidha, Serikali ya Tanzania imetoa shilingi bilioni mbili kama fedha za dharura kwa *TAZARA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zilizopatikana pamoja na dola za Kimarekani milioni 3.17 ambazo *TAZARA* inadai kutoka kwa wateja wake mbalimbali, zinatosha kabisa kurejesha hali ya kawaida katika mamlaka hiyo. Hivyo basi, Serikali inaiagiza Menejimenti ya *TAZARA*, kudai madeni yote kutoka kwa wadaiwa wake haraka iwezekanavyo ili fedha itakayopatikana iingie mara moja kwenye matumizi ya mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari wafanyakazi wameshalipwa mshahara wa mwezi Mei, 2013 na ifikapo Jumatatu, tarehe 9 Septemba, 2013 watakuwa wameshalipwa mishahara yao yote ya mwezi Juni, Julai na Agosti, 2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nilizozipokea sasa hivi hapa, ni kuwa, fedha yote inayotosheleza mishahara ya Juni, Julai na Agosti, imeshapelekwa benki kuanzia jana, hivyo kazi iliyopo sasa hivi ni ya kibenki tu ya kuingiza fedha kwenye akaunti za wafanyakazi wote Tanzania na Zambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, mategemeo ya Serikali ni kwamba, wafanyakazi wote wa *TAZARA* wawe wamerejea kazini siku ya Jumatatu, tarehe 9 Septemba, 2013 bila kukosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgomo huo umesababisha treni 13 zenye mabewa 252 ambayo yamebeba mzigo wa tani 10,000 kukwama njiani. Mzigo huo ni pamoja na tani 3,600 za shaba, tani 630 za *manganese*, tani 3,015 za mbolea, tani 500 za saruji, tani 1,170 za mafuta na tani 1,665 za bidhaa mchanganyiko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo, zaidi ya wakazi 46,000 wa Dar es Salaam wameathirika vibaya kwa kukosa huduma ya treni ya mjini waliyoizoea kuanzia siku hiyo ya mgomo. Aidha, abiria 24,000 wenye tiketi wakiwemo watalii, walikosa huduma ya usafiri wa treni na *TAZARA* ikalazimika kuwarejeshea nauli abiria hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya hasara ambayo *TAZARA* imepata mpaka tarehe 5 Septemba, 2013 ni zaidi ya dola za Kimarekani milioni 1.4. Serikali hivyo basi, inawahimiza wafanyakazi wa *TAZARA* kurejea kazini bila kukosa siku ya Jumatatu, tarehe 9 Septemba, 2013, asubuhi na kuchapa kazi kwa bidii ili kufidia hasara iliyopatikana katika kipindi hiki cha mgomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali zetu mbili zimeiagiza Bodi ya Wakurugenzi ya *TAZARA* kukutana mapema iwezekanavyo kwa ajili ya maandalizi ya

kikao cha Baraza la Mawaziri ndani ya mwezi huu Septemba, 2013 kutafakari hali iliyojitokeza na kuchukua hatua stahili za pamoja ili hali hiyo isijitokeze tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Waziri wa Uchukuzi na wewe kwa taarifa hiyo.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

***Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2013 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments)(No.3) Bill, 2013)***

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

*(Muswada uliotajwa hapo juu Ulisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

***Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2013 (The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2013)***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge jana tulimaliza uchangiaji, sasa nitawaita watoa hoja ili

waanze kujibu hoja zao, Naibu Waziri dakika 20 na baada ya Naibu Waziri ataingia Mheshimiwa Waziri.

Waheshimiwa Wabunge nilishawaona na nimeshawaambia nitawapa nafasi, ngojeni tufanye kwanza kazi, Mheshimiwa Naibu Waziri dakika zako 20!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba nami niweze kuchukua fursa hii kuchangia Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza na kumshukuru kipekee Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Mathias Chikawe, kwa uongozi wake na maelekezo ambayo ananipa mara kwa mara na kwa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa namna alivyoshiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa kuandaa Muswada huu ambao umewasilishwa katika Bunge lako Tukufu na kwa maelezo yake ya ufafanuzi aliyoyatoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ya kuhakikisha

kwamba Muswada huu unafikia hatua ya kuwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kipekee kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kuuchambua na kuuboresha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ulioko mbele yako, umefanyiwa marekebisho yatokanayo na maoni na ushauri wa Kamati hii. Kamati hii imechangia sana katika kuboresha Muswada huu kwani baada ya kuratibu maoni ya wadau mbalimbali, waliyafanyia kazi maoni hayo na kuja na mapendekezo ambayo Serikali imeyazingatia katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kipekee napenda kuwashukuru wajumbe wote wa Kamati, lakini pia Waheshimiwa Wabunge wote kwa namna ambavyo wamechangia Muswada huu na kwa maoni na ushauri ambao wameutoa katika kusaidia kuboresha Muswada huu*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na deni kubwa nisipotoa pongezi za kipekee kabisa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuridhia mchakato huu wa mabadiliko ya Katiba. Kuwepo kwa mchakato huu na sheria hii tunayoifanyia marekebisho leo hii, ni matunda ya uongozi wake na sina mashaka

kabisa kwamba historia itamtunuku tuzo njema, kwa kupanua demokrasia na uhuru wa watu katika utawala wake ikiwemo kupatikana kwa Katiba iliyoshirikisha wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na uzoefu wa nchi nyingine, mchakato wa Katiba nchini mwetu umekuwa wa wazi, uhuru na shirikishi kutokana na utashi wa Mheshimiwa Rais mwenyewe usiotiliwa shaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sote tumeshuhudia utashi huo, pale aliporuhusu mchakato wa mabadiliko ya Katiba, lakini zaidi pale alipoonesha utayari wa kukutana na Vyama vya Siasa, Asasi za Kiraia na makundi mbalimbali kupokea manung'uniko juu ya sheria iliyopitishwa na Bunge na hatimaye Muswada huu kurejeshwa Bungeni kwa marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utashi huo unaweza kuoneshwa tu na mtu mwenye busara, mtu mwenye hekima, mtu mwenye moyo wa uzalendo na mapenzi mema kwa nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo fursa adimu mbele yetu ya kutafsiri ndoto zetu juu ya Tanzania tunayoitamani. Tanzania yenye neema tele, Tanzania yenye fursa na ustawi wa kila Mtanzania bila kujali rika, jinsia, hali ya kipato au elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato huu wa Katiba ni njia yenye uhakika ya kutufikisha huko. Ikiwa sote lengo letu ni kufika kenye nchi ya ahadi, hatuna

sababu ya kufarakana ili hali sote tuna lengo la kujenga nchi yetu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia na dhamira ya Mheshimiwa Rais na Serikali yake ni njema na tungetegemea Kambi ya Upinzani nayo kuonesha nia njema vivyo hivyo. Hatuna budi kuaminiana na kushirikiana katika kufanikisha jambo hili jema kwetu sote. Sisi sio Watanzania wa mwisho kuishi, wala nchi hii si yetu peke yetu, bali kizazi chetu tumepewa dhamana ya kuwaandalia wanaokuja mbele yetu, nchi yenye amani, utulivu, ustawi na maendeleo. Tusikubali kupoteza fursa hii adimu, tuongozwe na nia njema na lengo kuu ambalo ni kujenga Tanzania tunayoiamini na kuitamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niruhusu niweze kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ya kisheria na tafsiri kama ambavyo imeibuliwa na Waheshimiwa Wabunge. Wapo Waheshimiwa Wabunge waliozungumzia utaratibu ambao wao wanafikiri ni vema ungefuatwa ili kuboresha Muswada huu. Aidha, wapo Waheshimiwa Wabunge waliotoa mapendekezo ya kuboresha Muswada, lakini pia wapo Waheshimiwa Wabunge waliotoa tahadhari kwa baadhi ya masuala. Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru sana kwa michango yenu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali yetu ni sikivu, kwa kiasi kikubwa tumezingatia mapendekezo hayo ya Waheshimiwa Wabunge katika Muswada huu.

Kwanza, kabisa hoja ya kwanza iliyotolewa na Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge wa Viti Maalum, ambaye alitaka kufahamu ni kwa nini nafasi za juu za uongozi katika Bunge Maalum, hazitokani na sifa bali kubadilishana baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa suala la Katiba ni suala la Muungano, ni muhimu upatikanaji wa Katiba hii mpya, ukatekelezwa kuzingatia pande zote mbili za Muungano. Kubadilishana katika nafasi hizo hakuondei umuhimu wa suala za sifa za uongozi kuwepo. Vilevile viongozi wote hawa wawili waliotajwa, wanaopendekezwa wana sifa za kuliongoza Bunge Maalum, lakini si hiyo tu, sifa za mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti zitaanishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili iliyotolewa na Mheshimiwa Ester Bulaya, ilikuwa ni kwamba, Spika naye aweze kufikiriwa kuwa Mwenyekiti wa muda. Ni maoni ya Serikali kwamba, kumfanya Mheshimiwa Spika kuwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum, ni kumnyima fursa na haki yake ya kugombea nafasi ya Uenyekiti wa Bunge Maalum, endapo atapenda kugombea nafasi hiyo. Aidha, ni mapendekezo yetu kama Wizara kwamba, Makatibu wanaopendekezwa, wanao uzoefu wa kutosha kuratibu na kusimamia uchaguzi wa Mwenyekiti wa Muda wa Bunge Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu kuhusiana na aya (e) ya Jedwali la Marekebisho kwamba, haitoi

muda wa mapumziko iwapo theluthi mbili ya wajumbe wa Bunge Maalum haitapatikana kutoka katika kila upande kabla ya kupigiwa kura nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Betty Machangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaamini kwamba utaratibu wa namna ya kupiga kura kama kama ulivyoainishwa katika kifungu cha 26 cha Sheria mama, utaanishwa katika Kanuni za Bunge Maalum. Hivyo, endapo itaonekana kwamba kuna haja ya kuweka muda wa mapumziko kati ya kipindi kimoja cha kupiga kura na kipindi kingine cha kupiga kura, basi tunaamini ni vyema utaratibu huu ukaainishwa katika Kanuni za Bunge Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nne ilitolewa na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mbunge wa Same Mashariki, ambaye alishauri kwamba katika kifungu cha 24(4), ni vema Serikali isijifunge katika uteuzi wa watumishi kwa kuteua tu watumishi wa Bunge pamoja na Baraza la Wawakilishi. Mapendekezo haya ya Mheshimiwa Mbunge tunayapokea, Katibu wa Bunge Maalum na Naibu wake naamini watazingatia hilo katika uteuzi wa watumishi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, taasisi ambazo Mheshimiwa Mbunge amezipendekeza kuongezwa ni taasisi za Umma, ambapo kama ambavyo mnaona katika Muswada au jedwali la marekebisho, tayari kama Serikali tumezingatia katika kifungu hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ilitolewa na Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yussuf Masauni, ambapo ilipendekeza kwamba, katika uteuzi wa Wajumbe wale 166 wa Bunge Maalum, ni vema uwiano wa kijinsia ukazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Masauni kwa namna ambavyo anatetea ukuzaji wa uwiano wa kijinsia. Pendekezo hili tumelizingatia katika mapendekezo ya marekebisho ya kifungu cha 22(2)(b) ambapo katika mapendekezo ya marekebisho ambayo tumewasilisha, ni kwamba wakati Mheshimiwa Rais anateua wajumbe wale 166 wa Bunge Maalum, atazingatia suala la jinsia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine iliyotolewa na Mheshimiwa Masauni ni kwamba, katika kifungu cha 22(1)(c), kiongezwe kifungu kidogo cha (9) ambapo ni vyema Rais asibanwe, aweze kuwa na uwezo wa kuchagua hata nje ya majina matatu aliyowasilishiwa endapo katika yale majina matatu anayowasilishiwa na taasisi itaonekana waliowasilishwa hawana sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunaona kwamba, siyo vema kuingiza pendekezo hilo katika sheria kwani linakiuka misingi ya uwazi ambayo inapendekezwa na sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mbunge wa Mbozi, kuhusiana na

Mwenyekiti wa muda kuwa Mwenyekiti wa Bunge Maalum. Tunaamini kwamba, kumruhusu Mwenyekiti wa Muda kugombea nafasi ya Uenyekiti inaweza kumsababishia kushindwa kusimamia uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum kwa haki na uwazi kwa vile yeye mwenyewe atakuwa na masilahi binafsi kwenye uchaguzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya nane iliyotolewa na Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari ambaye alipenda kufahamu lini Kanuni za Bunge Maalum la Katiba zitapitishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka, 2013. Katika kifungu cha 22A(1)(a) kama kinavyopendekezwa na Serikali, kinampa mamlaka Mwenyekiti wa muda wa Bunge Maalum pamoja na mambo mengine, kusimamia uandaaji na upitishwaji wa Kanuni za Bunge Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tisa iliwasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, ambaye alipendekeza kwamba ni vema siku 20 za nyongeza za muda wa uhai wa Bunge Maalum zisitajwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii tumeizingatia katika Muswada wa Sheria hii na tunamshukuru kwa kuliona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kumi, ni hoja iliyowasilishwa na Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Muhammad Chomboh, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Stella Manyanya na Mheshimiwa Adam Malima. Waheshimiwa Wabunge hawa, waliridhia kwamba idadi ya Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba iendelee kuwa 166, nasi tunaafiki na tunawashukuru sana kwa kuliona hili, maelezo marefu zaidi atayatoa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hii imezingatiwa kama hoja ya kumi na moja. Wabunge Mheshimiwa Pindi Chana, Stella Manyanya, Mheshimiwa Muhammad Chombo, Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Anne Malecela, nao pia walielezea Mamlaka ya Rais ya kuteua wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba aendelee kuwa na mamlaka hayo. Tunawashukuru pia kwa kuliona hili, hawa ndiyo wanatambua demokrasia, haiwezekani ikawa kwenye nyumba kila mtu ukamwachia afanye anavyotaka, bado Mheshimiwa Rais ndiyo baba wa nchi hii, bado ndiyo kiongozi wa nchi, bado anatakiwa kuwa na Mamlaka ya kufanya uteuzi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kuhusiana na sifa za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum kuainishwa kwani siyo kila mtu anaweza kuongoza Bunge Maalum la Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili kweli na hoja hii tumeizingatia katika Muswada wa sheria hii. Aidha, sifa

na vigezo zaidi zitainishwa kwenye kanuni za Bunge Maalum la Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kumi na tatu iliwasilishwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, kuhusiana na ushiriki wa Shirikisho la wafanyakazi na kwamba ni muhimu sana ushiriki wao ukaingizwa katika sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulihakikishia Bunge lako kwamba, hoja hii imezingatiwa katika Muswada wa Sheria chini ya kifungu cha 22(1)(c)(vi).

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako na kwa kutumia muda vizuri kabisa. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri ili aje kuhitimisha hoja yake. Mheshimiwa Mathias Chikawe!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kwanza, kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, kwa kunipa uhai leo hii nikasimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili niweze kihitimisha hoja ambayo niliiwasilisha ndani ya Bunge hili hapo juzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru wewe na Mheshimiwa Naibu Spika, kwa jinsi mlivyoweza kuliendesha Bunge hili kwa umakini na

umahiri sana, umahiri wa hali ya juu, mpaka leo tumefikia hatua ya kuweza kuhitimisha hoja yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, nichukue nafasi hii nimshukuru Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Fredrick Mwita Werema kwa ushirikiano wake mkubwa sana aliouonesha kwangu na kwa watendaji wengine katika Wizara yetu, mpaka sasa tumeweza kufanikisha hoja yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia, Naibu Waziri wa Wizara wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Angellah Kairuki, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Wizara hii na ninyi wenyewe mmejionea jinsi alivyowasilisha hapa na kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Ni mtu mahiri, ni mtu anayechapa kazi sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na kushukuru, nimshukuru sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana. Mheshimiwa Chana ni mahiri sana, ni Mwenyekiti hodari, Mwenyekiti anayejua kazi yake. Kwangu mimi siku zote nasema yeye ndiyo Mwenyekiti wa Bodi yangu na mimi ni Mtendaji Mkuu. Wanayoagiza karibu yote tunayatekeleza na kwa kweli ameonesha umahiri mkubwa sana kwa alivyoshughulikia Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja naye nimpongeze pia, Makamu wake Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, naye alishika kiti hiki mara kadhaa,

ametuendesha vizuri sana sana. Kupitia hao wawili niwapongeze pia wajumbe wote wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri sana waliyofanya, kwa uongozi wao mahiri na kwa kweli kwa ushauri ambao wamekuwa wakitupatia mara kwa mara mpaka tumefikia hatua hii. Nawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwasahau Waheshimiwa Wabunge ambao waliamua kuja kwenye Kamati hii na kutoa michango yao ya mawazo, nayo imetusaidia sana. Nimtaje mmojawapo Mheshimiwa Ester Bulaya, mara nyingi sana amekuja kutoa maoni yake na kushiriki nasi japo yeye si mjumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwapongeze Wabunge wote hawa waliokuja wakatusaidia na sasa tumefikia hatua hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umechangiwa na Wabunge 38; Wabunge waliozungumza walikuwa 23 na Wabunge 15 walichangia kwa maandishi. Utaniruhusu niwataje maana hawa wametoa mchango muhimu sana na vizuri basi wakafahamika kwa mchango wao jinsi walivyoutoa. Waliotoa kwa kuzungumza walikuwa ni Mheshimiwa Dkt. Pindi Hazara Chana, Mheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Augustine Mrema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa na neno la kusema kuhusu Mheshimiwa Augustine Mrema hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Adam Malima, Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Suleiman Nchambi na Mheshimiwa Betty Machangu. Mheshimiwa Betty Machangu, naye pia alikuwa anakuja katika vikao vya Kamati hii wakati naamini siyo Mjumbe wa Kamati hii, lakini ametusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Juma Mkamia, Mheshimiwa Subira Mgalu, Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, Mheshimiwa Mary Mwanjelwa, Mheshimiwa Dkt. Khamis Kigwangalla, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Mohamed Chomboh, Mheshimiwa Livingstone Lusinde, Mheshimiwa Kapteni John Komba, Mheshimiwa *Engineer* Stella Manyanya, Mheshimiwa Riziki Lulida, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Godfrey Zambi, Mheshimiwa Said Nkumba na Mheshimiwa *Engineer* Hamad Masauni. Hawa ndiyo waliotoa michango yao kwa kuzungumza hapa ndani ya Bunge, nao nawapongeza sana na nawashukuru kwa michango yao mizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kabla hujaendelea naomba nitambue uwepo wa Mheshimiwa Shibuda ndani ya Ukumbi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa unaweza kuendelea.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nautambua uwepo wake Mheshimiwa Shibuda ni mtu mahiri, ni mtu *independent,* ni mtu mwenye kujua kuchagua upi ...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri samahani, naomba pia nitambue na uwepo wa Mheshimiwa Mwatuka yupo ndani ya ukumbi huu. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwatuka alikuwepo hata jana na yeye namtambua, ni dada yangu lazima aje kuniunga mkono, namshukuru sana kwa kuwepo kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni wafuatao:-

Mheshimiwa Faith Mitambo, Mheshimiwa Omary Badwel, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari, Mheshimiwa Abdusalaam Amer, Mheshimiwa Shaffin Sumar, Mheshimiwa Nassib Suleman Omar, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Innocent Kalogeris, Mheshimiwa Hussein Mussa Mzee, Mheshimiwa Kidawa Salehe, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Sara Msafiri, Mheshimiwa Augustino Masele, Mbunge wa Mbogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndiyo waliochangia hoja yetu na nataka nichukue nafasi hii kuwashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini chimbuko la Muswada huu tuliouleta hapa Bungeni. Tarehe 31 Desemba, 2010, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, alitangaza uamuzi wa busara sana, uamuzi alioufanya wa kuamua kwamba nchi yetu sasa itafute Katiba mpya, alitoa sababu nyingi, lakini kubwa ni kwamba, Katiba tuliyokuwa nayo sasa imetutumikia vema kwa muda wa miaka 50, lakini mambo mengi yamebadilika, dunia imebadilika na Tanzania yenyewe imebadilika na Watanzania pia wamebadilika. Akaona sasa ipo haja tukae chini ili tuangalie namna gani tutapata Katiba nyingine ambayo itatuvusha katika kipindi cha miaka 50 ama hata zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, alipoutangaza uamuzi ule na sababu zake nzuri, uamuzi ulipokelewa vizuri sana, ulipokelewa na watu wote waliokuwa wanataka Katiba mpya, isipokuwa wale tu ambao walikuwa wanadai Katiba mpya kinafiki. Ndiyo, wakaupokea lakini wakasema aaah, mbona inakuja mapema sana. Sasa tukashangaa, watu hawa walikuwa wanaitaka, lakini sasa hawaitaki, tukasema kumbe hawa wenzetu wala walikuwa hawaitaki, walikuwa wanafiki tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tangazo lile, Serikali ikaanzisha mchakato wa kutunga Sheria

ambayo itaendesha shughuli yote ya kuuendesha mchakato huu mpaka tutakapofikia Katiba hiyo mpya. Mchakato huu ulipoanza, tukatunga Sheria, Sheria ile ilipitishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na ilipitishwa katika hali karibu sawa na hii ambayo tunaiona sasa, ya Waheshimiwa Wabunge wanaotaka Katiba mpya kususia utaratibu wa kuipata Katiba hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hiyo, ilipopitishwa Sheria hiyo, namba 8 ya mwaka 2011, tarehe 1 Desemba, Sheria hiyo, ilianza kutumika, lakini ndani ya siku 80 toka Sheria hiyo ianze kutumika, tulifanya mabadiliko. Mabadiliko ya kwanza ya Sheria hiyo, yalitokana na nini! Mabadiliko haya yalitokana na mazungumzo marefu sana aliyoyafanya Mheshimiwa Rais na watu mbalimbali, vikiwemo Vyama vya Siasa, Mashirika ya Dini, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Mashirika ya Kijamii na ya Kiraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais alikaa nao Ikulu, akazungumza nao, wakaonesha *reservations* zao kuhusu Sheria ile. Rais akakubali akasema, *fine*, sasa tutafanya mabadiliko kwenye Sheria hii katika awamu tatu. Awamu ya kwanza ishughulikie na upatikanaji wa Tume ambayo itaendesha mchakato huu. Awamu ya pili, ndiyo hii ambayo tupo karibu kuhitimisha ya kukamilisha jinsi gani Bunge la Katiba litapatikana na litafanyaje kazi na awamu ya tatu itashughulikia mchakato wa kura ya maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuko katika awamu ya pili na haya yalikuwa ni makubaliano ya Rais na

Vyama vya Siasa na Asasi mbalimbali ambazo alikutana nazo Ikulu. Rais alifanya kazi kubwa sana na hakuna aliyeweza kuieleza kazi hiyo vizuri, zaidi ya Mheshimiwa Tundu Lissu. Mheshimiwa Tundu Lissu tarehe 9 Februari, 2012, wakati tunajadili mabadiliko ya kwanza ya Sheria hii, alikuwa na maneno mengi sana mazuri ya kusema kuhusu Rais yetu. Alisema maneno yafuatayo:-

Nataka ninukuu kwenye *Hansard* hiyo ya tarehe 9, alisema: "Kwa maana hiyo, wakati anazungumzia umuhimu wa Rais alivyoitisha vikao hivi mpaka akakubaliana kufanya mijadala na watu mbalimbali, mpaka akakubaliana tufanye marekebisho ya Sheria. Mheshimiwa Tundu Lissu akasema maneno yafuatayo:-

"Kwa maana hiyo, Rais anapoacha shughuli zake nyingi nyingine za Kitaifa ili kuzungumza na watu ambao wala hawajibiki kisheria kukutana au kuzungumza nao kwa jambo lolote lile, Rais, anapotumia siku nne na saa karibu 20 kuzungumza nao juu ya jambo moja, Rais anapokubali kukaa hadi saa sita za usiku kujadili nao juu ya jambo hilo na Rais anapokubali kuacha shughuli nyingine nyingi ili kukutana na viongozi wa Vyama vyingine vya Siasa, Viongozi wa Kidini na wawakilishi wa Taasisi za Kiraia, kujadili nao juu ya jambo hilo hilo, yote haya yanadhihirisha umuhimu wa jambo hilo Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule alilikubali na kama alivyomnukuu Mheshimiwa Adam Malima jana, akamsifu sana, lakini leo ghafla, yote hayo

yameyeyuka, wakati Sheria ile nzito, Sheria mama tumeshaipitisha, tunachofanya sasa wala si cha ajabu, tunachofanya sasa ni kuweka utaratibu wa jinsi ya kutekeleza Sheria mama. Hatutungi kitu kipya, hawa watu 166 walipitishwa kwenye Sheria ile na hakuna hata aliyeipigia kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo inakuwa ni hoja, wakati si hoja kimsingi. Tuseme tu kwamba, baada ya kukubaliana hivyo, mabadiliko ya kwanza yakapita, sasa tuko kwenye mabadiliko ya pili, ambayo tunataka kuweka utaratibu ni jinsi gani tutaweza kupata watu 166 wa kuingia katika Bunge la Katiba, ni jinsi gani Bunge hili la Katiba litapata Mwenyekiti wake na ni jinsi gani Mwenyekiti huyu ataendesha na atakuwa na kazi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri haya ni mambo ambayo ni lazima tuyazungumze, tuyaweke sawa. Sasa tumeleta mapendekezo yetu, tunaamini ni mapendekezo ya msingi sana.

Waheshimiwa Wabunge tunawaomba kama yalivyo myajadili, myapitishe ili tuweze kumaliza awamu hii ya pili. Awamu ya tatu tunategemea labda mwezi wa 10, tutakuja na Sheria nyingine, itakayoweka utaratibu wa jinsi ya kuendesha kura ya maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa safari hii ushirikishwaji ulikuwaje, imezuka hoja hapa kubwa tu, ikafanya mpaka watu wakatoka. Wanasema wadau kutoka Zanzibar hawakushirikishwa. Nataka

nilithibitishie Bunge hili na wananchi kwa ujumla, mchakato huu umepitia hatua zote unazostahili kupitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi wa tano mwaka huu, Serikali ya Zanzibar ilipokea mapendekezo yetu haya, ikayajadili na wataalam, akiwemo Waziri wa Sheria, ambaye lazima nichukue nafasi hii kumshukuru sana na kumpongeza kwa kazi nzuri aliyoifanya katika suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamepitia, wakaamua, wakatuletea barua, wakatuletea maoni yao na sisi hatukufanya ajizi, maoni yale tumeya-*incorporate* yote, bila hata kubadili. Tena hata walipopendekeza kidogo sisi tukaongeza ili jambo hili liwe zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushirika wa Serikali ya Zanzibar, ambayo Serikali hiyo, rafiki zangu hawa wa *CUF* wamo, ndiyo Serikali yao. Serikali ya Zanzibar, ni Serikali yao ya CUF na Chama cha Mapinduzi. Unashangaa Serikali yao ambayo inawawakilisha Wazanzibari wote, inalikubali jambo hili, wao wachache wanalikataa wanatoka nje, wanamwakilisha nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao ni bora kuliko Rais wao aliyechaguliwa na Wazanzibari wote, Rais wao analikubali, wao wanasema sisi hatutaki, wao wanamwakilisha nani? Labda wangekaa wakajiuliza swali hilo. Naamini, ushiriki wa Serikali ya Zanzibar na watu wa Zanzibar ulikuwa ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, katika Kamati vile vile walikuja Wazanzibari na nikapata nafasi ya kukutana na rafiki yangu Shoka, ambaye zamani tulikuwa naye kwenye Bunge hili, akiwakilisha Chama kutoka Zanzibar, kinaitwa *ADC*. Alikuja akatoa maoni mazuri, sisi tulikuwepo siku ile ya kwanza na wengine wengi wa Jahazi Asilia na kadhalika, walikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapowaalika watu waje, huwezi kuwalazimisha waje na haisemwi kwamba ni lazima, kwanza hakuna Sheria inayosema kwamba lazima Kamati izunguke katika vituo vyote vitatu. Maana vituo vitatu vya Bunge ni Zanzibar, Dar es Salaam na Dodoma, lakini Kanuni haisemi kwamba lazima uzunguke kwenye vituo vyote, unaweza ukakaa Dodoma, ukaita watu, unaweza ukakaa Dar es Salaam, ukaita watu na unaweza ukakaa, Zanzibar ukaita watu na tunategemea watu wa Dar es Salaam, kama wana hamu na jambo hilo, watakwenda kulitolea maoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kikao cha Kamati kilikaa, walikaa karibu wiki mbili pale, walipokea maoni ya watu wengi, nawashukuru. Ninachojaribu kusema ni nini, kwamba, ushiriki wa Zanzibar kama Serikali na kama watu, ulikuwa upo na ni mkubwa sana, lakini zaidi ya yote, sisi Waheshimiwa Wabunge ni wawakilishi wa wananchi. Sisi ndiyo tunawakilisha wananchi wote, sasa Mbunge akiwa ameshiriki, anakujaje kusema tena kwamba wananchi hawajashiriki, wakati yeye ameshiriki na Wabunge hawa, wengi waliotoka humu

wamo kwenye Kamati ile ya Katiba na Sheria na wengi wameshiriki toka mwanzo mpaka mwisho, rekodi zinaonesha hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachojaribu kusema ni kwamba, ushiriki katika ujadili wa hoja hii ulikuwa ni mkubwa sana, ulikuwa ni ushiriki wa Serikali, ulikuwa ni ushiriki wa wananchi wa Tanganyika, kwa maana ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumzia ushirikishwaji huo, niseme tu kwamba, upo kweli umuhimu wa wadau wote kushiriki au wadau wengi kushiriki, lakini utaratibu huu kama ilivyokwishasemwa jana, ulianza mwaka 1995 tu, kabla ya hapo, ilikuwa ni Bunge peke yake ndilo linatunga Sheria bila ya kuwa na haja ya kupata maoni ya wadau wowote. Ni utaratibu tumejiwekea ili kuweza kushirikisha watu, ni jambo zuri, lakini halipunguzi wala halinyimi Bunge hili nafasi yake iliyokuwa nayo ya kutunga Sheria. Bunge hili ndilo lenye kazi ya kutunga Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo tuliyoleta mbele yenu hapa, mnaweza mkayabadilisha kichwa chini, miguu juu kama mnataka, maana nyinyi ndiyo wenye kazi hiyo. Pamoja na maoni yote yaliyotolewa na wadau, haiwafutii ninyi nafasi ya kutunga Sheria, kwa hiyo, kutokushiriki kwa sababu tu kwamba, wananchi hawakushirikishwa, ni sababu ambayo ni hafifu sana kwa kweli. Labda mtu anaweza akawa na sababu yake nyingine, akaitafuta hii, maana hii ndiyo

ya kupatikana kwa haraka haraka, lakini nayo haina msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya yale mabadiliko ya kwanza, Tume ya Katiba ikaanza kazi yake, Tume inayoendeshwa na Mheshimiwa Dkt. Joseph Sinde Warioba na nichukue nafasi hii kumpongeza yeye na wana Tume wake, kwa kazi nzuri sana sana waliyoifanya mpaka sasa. Wamezunguka nchi nzima, wamekusanya maoni ya wananchi kwa kadri walivyoweza, wakafanya kazi wakayachambua, wakaandika Rasimu ya Katiba, ambayo imetokana na maoni ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikabidhiwa Rasimu hiyo na sisi tukasema wananchi sasa wakae kwenye Mabaraza, wayazungumze yale yaliyomo ndani. Hiyo kazi imekamilika nafikiri mpaka jana watu wote waliokuwa Mikoani wamerejea Dar es Salaam, sasa wanaanza kazi ya kuchambua hayo maoni tena, tunategemea wataandika Rasimu nyingine pamoja na taarifa yao, watamkabidhi Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais naye kwa mujibu wa Sheria hii, anatakiwa alikabidhi Bunge la Katiba liijadili ndani ya mwezi mmoja, baada ya kufanya vitu kadhaa, ikiwemo kutangaza kwenye magazeti ya Serikali na kadhalika. Ninachojaribu kusema ni nini, watu wengi sana wamejitokeza, ukiacha yale Mabaraza ya Wilaya, Wilaya 143, kulikuwa na makundi mengine ya watu 675 yaliyojiandikisha na yametoa maoni yake kwa Tume hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Tume bado ina kazi kubwa sana ya kuyachambua maoni haya na kuandika hiyo Rasimu mpya, lakini tuna imani sana na Tume hii na tuna hakika wataifanya kazi yao vizuri na tutaletewa basi tuijadili maana yake sisi tutakuwa wajumbe wa Bunge la Katiba, tutapata nafasi ya kuijadili Rasimu hiyo kwa niaba ya wananchi wetu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haya niliyokuwa nayasema ni ya kijumla jumla, sasa nijaribu kujibu hoja ambazo zililetwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani katika taarifa yao, walihoji kuhusu uhalali wa marekebisho ya sehemu ya (c) na (e) ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho. Kilichohojiwa pale ni nini? Walisema yaliyomo katika sehemu ile ya (C) na (E) ni mambo mapya kabisa, hayakuwamo katika Muswada wetu tuliousoma kwa mara ya kwanza hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni kweli, haya ni mambo mapya, lakini yalitokana, wakati tunauchambua huu Muswada mambo mapya yaka-*crop up,* tukasema haya ni muhimu yaingizwe katika mabadiliko haya na tumepewa uwezo huo na Kanuni za Bunge hili, Kanuni ya 86(10) inampa mtoa hoja uwezo wa kubadili au kurekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sisi tulibadili, tumeleta hayo na ni mazuri, yalijadiliwa na Kamati na

ndani ya Kamati ile Wapinzani wapo wengi. Niseme katika hatua hii kwamba, Wapinzani walichangia vizuri sana katika mabadiliko haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu ameeleza hapa jana na ameeleza vizuri sana, jinsi mjadala ule ulivyokwenda na wenzetu walifanya nini ndani ya kikao hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hilo la kusema kwa nini haya yameletwa na ni mapya, hayana uhalali, la msingi ni kwamba uhalali upo na tunapata uhalali huo katika Ibara ya 86(10) ya Kanuni za Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lililetwa na ambalo pengine nilizungumzie ni la idadi hii ya makundi 166. Kama nilivyosema mwanzo, ilikubaliwa ndani ya Sheria mama, ambayo watu waliigomea, halafu baadaye wakarudi wakaisifu sana, Sheria hiyo hiyo na zilikuwa sifa nyingi, Mheshimiwa Malima jana alinukuu sifa hizo na sitaki kuzirudia, lakini zilisemwa kuhusu uzuri wa Sheria ile ambayo ilitaja kwamba watakuwapo wajumbe wengine 166.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haikuwa tatizo wakati ule na naamini siyo tatizo mpaka sasa. Kamati imekubali na wajumbe wote waliochangia katika hoja hii, wameikubali namba hii ya 166. Kwa hiyo, mimi wala sitaizungumza kama vile ni hoja, maana si hoja, ilikubaliwa toka awali na imekubaliwa na Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wake ni nini? Hoja tu kwamba lazima mfike mahali muwe na namba ambayo kwanza ni *manageable*, lakini pili, italeta watu wengi wenye hekima, naogopa kusema itawakilisha. Kwanza lile Bunge si la uwakilishi, lile ni Bunge la watu wenye hekima katika nchi yetu ambao wanakaa kututungia Katiba. Hakuna hoja zingine wanazotuwasilishia mle ndani, hawaendi kubishana hoja, wanakwenda kutunga katiba ya nchi yetu, unahitaji vichwa vilivyotulia, vichwa baridi, wazee wa hekima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukasema, pamoja na Wabunge na hawa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Tutafute watu wengine 166 watafanya *around figure* pale ya 600, wakae watu hawa watutungie Katiba. Sasa tukasema, watoke kwenye makundi mbalimbali, makundi makubwa makubwa tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulisema watatoka kwenye *NGOs*, Asasi zisizokuwa za Serikali, za Kidini, Vyama vya Siasa vilivyokuwa na usajili wa kudumu, Taasisi za Elimu ya Juu, huko tutapata watu wenye busara watakuja, makundi yenye mahitaji maalum, hawa ni muhimu, kwa sababu kuna mambo wanayajua, sisi wengine hatuyajui. Vyama vya Wafanyakazi, hasa zile jumuiya zao kuu, jumuiya za wakulima, wafugaji, wavuvi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ikatokea wakati tuko kwenye Kamati, mabishano yalikuwa makubwa, wakasema, tuorodheshe wote hawa. Nimewaambia

hapa sasa hivi, kuna makundi 675 yaliyojitokeza safari hii tu kuhusiana na Katiba, haya tunayafanyaje, tukisema tunaorodhesha wote hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Lukuvi wakati anachangia na nimpongeze sana, alifanya kazi nzuri sana. Alizungumza juu ya namba za hivi vikundi mbalimbali, ni namba kubwa mno, ukisema unaorodhesha, ndani ya Sheria hii, haitakuwa ya mabadiliko itakuwa ni Sheria ya aina yake. Hata ukisema unafanya kama ni *Schedule*, bado kitakuwa ni kitu cha aina yake, lakini si hivyo tu, kuna hatari ya kuyaacha mengine. Unaweza ukaandika yote ukadhani umekamilisha, kumbe umesahau mawili au matatu na yale unayafanyaje, watakuja kukuuliza mbona sisi umetuacha, utafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna hatari nyingine ya kuandika mengine ambayo si muhimu, wala hayapo, pengine yameshafutwa. Katika moja ya mifano yao waliyotoa pale wakaandika, wawakilishi wa wakulima, wakaandika *TFA*. Tukasema hapana, *TFA* siyo, hiyo ni kama kampuni tu, ina watu wana *shares* mle, wamekaa basi. Haiwakilishi wakulima kama tunavyosema inawakilisha wakulima wote, si kweli.

Kwa hiyo, nasema katika hili suala la kuorodhesha, kuna mambo mawili yanaweza kutokea, unaweza ukaorodhesha watu siyo, au ukasahau watu muhimu. Kwa hiyo, tukasema, Rais atazingatia makundi haya makubwa na amewahi kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, amefanya hivyo na amefanya kazi nzuri sana, jana tumeelezwa hapa na Mheshimiwa Lukuvi vile vile. Kazi ambayo ameifanya wakati anateua Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Kwa hiyo, Ibara hii nayo tumesema inabaki hivi ilivyo kwa sababu tunadhani inatosheleza. Rais si mtu mmoja, Rais ni Taasisi, kuna watu, kuna vichwa vizuri mle, kuna vichwa baridi sana mle, vitamshauri, havitafanya makosa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Watanzania wawe na imani na hilo na tumekwishafanya mwanzo na sasa tutaweza kufanya tena. Sasa hili ndilo lilikuwa kubwa, mabadiliko ya hii katika 22(1) (c).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna moja ambalo ni jipya tumelileta na hili lilitokana na kuona tu. Sheria inasema kwamba, Bunge hili litakapokuwa linapitisha Katiba hii, litaipitisha kwa misingi ya theluthi kutoka Tanzania Zanzibar na theluthi mbili ya Wajumbe kutoka Tanzania Bara. Wakishapiga kura hawa wakapatikana theluthi hizi mbili kutoka pande zote mbili, basi Katiba sasa itapita, itakwenda kwenye *referendum* kupigiwa kura na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukajiuliza, kwa mfano, theluthi mbili haipatikani kwa upande mmoja, au haipatikani kwa pande zote mbili, mnafanyaje? Ndiyo Katiba haiendi popote? Bunge hilo lina uwezo wa kusema hivyo? Tukasema hapana, tukasema ijadiliwe tena ndani ya hilo hilo Bunge ipigiwe tena kura, ikishindikana tena, hoja zinazofanya jambo hili likwame ziainishwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu hizo hoja zijadiliwe, zipigiwe tena kura kwa misingi ya theluthi mbili. Kwa hiyo, hoja hizo zipigiwe kura kwa misingi ya *simple majority* na iandikwe wanavyopeleka huko kwenye *Referendum,* isemwe kwamba hoja hizi zilipigiwa kura ya *Simple Majority*. Tulishindwa kupata ile *two third majority.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tutajitahidi sana kuhakikisha kwamba hii inapatikana, maana nia na toka tulivyoanza ni kutafuta *consensus,* kujenga *consensus* ya Kitaifa, kujenga makubaliano ya Kitaifa ili tukubaliane tufike mwisho. Tutahakikisha tunajitahidi kupata huo muafaka wa Kitaifa, makubaliano ya Kitaifa, ili wapitishe kwa hizo theluthi mbili zinazotakiwa, lakini tukasema wakishindwa basi utaratibu huu utumike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilituletea mgogoro siyo mgogoro, lakini majadiliano ya moto sana. Tulikuwa tunasema haya, Mheshimiwa Rais amepokea Rasimu ameitangaza kwenye Magazeti ya Serikali na Magazeti mengine, kisha ameamua sasa kuliitisha Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda wakati nazungumzia hili nitoe jibu Bunge lenyewe litaitishwa wapi. Kwa kawaida mwenye kuitisha Bunge, anasema nataka Bunge hili likutane mahali fulani. Kwa hiyo, siyo wajibu wetu sisi sasa hivi kusema Bunge hili likutane Dar es Saalam, likutane Dodoma au likutane

Arusha au Kigoma ama Nachingwea au sehemu nyingine yoyote ambayo tungependa sisi likutane. Lakini yule mwenye kuliitisha atatamka katika ile taarifa yake ya kuliitisha Bunge, kwamba naliiitisha Bunge la Katiba, nataka Bunge hilo likutane mahali fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema Rais si mtu mmoja peke yake, kuna watu watamshauri na nafikiri Waziri wa Katiba na Sheria naye atapata nafasi hiyo ya kumshauri. Basi wajumbe watakaa, watatulia, watafanya kazi katika siku zilizopangwa, kazi nzuri ya kutupatia Katiba itakayotuendesha vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukasema *okay,* Bunge limeitwa, tunafanya nini. Wote tumeshafika, kwa mfano, tumeitwa labda Dodoma hapa, wote tumekuja Dodoma, kiongozi wetu ni nani? Nini kinafanyika siku ile ya kwanza Bunge linafunguliwa, si lazima tuwe na Mwenyekiti, tukasema nani atakayeongoza Bunge hilo mpaka tutakapopata Mwenyekiti wa kudumu. Maana yake Mwenyekiti wa kudumu lazima achaguliwe. Kanuni zetu lazima zipitishwe kwanza, halafu ndipo Mwenyekiti wa kudumu apatikane, kutokana na Kanuni maana yake Mwenyekiti anapatikana kutokana na Kanuni. Sasa tunapitishaje Kanuni, tunaendeshaje uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukawa na *proposal* kadha wa kadha. Lakini tumeleta moja hapa kwamba, Makatibu wa Bunge na Katibu wa Baraza kwa vyeo vyao hivyo watakuwa ndio watakaotuongoza mpaka tupate Mwenyekiti wa

muda. Au watuongoze ili tupitishe Kanuni, ili tumchague Mwenyekiti wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tumeleta *proposal* hapa tunataka muiangalie, mnaweza mkatoa maoni yenu. Kuna watu wana maoni tumtaje mtu fulani, pengine Jaji Mkuu labda aje awe Mwenyekiti wa Muda mpaka tutakapomchagua Mwenyekiti wetu, au mmoja wa Maspika wa Bunge au Baraza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge letu hili tulipoanza, tulimchagua Mheshimiwa Mama Anna Abdallah, alikuwa *most Senior,* ndiye akatuendesha mpaka tukamchagua Mama Anna Makinda kuwa Spika wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi ilikuwa rahisi kusema Mama Ana tukakubaliana. Bunge hilo la watu 600 sijui kama itakuwa rahisi kama ilivyokuwa katika Bunge hili. Kwa hiyo, tumeleta mapendekezo ambayo tunadhani mkitushauri basi tutafumbua jambo hili na tutaweza kupata mtu ambaye atatuendeshea Bunge letu mpaka tukapata Kanuni na kupata Mwenyekiti na Makamu wake na viongozi wa Bunge hilo kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni mambo ambayo yamo katika mapendekezo yetu na kwa vile jana wamezungumza watu hapa na leo wote wamekuwa wakiunga mkono. Kwa kweli hakuna hata mmoja aliyekwenda kulalamika kuhusu vipengele, wote walisema ipite. Nafikiri basi hali hiyo itaendelea katika

hatua yetu itakayofuata ya vifungu na itaendelea hivyo hivyo na mwisho Muswada huu upitishwe na kuwa sheria ya nchi yetu. Ni sheria muhimu sana, kwa sababu inaweka utaratibu wa kupata Bunge la Katiba. Viongozi wa Bunge hilo, uendeshaji wa Bunge hilo, kwa hiyo ni kasheria kadogo kana Vifungu sita tu, lakini ni muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilikuwepo moja limeuliza wapi na hili nimejaribu kulijibu, Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Omary Baduwel, waliliulizia sana hili, walikuwa wanataka kujua wapi tutafanyia Bunge hili. Kwa hili nimesema mwenyewe atakayeitisha atatuambia wapi tufanyie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kueleza kimsingi nini kilitokea mpaka hapa tulipofika na kwa nini tumeuleta Muswada huu mbele yako na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka nichukue nafasi hii, kurudia kuwashukuru wote waliochangia katika hoja yangu na niwaombe sasa muipitishe hoja hii ili iwe Sheria, ili tuweze kuendelea na mchakato wetu wa kuipatia nchi yetu Katiba mpya, Katiba ambayo itatuongoza katika maendeleo ya kisiasa, maendeleo ya kiuchumi na maendeleo ya kijamii, Katiba ambayo itaendeleza hali yetu ya amani na utulivu, Katiba ambayo itawafanya Watanzania, wajiletee maendeleo yao wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumsifu Mheshimiwa Dkt. Augustine L. Mrema. Mheshimiwa Dkt. Mrema ni mwanasiasa wa siku nyingi, ni mwanasiasa ambaye ni Mzalendo. Nilimwambia jana Mheshimiwa Mrema, wewe utakuwa mwanasiasa mpaka siku ya mwisho kwa sababu una sifa moja kubwa tu. Unaipenda Tanzania na kwa sababu unaipenda nchi hii uko tayari kuifia, kwa mazuri yake, utasimama imara, kwa mabaya yake utajaribu kuyarekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mrema yuko humu ndani kuchangia, pale tulipokosea nina hakika atasema, lakini tutakapopatia atatuunga mkono. Hivyo ndivyo walivyotakiwa kufanya ndugu zangu hawa waliotoka. Wangekaa humu ndani wakatoa maoni yao kwa mintarafu ya nchi yetu. Tunataka kuijenga nchi hii kwa pamoja. Sasa mkiondoka, mkikimbia nje, sijui, lakini Mheshimiwa Mrema, nakuheshimu sana kwa kitendo chako hicho cha juzi na cha jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono, nimemwona hata Mheshimiwa Mbunge Asha Mohamed Omari kutoka Pemba naye amesimama kuunga mkono hoja hiyo.

Baada ya hoja hiyo kutolewa na kuungwa mkono, naomba sasa tuendelee na hatua inayofuata.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

## Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2013
## *(The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2013)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kazi kubwa sana ya majadiliano na ya muda mrefu, kazi nzito kwa masilahi ya nchi yetu, kwa masilahi ya Watanzania, sasa naomba tushirikiane vizuri bega kwa bega ili sasa tuweze kuhitimisha kazi hii ya Kikatiba ya utungaji wa sheria. Tumeingia Kamati ya Bunge Zima na tunazo *Amendments* mbalimbali.

Ibara ya 1

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 2

## SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. MATHIAS M. CHIKAWE, MINISTER FOR CONSTITUTIONAL AND LEGAL AFFAIRS AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE CONSTITUTIONAL REVIEW (AMENDMENT) ACT, 2013

Made under section S.O 83(10)(b)

---

A Bill entitled "The Constitutional Review (Amendment) Act, 2013 is amended generally as follows:-

**A:** In Clause 2 by deleting the phrase "on the basis of collected views and recommendation of the public" appearing in the proposed definition of the term "Draft Constitution".

**B:** In Clause 3 by –

(a) deleting paragraph (a) and substituting for it the following:

"(a) by deleting the opening phrase of paragraph (c) appearing in subsection (1) and substituting for it the following:

"(c) one hundred and sixty six members appointed by the President in consultation with the President of Zanzibar from the following:"

(b) inserting immediately after paragraph (a) the following:

"(b) deleting paragraph (vi) and substituting for it the following:

(vi) the Trade Union Organisations";

(c) renumbering paragraph (b) as paragraph (c).

**C:** By adding immediately after clause 3 the following

clauses:

"Addition of section 22A

**4.** The principal Act is amended by-

(a) adding immediately after section 22 the following new section:

"Interim Chairman

**22A**.-(1) Without prejudice to the provisions of section 23, after the convening of the Constituent Assembly, the Clerk of the National Assembly and the Clerk of the House of Representatives shall manage and supervise the process of electing the Interim Chairman of the Constituent Assembly who shall be responsible for-

(a) developing and adopting the Standing Orders of the Constituent Assembly; and

(b) conducting the election of the Chairman and Vice Chairman of the Constituent Assembly.

(2) The Interim Chairman elected by the Constituent Assembly under subsection (1) shall not be eligible to contest for the chairmanship of the

Constituent Assembly."

Amendment of section 23

**5.** The principal Act is amended in section 23 by-

(a) adding immediately after subsection (3) the following:

"(4) Qualifications and procedures for election of Chairman and Vice Chairman shall be as may be prescribed in the Standing Orders."

(b) renumbering subsections (4), (5) and (6) as subsection (5), (6) and (7) respectively;"

(b) renumbering clause 4 as clause 6."

**D:** In clause 6 as renumbered by-

(a) deleting the proposed sub-clause (4) and substituting for it the following:

"(4) The Clerk of the Constituent Assembly shall, upon consultation with the Deputy Clerk and public institutions, nominate such number of staff from the National Assembly, the House of Representatives and from public institutions, as may be necessary for better performance of the functions of the Constituent Assembly.

(5) The staff under subsection (4) shall be nominated through secondment for the prescribed period of the Constituent Assembly."

(b) renumbering subsection (5) as subsection (6).

**E:** By-

(a) adding immediately after clause 6 as renumbered the following:

"Amendment of section 26

**7.** The principal Act is amended in section 26 by adding immediately after subsection (2) the following:

"(3) Where the support of two third majority of the total number of members is not attained as required under subsection (2), the Chairman of the Constituent Assembly shall identify issue or issues in controversy for the purpose of voting for the second time in respect of such issue or issues.

(4) The issue or issues as identified under subsection (3) shall be passed by the Constituent Assembly based on the support of two third majority of the total number of members hailing from Mainland Tanzania and two third majority of the total number of members hailing from Tanzania Zanzibar.

(5) Where the support of two third majority is not attained as required under subsection (4), the Constituent Assembly shall vote for the third time, and the issue or issues shall be

determined by simple majority of the total number of members hailing from Mainland Tanzania and simple majority of the total number of members hailing from Tanzania Zanzibar.

(6) Upon completion of voting under subsection (5), the proposed Constitution shall be presumed to have been passed by the Constituent Assembly and the provisions of the Referendum Act shall apply.

(7) Procedures for voting under this section shall be as prescribed in the Standing Orders."

(b) renumbering clauses 5 and 6 as clauses 8 and 9 respectively.

**F:** In clause 9 as renumbered by deleting the proposed sub-clause (4) and substituting for it the following:

"(4) The Chairman of the Constituent Assembly, after consultation with the Vice Chairman may, upon approval by the President in agreement with the President of Zanzibar, extend the period under subsection (3) for such period as may be appropriate to accomplish the functions of the Constituent Assembly."

Dodoma, **MATHIAS .M. CHIKAWE**
……………………, 2013 *Minister for*
*Constitutional and Legal Affairs*

## FURTHER SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY THE HON. MATHIAS M. CHIKAWE, MINISTER FOR CONSTITUTIONAL AND LEGAL AFFAIRS AT THE SECOND READING OF THE BILL ENTITLED "THE CONSTITUTIONAL REVIEW (AMENDMENT) ACT, 2013"

*(Made under S.O. 86 (10)(b))*

A Bill entitled "The Constitutional Review (Amendment) Act, 2013" is further amended as follows:-

**A:** In clause 3 by deleting the word "consultation" appearing in the proposed paragraph (c) and substituting for it the word "agreement".

**B:** In clause 5 by deleting the proposed amendment of section 23 and substituting for it the following:

"Amendment of section 23

**5.** The principal Act is amended in section 23 by-

(c) adding immediately after subsection (3) the following:

(4) A member shall not be eligible for nomination or election as a Chairman or Vice Chairman unless that member-

(a) possesses a degree in law, economics or political science from a recognized university;

(b) possesses experience and

competence in chairing public assemblies or *fora*;

(c) has not been convicted by any court in the United Republic and sentenced to a term of imprisonment exceeding six months for any offence involving dishonesty and moral turpitude.

(5) Procedure for application, nomination and election of Chairman and Vice Chairman shall be as may be prescribed in the Standing Orders.

(d) renumbering subsections (4), (5) and (6) as subsections (6), (7) and (8) respectively;"

**C:** In clause 6 by deleting the proposed amendment of subsection (4) and substituting for it the following:

"(4) The Clerk of the Constituent Assembly shall, upon consultation with the Deputy Clerk, nominate such number of staff from the National Assembly, the House of Representatives, Offices of the Attorneys General of the United Republic and Zanzibar and from other public institutions, as may be necessary for better performance of the functions of the Constituent Assembly."

Dodoma, **MMC**
………………..…., 2013 *MCLA*

**JEDWALI LA MAREKEBISHO LITAKALOWASILISHWA NA MHE. MATHIAS M. CHIKAWE, WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA WAKATI WA KUSOMWA KWA MARA YA PILI MUSWADA UNAOITWA "MUSWADA WA MAREKEBISHO WA SHERIA YA MABADILIKO YA KATIBA, 2013**

---

Limtengenezwa chini ya Kanuni ya 83(10)(b)

---

Muswada uitwao "Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, 2013 (The Constitutional Review (Amendment) Act, 2013) unafanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:-

**A:** Katika Ibara ya 2 katika tafsiri ya neno "Rasimu ya Katiba" kwa kufuta maneno "kutokana na maoni na mapendekezo ya wananchi".

**B:** Katika Ibara ya 2 kwa-

(d) kufuta aya ya (a) na badala yake kuweka aya ifuatayo:

"(a) kwa kufuta maneno ya utangulizi kwenye aya (c) yanayojitokeza katika kifungu kidogo cha (1) na badala yake kuweka aya ifuatayo:

"(c) wajumbe mia moja stitini na sita watakaoteuliwa na Rais kwa kushirikiana na Rais wa Zanzibar kutokana na wafuatao;"

(e) kuingiza aya ifuatayo baada ya aya (a)-

"(b) kufuta aya (vi) na badala yake kuweka aya ifuatayo:

"Shirikisho la Wafanyakazi";

(f) kubadilisha aya (b) kuwa aya (c).

**C:** Kwa kuongeza baada ya Ibara ya 3 Ibara zifuatavyo:

"Kuongeza kifungu cha 22A

**4.** Sheria Mama inarekebishwa kwa-

(a) kuongeza baada ya Kifungu cha 22 Kifungu kipya kama ifuatavyo:

"Mwenyekiti wa muda

**22A**.-(1) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 23, baada ya kuitishwa kwa Bunge Maalum, Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katibu wa Baraza la Mapinduzi watasimamia mchakato wa kumchagua Mwenyekiti wa muda wa Bunge Maalum kwa madhumuni ya-

(a) kusimamia uandaaji na kupitishwa kwa Kanuni za Bunge Maalum; na

(b) kuendesha uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge Maalum.

(2) Mwenyekiti wa muda aliyechaguliwa na Bunge Maalum chini ya kifungu kidogo cha (1) hatakuwa na sifa ya kugombea nafasi ya uenyekiti wa Bunge Maalum.

Marekebisho ya kifungu cha 23

**5.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 23 kwa-

(a) kuongeza baada ya kifungu kidogo cha (3) kifungu kifuatacho:

"(4) Sifa za wagombea na utaratibu wa uchaguzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti utakuwa kama ulivyoainishwa kwenye Kanuni."

(b) kubadilisha kifungu kidogo cha (4), (5) na (6) kuwa kifungu kidogo cha (5), (6) na (7) ipasavyo.

(b) kubadilisha ibara ya 4 kuwa ibara ya 6 ipasavyo."

**D:** Katika Ibara ya 6 kama ilivyobadilishwa kwa-

(a) kufuta mapendekezo ya ibara ndogo ya (4) na badala yake kuweka ibara zifuatazo:

"(4) Katibu wa Bunge Maalum baada ya kushauriana na Naibu Katibu na taasisi za umma, atateua idadi ya watumishi kutoka miongoni mwa watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Baraza la Wawakilishi na taasisi za umma kwa kadri itakavyohitajika kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge Maalum.

(5) Watumishi walioteuliwa chini ya ibara ndogo ya (4), watateuliwa kwa masharti ya kuazimwa katika kipindi chote cha Bunge Maalum."

(b) kubadilisha kifungu kidogo cha (5) kuwa kifungu kidogo cha (6).

**E:** Kwa-

(a) kuongeza ibara mpya baada ya ibara ya 6 iliyobadilishwa kama ifuatavyo:

"Marekebisho ya kifungu cha 26

**7.**-(1) Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 26 kwa kuongeza baada ya kifungu kidogo cha (2) vifungu vifuatavyo:

(3) Pale ambapo theluthi mbili ya idadi ya jumla ya Wajumbe haijafikiwa kama inavyotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (2), Mwenyekiti wa Bunge Maalum atabainisha suala au masuala yaliyobishaniwa kwa madhumuni ya kupigiwa kura kwa mara pili.

(4) Suala au masuala yaliyobainishwa chini ya kifungu kidogo cha (3) yatapitishwa na Bunge Maalum kwa kuzingatia kuungwa mkono kwa theluthi mbili ya wajumbe wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya wajumbe wote kutoka Tanzania Zanzibar.

(5) Pale ambapo kuungwa mkono kwa theluthi mbili hakujafikiwa kama inavyotakiwa chini ya kifungu kidogo cha (4), Bunge Maalum litapiga kura kwa mara ya tatu, na suala au masuala yataamuliwa kwa wingi wa kura za jumla za wajumbe kutoka Tanzania Bara na wingi wa kura za jumla za wajumbe kutoka Tanzania Zanzibar.

(6) Baada ya kupiga kura chini ya kifungu kidogo cha (5), Katiba inayopendekezwa itachukuliwa kuwa imepitishwa na Bunge Maalum na masharti ya Sheria ya Kura ya Maoni

yatatumika.

(7) Utaratibu wa kupiga kura chini ya kifungu hiki utakuwa kama utakavyoelezwa katika Kanuni za Bunge Maalum.

(b) kubadilisha ibara ya 5 na 6 kuwa ibara ya 8 na 9 ipasavyo.

**F:** Katika ibara ya 9 kama ilivyobadilishwa kwa kufuta ibara ndogo ya (4) inayopendekezwa na kuweka badala yake-

"(4) Mwenyekiti wa Bunge Maalum, baada ya kushauriana na Makamu Mwenyekiti, anaweza, kwa ridhaa ya Rais baada ya kushauriana na Rais wa Zanzibar, kuongeza muda uliotolewa chini ya kifungu kidogo cha (3) kwa kipindi kitakachofaa kukamilisha shughuli za Bunge Maalum."

Dodoma, **MATHIAS .M. CHIKAWE**
……………………, 2013 *Waziri wa Katiba na Sheria*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 3

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. SELEMANI SAID JAFO MEMBER OF PARLIAMENT FOR KISARAWE CONSTITUENCY AT THE SECOND READING FOR THE BILL TITLED "THE CONSTITUTIONAL REVIEW" (AMENDMENT) ACT, 2013**

*[Made under Standing Orders 86 (11) and 88 (2)]*

A Bill titled "the Constitutional Review (Amendment) Act, 2013 is amended as follows;-

A: In clause 3(b) by:

(a) Deleting the word *"three"* appearing in the fourth line and substituting for it with the word "nine".

(b) Inserting immediately after the word "appointment" appearing in the fourth line the following: "of three persons from the list"

B. The principal Act is amended in section 20,

(a) Deleting subsection (4) thereof and Substituting for the following:

"(4) upon presentation of the Draft Constitution to the Constituent Assembly by the Chairman of the Commission under subsection (3), the President shall, have powers by Order published in the Gazette, to dissolve the Commission or to resume the same when he found necessary to do so.."

(b) by adding a new subsection (5) as follows:

"(5) Dissolution of the Commission by Order of the President shall entail abatement of the powers of the Commission and the Secretariat ", and if he resumes the Commission shall had the same powers and function as it were before.

A: By adding immediately after clause 3 the following clause:

4. The Principal Act is amended by adding immediately after section 23 the following new section:

23B There shall be a Nomination Committee for candidates for the positions of the Chairman and Deputy Chairman of the Constituent Assembly.

(2) The Nomination Committee shall be comprised of:

(a) the Ministers responsible for legal affairs of the United Republic and Zanzibar,

(b) the speakers of the National Assembly and the House of Representatives;

(c) the Attorney Generals of the United Republic and Zanzibar;

(d) leader of the opposition of the National Assembly; and

(e) Leader of opposition of the House of Representative if any.

(3) The Nomination Committee shall elect one of its members to be the chairman.

A: The Principal Act is amended in section 37, by:

(a) deleting the entire section; and

(b) renumbering section 38 of the Principal Act as section 37.

**SELEMANI SAID JAFO (MP)**
**KISARAWE CONSTITUENCY**

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Katika Kifungu hicho nimeleta *Schedule of Amendment,* kwa mujibu wa Muswada wetu inaonesha kwamba *list* ya majina ambayo yatakayopendekezwa yatakuwa ni matatu. Kwa mtazamo wangu ni kwamba, mfano hizo taasisi zikiwa 20. Zikipendekeza majina matatu, maana yake tutapata majina 66. Kwa hiyo, maana yake bado itakuwa haijakidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hizo taasisi zikiwa pengine 50, maana yake tutapata majina 150, maana

yake hapo Rais utamfunga ni lazima achukue katika wale watu watatu. Nini maana yangu, ndiyo maana nimependekeza badala ya tatu iwe tisa kwamba Rais anakuwa na uwanja mpana wa kufanya maamuzi. Kwa kufanya hivyo, tutaweza kufika katika kiwango sahihi cha wale Wabunge wataoongezwa katika Bunge letu la Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo yaliyomo katika hoja yangu ambayo nimeileta hapa kwa ajili ya *Amendment.* Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Hili ni la Sera.

**MWENYEKITI:** Aaa, ni la sera, haya mzee wa sera, Waziri mwenye dhamana na Wizara, Mheshimiwa Chikawe!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la Mheshimiwa Jafo, nasikitika nashindwa kuliafiki. Tuliweka watu watatu, huo ndio utaratibu, kutoka kila mahali unapewa watu watatu ili uchague. Sasa watu tisa ni wengi mno ili uchague mmoja. Nadhani watatu ni namba ambayo ni *manageable* na haina mgogoro. Kinachotakiwa hapa siyo kutoka katika kila kikundi, hapana, ni zile *apex* tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema vipo vikundi 675 tu, safari hii waliozungumzia Katiba, acha wale

ambao wameandikishwa kama alivyosema Mheshimiwa Lukuvi jana. Sasa ukisema waje tisa tisa, hata hizo *apex* zao*,* zikiambiwa zilete tisa tisa, hiyo kazi kwa Rais itakuwa ni ngumu na hata muda uliopo ni mfupi sana. Bunge hili linaanza mwezi Novemba, nafikiri tubakiwe na tatu. *(Makofi)*

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Labda kwa upande wa Serikali kifungu Kidogo cha 2(a), ukisoma kilivyoandikwa kinatoa taswira au maana kwamba orodha hiyo, yenye majina yasiyozidi matatu, *for appointment as Members,* inaleta dhana kwamba Rais ni kama amefungwa, lazima achukue hayo majina kama Wajumbe. Lakini nadhani nia yao ilikuwa ni kwamba jina moja kati ya hao watatu. Mheshimiwa Jafo amekuja na kitu ambacho nadhani ni vema tukaielewa hoja yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua Sheria hii ambayo inapendekezwa ifanyiwe marekebisho. Kifungu cha 22(i)(c), ukaangalia yale makundi yametajwa yako tisa. Hata kama kila kundi kwa mantiki ya mmoja mmoja; Rais, anapelekewa anateua jina moja, ndiyo hoja yake, hupati wale Wajumbe 169, hata ukisema katika *Apex,* ziko nyingi. Hoja yake ni kwamba kwanza mpeni Mheshimiwa Rais, upeo mpana majina tisa, lakini katika majina hayo tisa ateue watu watatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo dhana nzima ya kusema ushirikishi wa wananchi katika masuala haya hasa kuelekea kwenye suala hili la Bunge Maalum.

Ndivyo ninavyomwelewa Mheshimiwa Jafo dhana yake kwamba, tumpe upana huo, lakini sasa katika kufanya hivyo, ametumia pia hesabu, unaona kabisa kwamba anadhani katika kila kundi hilo hata wakiwa wengi wengi kwa *umbrella* hiyo, kuwapata wajumbe 166 amefanya tu *roughly* kwamba kila kundi hata kama lingeleta wajumbe watatu mara hamsini au mara hamsini na tano, unapata Wajumbe 165, bado nafasi moja tu kufikia pale, ambapo Rais anaweza akaijaza kwa njia nyingine anayoiona inafaa, au akaiingiza katika kundi lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani Mheshimiwa Jafo ametusaidia na mimi lilikuwa linanisumbua sana eneo hili. Lakini kwa maelezo haya kama Serikali itaona busara hiyo ambayo amekuja nayo, nadhani tutakuwa tunakwenda mbele vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona ufafanuzi uliotolewa na Mheshimiwa Andrew Chenge ndiyo ambao nilikuwa nataka kuuzungumzia, tulikuwa tunahitaji ufafanuzi zaidi ili kufikia hayo maamuzi ambayo yamesemwa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kuna tatizo kutokana na mapendekezo haya ambayo

yamewasilishwa na Mbunge na kuungwa mkono na Wabunge kadhaa.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nijibu hoja ya Mheshimiwa Chenge, naiona hofu yake, lakini kimsingi kwanza kama Serikali tunaomba turekebishe badala ya kusema majina matatu. Kwanza tuseme majina matatu ambapo katika majina hayo, moja linaweza likafikiriwa kwa uteuzi. Unaposema linaweza kufikiriwa kwa uteuzi siyo *guarantee* kwamba ni lazima atateuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini siyo hivyo tu, Mheshimiwa Chenge nakubaliana naye, lakini kwa upande mwingine naomba kidogo nitofautiane naye, kwa sababu haya makundi hatuna uhakika kwamba yatakuwa 55, yanaweza yakajitokeza makundi hayo ya *apex.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mwisho wa siku ziko taasisi nyingi, kama ambazo zimeainishwa katika Kifungu cha 22(i)(c) ambazo haziko katika muungano wa *apex;* yako Makanisa mbalimbali na Taasisi za kidini na Misikiti mingine, yako mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali ambayo hayaingiia kwenye *apex.* Mwisho wa siku Rais atakapowaalika, *so long as* ataalika makundi haya, kama yalivyoainishwa katika Kifungu cha 22(1)(c), yanaweza kuleta majina yao matatu matatu. Katika hayo matatu matatu huenda mojawapo likafikiriwa katika uteuzi, lakini si lazima kila kundi likafikiriwa. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Sielewi ukakasi unatoka wapi, kwa sababu hapa inasema *not more than nine.* Maana yake ni kwamba, hatujui hali itakuwaje. Inawezekana hizo taasisi zitakazo-*submit* majina yao, zikawa siyo zaidi ya 60 kwa mfano au siyo zaidi ya arobaini. Unaposema kwamba *not more than three,* ina maana utamfunga Rais, atafute uwanja mwingine mpana wa kuweza kupata watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nimesema kwamba, kwa nini tusiweke *nine.* Ina maana kwamba watu wanaweza wakawasilisha majina matatu, manne, matano, sita kwa kadiri wenyewe katika taasisi yao wanavyoona inafaa. Lengo langu ni kutoa uhuru mpana, ili mradi mwisho wa siku kila taasisi iweze kupeleka majina ya kutosha na *selection* iweze kufanyika, *at least* Rais, asije akajikuta kwamba amechagua majina tisini na hana sehemu nyingine ya kuchagua kutoka kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo hoja yangu tu na naomba kama ikiwezekana Mawaziri na Serikali iweze kunikubalia na kuelewa nini maana yangu katika eneo hilo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwa mara ya mwisho Mheshimiwa Naibu Waziri, halafu nitalihoji Bunge.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge na

Waheshimiwa Wabunge wamelisemea sana, naomba Serikali tuafiki, basi tupokee majina tisa, lakini kwenye kufikiriwa kwenye uteuzi basi, mmoja ndiye afikiriwe kwenye uteuzi na si lazima apate. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 4

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika kifungu hicho nimesema, "*The Principal Act is amended in section 20 by deleting subsection (4), thereof and substituting for the following: upon presentation of the draft Constitution to the Constituent Assembly by the Chairman of the Commission under subsection (3), the President shall, have powers by order published in the Gazette, to dissolve the Commission", or to resume the same when he found necessary to do so."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa lengo langu kubwa, nadhani Watanzania walishuhudia mchakato huu wa Katiba. Tulipoanza na mchakato huu wa Katiba ulikuwa na maneno makali kweli kweli! Wengine maneno makali mpaka kuinyooshea kidole Tume, mpaka kusema kwamba CCM imewatengenezea watu ulaji tu! Kuna maneno mengine makali sana na Watanzania wengi sana wanasema kwamba hii Tume inaendelea kukaa na baadaye sijui itafanya nini. Kweli

mimi nashukuru kwamba bahati nzuri Bunge hili liliafiki katika mchakato ule kwamba hii Tume iweze ku-*exist* na bahati nzuri imefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kuangalia sasa mapendekezo ambayo yapo katika Muswada huu, inaonekana kwamba tunapoondoka mwishoni, suala zima la Bunge la Katiba na kazi za Tume ukija kuangalia, kazi za Tume zenyewe zinaainisha kwamba ni kuchukua maoni mpaka itakapo-*submit*.

Mimi nilipendekeza hasa, ikiwezekana baada ya kuwasilisha ile rasimu katika Bunge la Katiba, maana yake ni nini? Ni kwamba Mheshimiwa Rais sasa awe na *flexibility* ya kufanya maamuzi ya kuangalia uhai wa Tume.

Kwa hiyo, aamue atakavyoona inafaa kwa busara. Sheria isifungwe mpaka kwenda kwenye *referendum* kwa sababu najua kwamba baada ya kazi inawezekana kuna kazi nyingine zitapungua. Hili ni kutokana na kilio cha Watanzania wengi waliokuwa wanapiga kelele mpaka wengine kuwavunjia heshima wazee wetu ambao kwa kweli wapo tu, kwa kweli hata mimi nilikuwa najisikia vibaya sana.

Sasa kwa kulinda heshima yake, basi Mheshimiwa Rais awe na mamlaka na *flexibility* ya kusema kwamba ni muda gani sasa anaweza akai-*dissolve* ile Tume kwamba sasa hivi nadhani kazi ya Tume imetosha baada ya kuwasilisha kazi yake. Vilevile awe na fursa ya kuona kwamba kama kuna jambo linafaa, basi Rais

asifungwe kui-*resume* tena ile Tume, ikaweza kufanya kazi kwa maslahi ya wananchi kwa sababu tunachoangalia ni maslahi ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili Mheshimiwa Jafo wala asipoteze nguvu nyingi sana kulisemea, kwa sababu na mimi naliona na ninalikubali kwa sababu naona inawezekana ilikuwa tu ni *oversight* kwa upande wetu tulipokuwa tunatunga hii sheria. Haiwezekani Tume ikaendelea bila kuvunjwa. Inafika mahali ni lazima imalize kazi yake ili mambo mengine yaendelee.

Kwa hiyo, hii naikubali isipokuwa tu pengine lugha hii, mambo ya '*resume'* na nini, na tutaomba wataalam wetu wa Sheria wai-*reflect* vizuri ili maneno kama *resume* halafu *typos* na mengine yapo kwenye *subsection five, "if he resume the Commission shall have the same power,"* ni Kiingereza tu. Nafikiri watu wetu watai-*brush up.* Lakini nakubaliana na hiyo *concept* kwamba Tume lazima iwe *dissolved at a certain time.*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ilivyo sasa kwenye kifungu cha 37 kinasema hii Tume itakwisha lini. Kifungu cha 37

kinasema: "*upon declaration of the results by the National Electoral Commission, the President shall by order publish in the Gazette dissolve the Commission.*" Kwa hiyo, Sheria inatamka Tume itakoma lini. Nadhani anachosema Mheshimiwa Jafo kinatokana na mabadiliko tuliyofanya au yaliyopo kwenye mapendekezo ya marekebisho ya sheria kwenye Bunge la Katiba. Tumefanya mabadiliko kusema kwamba uamuzi wa Bunge la Katiba, kwa vyovyote vile hautarudi kwenye Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Sasa ukishafanya hivyo, ina maana, na ndicho anachozungumza Mheshimiwa Jafo; inabidi sasa uende kwenye Sheria kwenye kifungu cha 20(4) anachopendekeza, kile kinachosema: "Kwa madhumuni ya kifungu kidogo cha tatu, Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume wanaweza kutoa ufafanuzi utakaohitajika wakati wa majadiliano katika Bunge Maalum."

Sasa ninachoona Mheshimiwa Jafo anasisitiza ni kwamba hatuna haja ya kuwa na Tume wakati huo ambapo Bunge la Katiba linaendelea. Kwa hiyo, napendekeza kubadilisha kidogo mapendekezo ya Mheshimiwa Jafo ili kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 20 cha Sheria mama, kwanza kwa kufuta kile kifungu cha (4) kinachosema: "Kwa madhumuni ya kifungu kidogo (3)  Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume wanaweza kutoa ufafanuzi utakaohitajika wakati wa majadiliano katika Bunge Maalum."

Kifungu cha (3) kinasema: "Mheshimiwa Rais baada ya kushauriana na kukubaliana na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar, atamwagiza Mwenyekiti wa Tume kuiwasilisha Rasimu ya Katiba kwenye Bunge Maalum." Pendekezo la Mheshimiwa Jafo ni kwamba huo ndiyo uwe mwisho wa Tume.

Kwa hiyo, tunapendekeza kwanza mambo mawili. Kwanza, kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 20, lakini pili, kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 37 cha Muswada. Ninapendekeza hivi, *dissolution,* yaani ukomo wa Tume utawekwa kwenye kifungu cha 37 kinachosema: "Baada ya matokeo ya kura ya maoni kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Rais kwa kupitia amri itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali, ataivunja Tume."

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuvunjwa kwa Tume kwa amri ya Rais kutakuwa na maana ya ukomo wa mamlaka ya Tume na Sekretarieti. Kwa hiyo, napendekeza marekebisho mawili hapo. Kifungu kidogo cha (4) kifutwe kwenye *section 20* na tuweke kifungu kipya cha (4) kitakachosomeka kama ifuatavyo:-

*"Notwithstanding the dissolution of the Commission under section 37(1), the Clerk of the Constituent Assembly may upon consultation with the Chairman of the Constituent Assembly invite the Chairman, Vice Chairman or any other member of the dissolved Commission to give clarification which may be*

*required during the debate by the Constituent Assembly." (Makofi)*

Maana yake ni kwamba, ule utaratibu wa kupata ufafanuzi kutoka kwa Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti au Mjumbe yeyote wa Tume wakati Bunge hili linaendelea, bado utakuwepo kama kutakuwa na sababu. Sasa ukishafanya hivyo, pendekezo ambalo hatujafika, lakini nilikuwa nafikiri liende kwenye kifungu cha 37 ni kukifuta kifungu kidogo cha kwanza kama nilivyokisoma, kinachosema: "Baada ya matokeo ya kura ya maoni kutangazwa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Rais kwa kupitia amri itakayochapishwa kwenye Gazeti la Serikali ataivunja Tume." Nashawishi kwamba kifungu hicho kifutwe na kiandikwe upya kama ifuatavyo:-

*"Upon submission of the draft Constitution to the Constituent Assembly under section 20(3), the President shall by order published in the Gazette dissolve the Commission." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuweka vizuri sana vifungu hivyo viwili ili kuondoa ule ukakasi na kuleta ladha ya maneno na Muswada wenyewe, sasa nitawahoji.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya*

*Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafo tulishapita kwenye hatua ya kukurudishia wewe. Tulishamaliza! Sasa ikishajibiwa, tunaingia kwenye kuhoji tu, haturudi tena kwako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na kifungu kinachofuata.

Ibara ya 5

**NDG. ANSELM MREMA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kifungu kipya cha (5) kilichowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pindi Chana, unachangia lakini huna *amendment* hapa. Si ndiyo eh! Washa *microphone,* tafadhali.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Kifungu kipya cha tano kilichowasilishwa na Mheshimiwa Waziri kinahusu sifa za kumchagua Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Bunge la Katiba. Kifungu hicho kinasema: "*A member shall not be eligible for nomination or election of a Chairman or Vice Chairman unless that member possess a degree of Law, Economics or Political Science from recognised University*."

Kwanza naungana nayo, lakini naomba kushauri kwamba hapa kuna *degree* nyingine hatujazitaja. Kwa

mfano, wale wenye *degree, let us say* masuala ya *Engineering* au *Language* na mimi nadhani kwa namna moja au nyingine wanaweza wakakidhi kukalia Kiti ili mradi ana *degree*.

Naomba kushauri kwamba iishie: "*possess a degree from a recognised University",* kuliko tukizitaja. Maana ukizitaja na mwingine ana *degree,* lakini tu kwa kuwa inahusu masuala ya *Engineering,* haikutajwa kwenye Sheria, basi hatakuwa na haki ya kukalia Kiti cha Bunge la Katiba. Nadhani suala la msingi iwe ni elimu na elimu yenyewe iwe ni *degree from a recognised University* kuliko ukizitaja na nyingine ni *degree super,* lakini hujaitaja tu hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile!

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Mimi ilikuwa katika suala la mpangilio kidogo, jinsi mnavyokwenda na vile vifungu mnavyovisoma, mnakwenda tofauti kidogo na hii Sheria ya Marekebisho ilivyo.

Sasa nataka nipate huu mtiririko unavyokwenda, kwa sababu hizi *amendments* za Mheshimiwa Waziri ambazo amezileta na nyingine ambazo sisi tumezileta, jinsi zinavyokwenda ni tofauti kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipate maelekezo yako.

**MWENYEKITI:** Hilo nitalijibu tu mimi, siyo la Waziri. Umeona tuna kifungu ambacho kinakwenda kufanya *renumbering* ya hizo *clauses.* Lakini tumepokea marekebisho yako Mheshimiwa Ndugulile, yanahama kwenye kifungu unachofikiri na yatakuja sasa kwenye kifungu kingine ambacho ni kifungu cha sita.

Kwa hiyo, tunazo *amendments* zako hapa na tutakuita tu. Tumeshajipanga nazo vizuri. Kwa hiyo, unataka kuniwahisha kwenye shughuli ya mbele kabla hatujafika, sasa naomba uwe mpole, taratibu tu na twende pole pole.

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili atusaidie katika hilo, halafu tuone tunakwendaje.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakiri kwamba hili si la Sheria, lakini tumeliweka hili kwa sababu ya kupunguza watu watakaoomba. Nakubaliana na ushawishi wa Mwenyekiti wa Kamati, pengine tuiongezee hiyo *degree* iwe *relevant* na nini sasa, kwa sababu najua kuna watu wanasoma kwenye mtandao, nao wana *degree* na kuna watu wana *honorary degree*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kikubwa hapa ni uwezo wa ku-*manage* Mkutano. Hicho ndicho cha msingi. Sasa tulifikiri kwamba tuki-*limit* hivi itakuwa ni

sawa sawa. Lakini kama inaleta ukakasi, sisi hatuna tatizo kuongeza hayo mengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pindi Chana, halafu Mheshimiwa Eng. Manyanya! Mheshimiwa Ndugulile ulishajitoa kwenye hii hoja.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana sana na mawazo ya *Attorney General* kwamba tukishasema, *from* a *recognised University, Tanzania Commission of Universities* zina utaratibu wa ku-*recognise* hizi *degree.*

Kwa hiyo, kama tuna wasiwasi na *degree on line* au zile ambazo ndivyo sivyo, watakaotusaidia ni *Tanzania Commission of University,* kuna *authentic degrees*.

Kwa hiyo, nadhani tukisema "*posses a degree from a recognise University"* inakidhi kwa sababu tunao utaratibu wa kusema *this is a recognised and this is not a recognised* kupitia *TCU*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG* nitakupa nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, muda wa kuendelea na shughuli haupo pamoja nami, sasa nitaomba Bunge lirejee ili tuweze kumpa nafasi Waziri wa Nchi, atoe hoja ya kuongeza muda mpaka tutakapomaliza shughuli hii.

*(Bunge lilirudia)*

## HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu likubali kutengua kanuni ya 28 ili kuwezesha Bunge hili kukamilisha kazi iliyobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kuongeza muda wa Bunge iliafikiwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Hakuna asiyeafiki, wote wameafiki. Kwa hiyo, tunarudi kwenye Kamati ya Bunge Zima.

## KAMATI YA BUNGE ZIMA

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Eng. Stella Manyanya!

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kuunga mkono hoja hii ya kutokuangalia tu wataalamu wa Sheria na hizo fani chache zilizotajwa, kwa sababu uzoefu

umeonyesha kwamba, sio kila Mwanasheria ndiye mwenye busara au hekima.

Tunao watu wenye hekima kutoka fani mbalimbali ambao wanaweza kutusaidia katika kutuongoza kwenye kikao hicho. Kwa hali hiyo, kusisitiza tu kwamba iwe ni Sheria au *Economics,* mimi nadhani tutakuwa tunajinyima nafasi ya kuwapata watu wenye hekima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu nyingine ni kwamba tunapotunga sheria zetu au taratibu hizi, mara nyingi zinaangalia zaidi maisha yetu na ustawi wetu, na hili ni Bunge, siyo Mahakama. Kwa hali hiyo, naunga mkono kwamba kuwe na upana, lakini vile vile iwe ni kutoka katika Vyuo ambavyo vinaeleweka kwa *standards* zetu, kwa misingi kwamba inapotokea huyo mtu anateuliwa, basi kweli vyeti vyake viwe vimewasilishwa. Kwa sababu ukiangalia Katiba ya sasa inasema kwamba mtu hatastahili kugombea Ubunge mpaka awe na akili timamu, lakini sijaona kama tunapimwa kabla ya kugombea Ubunge, ndiyo maana tunapata matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tufute yale maneno yanayoitwa "*in Law, Economics or Political Science*." Sasa sentensi

itasomeka: "*possesses a degree from a recognised University." (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini naomba sifa hiyo iungane kwenye kuongeza "and" baada ya *University*." (b) "*possesses proven."* Naongeza neno, "proven*, experience and competence in chairing Public Assembly or forum*." *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri sasa niwahoji wanaoafiki kifungu hicho sasa kipitishwe kwa mujibu wa marekebisho hayo yaliyoletwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 6

**NDG. ANSELM MREMA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kifungu kipya cha (4) na cha (5), Mheshimiwa Waziri Chikawe amefanya *renumbering*, na hivyo kilichokuwa kufungu cha (4) sasa kinasomeka kama kifungu cha (6) na kina marekebisho ya Mheshimiwa Chikawe, Mheshimiwa Ndugulile na Mheshimiwa Mpina.

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Ndugulile!

**A SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. DR. FAUSTINE NDUGULILE, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KIGAMBONI CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF THE BILL TITLED "THE CONSTITUTIONAL REVIEW (AMENDMENT) ACT, 2013"**

____________

[*Made under Standing Order 86(9) & (11)]*

____________

A Bill titled "The Constitutional Review (Amendment) Act, 2013 is amended as follows:

A. In Clause 4 by deleting the words "relevant institutions" appearing in the third and fifth lines in sub-clause (4).

B. In Clause 6 by deleting the phrase "a period of not more than twenty days" appearing in sub-clause (4) and substituting for it with the following phrase:-

"such period of time that is necessary to complete the deliberations".

Hon. Dr. Faustine Ndugulile (MP.)
**KIGAMBONI CONSTITUENCY**

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Katika kifungu hiki ambacho kimetajwa sasa hivi, kilikuwa kinaongelea kwamba Katibu na Naibu Katibu

watafanya uteuzi wa Watumishi wa Bunge Maalum baada ya kushauriana na *relevant authorities*.

Sasa katika mapendekezo yangu, kwa sababu hatukuwa tumetoa tafsiri ya haya maneno, "*relevant authorities,"* nilikuwa napendekeza kwamba maneno haya yafutwe kwa sababu wanaweza wakafanya *consultation* na hizo *relevant authorities,* lakini kushirikisha hizi *relevant authorities* ambazo hazijaainishwa, maana yake ni nini, inaleta shida kidogo. Kwa hiyo, *relevant authorities* katika mstari wa tatu na mstari wa tano yafutwe ili kifungu kingine kiendelee kama kilivyo.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho tumekifanyia marekebisho. Nilikuwa nafikiria kwamba kilivyo sasa, bahati mbaya sijaona maandishi ya Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile. Lakini kilivyo sasa hapa, maana yake ni kumpa uwezo Katibu wa Bunge na Naibu Katibu wa Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilivyoandikwa sasa, tunampa *Clerk upon consultation with Deputy Clerk and consultation with Attorney General,* wote wawili *and other Public Institutions to nominate such number of staff from the National Assembly* na yeye anaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa zile *Public Institutions* hatuwezi kuwa *exhaustive,* kwa sababu nyingine, kwa mfano, kama unamtaka mtu wa *IT*, utamkuta yuko Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Ukitaka kumpata Askari utakuta yuko Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa hiyo, zile *Public Institutions* twende kwenye Sheria ya *Public Service Act,* utakuta zimekuwa *defined* kwamba ni Idara zote za Serikali. Labda kwa sababu mapendekezo ya Mheshimiwa Dkt. Faustine Ndugulile ni kwamba tufute kifungu hicho, lakini nafikiri anachofanya yeye ilikuwa ni kufuta kifungu hicho kama kilivyokuwa zamani. Sasa hivi kifungu hiki sisi tumekiandika upya na kipo kwenye *further schedule of amendment* ukurasa wa pili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile!

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jinsi alivyokuwa ameisoma *AG,* mimi sina shida nayo. Hiyo *schedule* ambayo anaiongelea, sisi wengine hatuna. Kwa hizo *wording* ambazo anazo yeye, ambazo anasema kwamba kwa kushirikiana Katibu, Naibu Katibu na kufanya *consultation with AG,* watawatoa katika *Public Institution.* Sina shida nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa naomba vilevile Meza yako itusaidie hizo *amendment* nyingi ambazo zinasomwa, sisi wengine hatuna huku. Sina tatizo na hicho kifungu kama kilivyo.

**MWENYEKITI:** Haya utaletewa. Tunaendelea. Mheshimiwa Andrew Chenge, ni kwenye hilo hilo la Mheshimiwa Dkt. Ndugulile?

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Chenge. Mheshimiwa Pindi ni hilo hilo la Mheshimiwa Dkt. Ndugulile?

**MHE. PINDI H. CHANA:** Ndiyo Mheshimiwa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Haya.

Mheshimiwa Mpina, tunamaliza moja moja, tusiyachanganye. Ngoja kwanza twende na hilo kwanza. Mheshimiwa Andrew Chenge.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisimama tu kusema ambacho Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema, kwamba inawezekana Mheshimiwa Dkt. Ndugulile hakupata hii *further schedule of amendment* ambayo ndiyo imepanua uwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika maboresho ambayo Serikali imeleta katika eneo hilo, nilikuwa najaribu kujiuliza, neno '*nominate'.* Maana unapo-*nominate* unategemea mtu mwingine atafanya kazi ya mwisho labda ku-*appoint.* Kwa vile hawa ni wa muda

na ndiyo mtiririko wa kifungu hiki kinavyosema, labda tungelikuwa wazi tu kwamba wata-*select,* maana hawa ni watumishi katika vyombo hivi. Kama ni Wabunge wata-*select* wale wanaodhani wanawahitaji, kama ni kutoka Baraza la Wawakilishi watafanya hivyo; kama ni kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tumekuteua wewe. Sasa nilikuwa na shida ya neno '*nominate'* kwa Kiingereza.

Katika kifungu kidogo kinachofuata, panaposema: "*the staff under sub-section (4) shall be nominated through secondment",* sasa nilikuwa na shida ya Kiingereza. Mimi nilikuwa nafikiria tungesema: "*the staff selected under subsection (4), shall be on secondment for the prescribed period of the Constituent Assembly".* Kwa hiyo, '*nomination'* mimi naona ni tatizo. Ukisema '*select'* ndiyo inakuja vizuri, maana wanawateua wao wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Pindi Chana!

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niko katika kifungu hicho hicho. Wakati tunajadili, *spirit* ilikuwa ndiyo hiyo '*secondment'.* Sasa wataalam wa lugha watatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, katika kifungu hicho tunaambiwa kwamba "*the Clerk of the Constituent Assembly shall upon consultation with the Deputy Clerk."* Wao wameandika '*nominate'*

*such number of staff from the National Assembly, the House of the Representative, Offices of the Attorney General."*

Saasa mimi ninachodhani, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni *Public Institution*. Kwa hiyo, nilidhani tusitaje *Office of the Attorney General* kwa sababu yeye yupo *under Public Institution,* na pale mbele anasema: "*of the United Republic and Zanzibar and from other Public Institution.*" Kwa kuwa *AG* ni *Public Institution,* naomba kushauri, *Office of the Attorney General* itoke, ibaki neno '*Public Institution'* maana ndani yake kuna watu wengi, yaani wataazimwa kutoka maeneo mbalimbali. Wamesema wataazima kutoka Ofisi ya Bunge na *Public Institution*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Public Institution* Kiswahili chake ni Taasisi za Umma. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni Taasisi ya Umma. Lakini tukiisema Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, ipo ndani ya Taasisi ya Umma! Sasa Taasisi za Umma nyingine hatujazitaja, tumezi-*generalize*.

Kwa hiyo, naomba sana hii Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iwe ndani ya Taasisi za Umma. Maana yake inawezekana tukahitaji watu kutoka Idara ya Mahakama na Mahakama nayo itabidi tutaje. Lakini hizo zote ni Taasisi za Umma mradi siyo *Private Sector,* siyo *NGO*, siyo *Religious Organization. For the purpose of this work* ni Taasisi za Umma. Vinginevyo, tuna mihimili mitatu na *Judiciary* wapo. *We can need judiciary people in one way or another*. *So*, tuseme tu

Taasisi za Umma. Mwanasheria Mkuu ni Taasisi ya Umma. Naomba kushauri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda nianze na hili la Mheshimiwa Chenge. Sina tatizo la ku-*select* badala ya ku-*nominate* ingawa *reference* ni ndogo, lakini sina tatizo la '*select*.'

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili la kuweka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Pindi Chana ni Mwanasheria na anajua *rules of interpretation* kwa sababu maneno aliyotaja pale mwanzo ametaja the *National Assembly and House of Representatives,* ni lazima uweke mbele sasa watu ambao wapo *relevant* na *issue* ya Bunge lile ambao ni Waandishi wa Sheria, na wale Waandishi wa Sheria huwezi kuwapata kwenye Bunge, utawapata kwenye Ofisi zetu sisi. Unaweza kuondoa bado ukasema ni *Public Institution*, lakini unajua hakuna ziada mbaya. Hakuna tatizo la kurudia maneno katika Uandishi wa Sheria.

Kwa hiyo, nilikuwa nashawishi kwamba ibaki kwa sababu mambo haya tunavyokwenda unaona upande huu, tuwe *specific* kwamba ni *Attorney General and Public Institution.* Sasa zile *Public Institutions* zinakuja kwa sababu umemtaja *Attorney General*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwenye neno '*select'!* Mheshimiwa *AG,* ile '*nominate'* na '*select'!*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naungana kabisa na mawazo ya *AG*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pindi Chana sijakupa nafasi.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Aaah! Nimesikia Pindi, samahani!

**MWENYEKEITI:** Eeh, kwa sababu tumeshamaliza, maana yake sasa nakwenda kuhoji, yaani sirudi tena kwa mujibu wa Kanuni.

Mheshimiwa *AG* ananiambia pale kwenye '*nominate'* anakubaliana na Mheshimiwa Chenge kwamba tunaweka '*select'* na ameongeza ile pale *Public Institution* pamoja na *Chamber* ya *Attorney General*. Kwa hiyo, sasa naenda kulihoji Bunge, haturudi tena kwako wewe mtoa hoja.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nawahoji kwa kuzingatia marekebisho haya yaliyofanyika na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

**KATIBU MEZANI – NDG. ANSELM MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna *amendment* ya Mheshimiwa Mpina.

**MWENYEKITI:** Aah, samahani sana.

Waheshimiwa Wabunge, naomba kufuta upitishwaji wa Ibara hiyo ya (6). Tulisahau marekebisho ya Mheshimiwa Luhaga Mpina. Mheshimiwa Mpina.

**SCHEDULE OF AMENDMENT TO BE MOVED BY HON. LUHAGA JOELSON MPINA, MEMBER OF PARLIAMENT FOR KISESA CONSTITUENCY AT THE SECOND READING OF THE BILL TITLED "THE CONSTITUTIONAL REVIEW (AMENDMENT) ACT, 2013"**

---

[*Made under Standing Order 86(9) and (11)]*

---

The Bill titled "The Constitutional Review (Amendment) Act, 2013" is amended as follows:-

Clause 4

by deleting words "Relevant Institutions" appearing between the words "and" and "appoint" in the third line and substituting for them with the word "Minister".

Hon. Luhaga J. Mpina (MP.)
**KISESA CONSTITUENCY**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho ambacho kimejadiliwa sana, pale kwamba "*upon consultation with the Deputy Clerk, nominate";* mimi nilifikiri kwamba ingekuwa busara sana kama katika *consultation* hiyo, Waziri mwenye dhamana ya Katiba na Sheria akawa miongoni mwa watu ambao wawe *consulted,* kwa sababu hili jukumu la kuweka watumishi ni jukumu kubwa, lakini vilevile yeye anakuwa ni kiungo kikubwa sana kati ya watumishi ambao watatoka kwenye *Public Institution* kuunganisha na Bunge, kwa maana ya kwamba kwa kule Zanzibar tunaye Katibu Mkuu wa Baraza la Wawakilishi ambapo hakutakuwa na tatizo katika uteuzi wa Uwakilishi kutoka kule. Hapa tunaye Katibu wetu wa Bunge, vilevile hakutakuwa na tatizo kabisa na uteuzi. Lakini sasa tunapofika kwenye *Public Institution,* kiungo chetu ni nani katika *Public Institution?* Kiungo chetu ni Waziri mwenye dhamana ya eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikuona sababu kwa nini Waziri amejitoa kabisa katika jukumu hili, kwa sababu mwisho wa siku kwa mfano, kama ilivyokuwa imeandikwa zamani, ilikuwa ni kwamba huyu Katibu Mkuu ata-*consult* huyu *Deputy Clerk* pamoja na *Public Institution.* Sasa ukizitaja tu *Public Institution,* hakuna mtu ambaye tumemfunga kengele pale. Mwisho wa siku wakishindwa kutoa ushirikiano tutamhoji nani? Tutamwuliza nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalishawishi Bunge kwamba hapa tuongeze neno '*Minister'* na bahati nzuri

neno '*Minister'* kule kwenye *definition* imetafsiriwa kwamba ni Waziri aliyepewa dhamana ya Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu ni hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hilo nalikubali, lilikuwa ni moja ya mapendekezo yetu ya awali ambayo tulibishania kidogo, lakini sasa kwa sababu Waziri mwenyewe ndiye mimi, nikasema sijui nikubali au nikatae! Nikasema basi nyie mliamulie. Kwa hiyo, mimi nalikubali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Pindi Chana, bado upo katika hilo tena?

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiniruhusu, naomba nitoe ufafanuzi, samahani lakini. Kama Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi kidogo!

**MWENYEKITI:** Sawa Mheshimiwa Pindi Chana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa ridhaa. Wazo hilo la kumweka Waziri ni nzuri, lakini wakati wa kujadiliana tulisema Bunge la Katiba halina *front bench* wala *back bench.* Hakuna Mawaziri, wote ni *delegates.* Ndiyo maana kuna mahali alitajwa Spika, wakasema aah, hebu tuache. Mle hakuna Spika, hakuna mtu anayekuja na koti lake,

wala hakuna Waziri wa Katiba na Sheria. Wote tunaingia kama *delegates*.

Kwa hiyo, kwenye Kamati tulilijadili sana, tukasema: Je, Mawaziri wengine? Kuna Waziri wa Muungano, kwa nini umtambue Waziri wa Katiba na Sheria na mle kuna masuala ya Muungano?

Kwa hiyo, tukasema wote waingie kama *delegates* kwa sababu utaratibu wa kufanya *secondment,* kuchukua watu kutoka kwenye Taasisi moja au nyingine ni masuala ya Utumishi, yanaeleweka. Tukianza kuweka Mawaziri, ndiyo hofu iliyoko. Kama mchango huu utasaidia Bunge lako au Kamati hii, nashukuru. Mtakachoamua, nitaunga mkono, lakini tulisema Bunge la Katiba halina Mawaziri, wote tunakuwa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mpina, bado nitarudi kwako. Ngoja, tunafanya majadiliano, tunarudi kwa mtoa hoja. Ngoja sasa Mawaziri wajibu halafu tutarudi kwako. Mheshimiwa Angellah Kairuki, halafu Mheshimiwa Waziri wa Utumishi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo Mheshimiwa Mpina ametoa hoja yake na kama ambavyo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na masuala ya Katiba alivyoridhia; kwanza kabisa naomba nimweleweshe

Mheshimiwa Pindi Chana kwamba, ni kweli kwamba Waheshimiwa Wabunge wote wa humu ndani na Wawakilishi wote wataingia kama Wajumbe wa kawaida ili waweze kuungana na Wajumbe wengine wale 166 bila kuja na kofia zao. Suala hili ni kabla ya Bunge hilo Maalum halijaanza kazi. Bado michakato ya uteuzi ipo na bado ukiangalia mwisho wa siku Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Mambo ya Katiba, kwa kufanya mashauriano na Taasisi nyingine husika labda na Mheshimiwa Waziri wa Utumishi wa Umma, bado jukumu hili huwezi kulikwepa. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mtoa hoja, Mheshimiwa Mpina!

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu imekubalika, sina hoja tena. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nitawahoji wanaoafiki kwamba nyongeza ya wakati wa kufanya *consultation*, nyongeza ya Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Katiba awemo katika kifungu hiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG* tumeshahoji, sasa tunarudi tena hapo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yenu ni kutunga Sheria. Sasa tuambieni, kitasomekaje hicho kifungu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho tunaafiki, lakini pia tunaomba kisomeke kama ifuatavyo: "*The Clerk and the Deputy Clerk of the Constituent Assembly, shall upon consultantion with the Minister responsible for Legal Affairs select such number of the Staff from the National Assembly*" na maneno mengine yanabaki kama yalivyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Sendeka!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki kuwarudisha nyuma, lakini nataka kusema tu kwamba unaposema "*upon consultation with the Deputy Clerk*" na ukaongeza na Waziri mwenye dhamana hapo, athari inayoweza kujitokeza ni kwamba Waziri mwenye dhamana ya Sheria wa Jamhuri ya Muungano au wa Zanzibar? Hapo tutaingia kwenye mgogoro mwingine. Ndiyo maana nilikuwa najaribu kusema, nataka niungane na pendekezo la Mheshimiwa Pindi Chana, kama hutaona kama nawarudisha nyuma, kwa afya tu, kwamba jambo hili liachwe kwa *Clerk of the National Assembly* na *Deputy* wake kama ilivyo hapa mwanzoni. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nasema, kama mkianza kumwingiza Waziri wa Sheria wa Jamhuri ya Muungano itabidi tena tumwingize na Waziri wa Sheria wa Zanzibar. Tutaanza kuleta migogoro. Tuwaachie Watendaji kwenye ngazi hii na haki kama mnavyosema, siyo tu kwamba inatakiwa itendeke, lakini inatakiwa ionekane inatendeka.

Kwa hiyo, kuondoa ukungu wa Waziri ambaye ana dhamana nyingine, hebu tuiondoe sisi ambao tuna Vyama, tuwaachie wale ambao hawana Vyama kwenye hatua hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chenge, nilikuona umesimama!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Hapana.

**MWENYEKITI:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ukiangalia katika Sheria mama, katika kifungu cha (3) kinachotoa tafsiri ya maneno yaliyotumika katika sheria, kinaeleza kabisa kwamba Waziri maana yake ni Waziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano mwenye dhamana ya mambo ya Katiba. Labda tu useme kwa kuboresha ambayo kimsingi na Mheshimiwa Waziri sidhani kama ana matatizo nalo, tunaweza tukaamua basi Waziri huyu wa Jamhuri ya Muungano anaweza akashauriana na

kukubaliana na Waziri wa Sheria wa Zanzibar, kama inawezekana.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo limezungumzwa kwenye Kamati na Kamati tulikubaliana nayo kwamba katika kifungu hicho tungemwondoa Waziri kikabaki kama kilivyo. Sasa kwa sababu hakuna sababu nyingine muhimu ya maana inayofanya turudishe tena *concept* ya Waziri, mimi nashauri kwamba kifungu hicho kibaki kama kilivyo bila kumweka Waziri wa Katiba na Sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wajumbe, baada ya kupata mjadala mzito, mzito kweli, wenye hoja nzito, nafikiri sasa tumalize.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tuhoji wanaoafiki kwamba kifungu hicho kibaki kama kilivyoelezwa mara ya kwanza na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu bila kumwingiza Waziri kwa mapendekezo ya Mheshimiwa Mpina waseme 'Ndiyo' na wasioafiki waseme 'Siyo.'

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, marekebisho ya Mheshimiwa Mpina hayazingatiwi kwenye mabadiliko haya.

Ibara ya 7

**NDG. ANSELM L. MREMA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kifungu kipya cha (7) kilichowasilishwa na Waziri wa Katiba na Sheria - Mheshimiwa Chikawe.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama katika kifungu kipya cha (7).

**MWENYEKITI:** Kifungu kipya cha (7)!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Ambacho amekisema Katibu.

**MWENYEKITI:** Ehe, Kifungu kipya cha (7).

Waheshimiwa Wabunge, naomba muwe mnasimama haraka!

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sheria mama tuko katika kifungu cha 26. Niseme tu, kwa sababu baadhi ya hawa walioleta *schedule of amendment* yawezekana usomaji wa marekebisho ukiyaunganisha na Muswada pamoja na Sheria mama yanawachanganya.

Mheshimiwa Jafo alikuwa na pendekezo kwenye ibara ambayo tumeshaipita, lakini naona labda ameshaiacha, sijui! Hoja yangu katika eneo hili ni

ndogo sana kwenye ibara ndogo ya (6), tunapotumia neno "*presumed*".

Kwanza niipongeze sana Serikali kwa kuja na wazo hili la kuvunja kama kuna *deadlock*, wamefanya kitu kizuri sana. Neno "*presumed"* nilikuwa nadhani tufikirie neno lingine. Kwa nini tusiseme "*Shall be deemed*"? "*Presumption"* inaleta, *you know*, yaani maneno yetu ya kisheria kule kwenye masuala ya ushahidi na nini, lakini hii itachukuliwa kama imepitishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo nilikuwa napendekeza hiyo kwamba badala ya neno "*pressumed"* kwenye ibara ndogo ya (6) "*Upon completion of voting under subsection (5), the proposed constitution shall be presumed."* Ndiyo nilikuwa nasema tupendekeze *"Shall be deemed to have been passed by the Constituent Assembly and provisions of the referendum act shall apply."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**: Kwanza haya maneno ya "*presumption"* na "*deeming"* kwa kweli ni *semantics,* yote yanafanana. Nafahamu Mheshimiwa Chenge alikwenda Havard, mimi nilikwenda *America.* Hayana tofauti kubwa, lakini kama inaleta uelewa unaofaa, basi tutoe neno "*presumption"* iwe "*be deemed*." Kwa sababu hata sisi wenyewe kwenye *drafting* tumetumia kama saa nne kubishana kuhusu

maneno hayo. Kwa hiyo, tuweke tu "*Shall be deemed to have passed by the Constituent Assembly".*

**MWENYEKITI:** Haya, kifungu hicho pamoja na marekebisho ya Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanaafikiwa?

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

Ibara ya 8

**NDG. ANSELM L. MREMA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kifungu kipya cha (7), Mheshimiwa Waziri Chikawe amefanya *renumbering*, ambapo sasa kifungu cha (5) na (6) kinasomeka kuwa kifungu cha (8) na (9). Kifungu cha (8) hakina marekebisho.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila Mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

**NDG. ANSELM MREMA - KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha (9) kina mabadiliko ya Mheshimiwa Dkt. Ndugulile.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ndugulile!

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki katika marekebisho ya

sheria inaonesha kwamba Bunge la Katiba litakaa kwa muda usiozidi siku 70 na kwamba kama muda huo hautatosha, basi Rais kwa kushauriana na Rais wa Zanzibar wanaweza wakaongeza muda mwingine usiozidi siku 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu hapa ni kwamba, majadiliano ya rasimu hii ya Katiba yanaweza yakawa marefu zaidi. Sasa iwapo tutajifunga kwamba ndani ya siku 90 suala hili litakuwa limekamilika, hatuna tena *leeway* ya kutoka pale, labda tena tulete marekebisho mengine ya sheria ili hicho kifungu tuweze kukiondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili mapendekezo yangu yalikuwa ni kwamba katika *phrase* ambayo inasema "*A period of not more than 20 days*", tuiondoe ile ili itupe nafasi na *room* na *flexibility* kwamba majadiliano haya yanaweza yakaendelea, ili hizi taratibu nyingine hizo za kura ambazo tulikuwa tumeziongelea, ziweze kukidhi badala ya tena ya kuja na mchakato mwingine wa kurekebisha sheria ili kuruhusu mchakato kuweza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo ilikuwa hoja yangu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nalo lilituletea maneno, tukalijadili sana. Lakini wenzetu wa Zanzibar walipendekeza kwamba isizidi siku 20. Baadaye tukaizungumza tukasema tumwachie Mwenyekiti azungumze na Mheshimiwa

Rais, lakini hatukuweka kikomo. Sasa haya ni mambo ya fedha. Mkiacha tu *open handed,* hilo Bunge linaweza likaendelea mpaka wakati wowote tu. Watu si wanasaini posho?

Kwa hiyo, nadhani kama tuna wasiwasi labda siku 20 hazitatosha, tulifunge tena, tuseme basi Mwenyekiti anaweza akaongeza akishauriana na Mheshimiwa Rais o*fcourse* kwa ajili ya bajeti, siyo zaidi ya siku 10 baada ya zile siku 20 kwisha.

**MWENYEKITI:** Mh! Umemaliza Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Nimemaliza.

**MWENYEKITI:** Wangapi mnasimama katika hoja hii kusudi tumalize? Maana yake tukisema hapa tunaendelea halafu watu wamesimama tena! Haya, nimekuona Mheshimiwa Chenge, Mheshimiwa Pindi Chana halafu tutarudi kwa Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. ANDREW J. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana sana na Mheshimiwa Ndugulile kwamba masuala ya mchakato wa Katiba mara nyingi yanakuwa na mjadala mrefu na hauwezi ukatabirika. Lakini wakati mwingine lazima tuangalie upande wa sarafu kwamba haliwezi tu likaachiwa watu waendelee kuzungumza maana lina gharama kubwa kwa hili zoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mambo mawili. La kwanza, kuuliza kama *schedule of*

*amendment* hii ya Serikali tunaachana nayo kwenye eneo hili? Maana na wenyewe walijaribu kuliona hilo. Kwa vile ni Muswada wa Serikali, wana haki kabisa ya kurejesha kama ni siku 20; unaongeza siku 20, unapima sasa kazi iliyopo, maana lazima ijengewe hoja, kwa nini mnahitaji siku 20? Zile *contentious issues,* mnadhani mnaweza mkazimaliza ndani ya muda huo? Kama hazitamalizika, ndiyo wazo la Serikali sasa kwamba ziongezwe siku 10 nyingine inakuwa kama siku 30 ndiyo mwisho. Siku 20 na 10 inakuwa siku 30 jumlisha na siku 70 unapata hizo siku 100. Sasa nadhani kwa dhana hiyo ya Serikali kwa kutambua gharama, lakini pia umuhimu wa mazungumzo katika Bunge Maalum la Katiba lipewe muda wa kutosha siku 20 na 10 nadhani inaweza ikawa kitu kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami wala siko mbali. Hapa mkononi mwangu nina *schedule of amendment* ya Serikali inayosema kwamba "Mwenyekiti wa Bunge la Katiba kwa kushauriana na Makamu Mwenyekiti na kwa kushauriana na Rais wanaweza waka-*extend the period under section (3) for such period as may be appropriate to accomplish the function of the Constituent Assembly.* Haina siku 10. Hii ambayo Wajumbe tumewagiwa, haina hizo siku 10.

**MWENYEKITI:** Tunayo Mheshimiwa?

**MHE. PINDI H. CHANA:** Ya siku 10 eh!

**MWENYEKITI:** Ah, hapana. Tuliyonayo hapa haina siku 10. Sasa tunaomba tu ushauri wako kwenye suala hili, kwa sababu tunajadili hoja ya Mheshimiwa Ndugulile.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Haya. Mheshimiwa Ndugulile amesema tusijifunge. Sheria inasema Bunge la Katiba litakaa siku 70. Baada ya siku 70 pale kulikuwa na maelezo kwamba kama kazi haijakamilika tutaongeza siku 20. Wasiwasi ni kwamba, kuna kifungu hapa tumeongeza kwamba tunaweza tukapiga kura ile *two third* mara mbili na kama haijakamilika, kuna ile *simple majority*. Haya mambo ya kura kutakuwa na *negotiation*, labda vipengele ambavyo hatujakubaliana vinahusu nini, watu wakajadili kwenye Kamati waje wapige kura tena, mara mbili mwisho tunaenda *simple majority*.

Sasa katika zile shughuli za kura na nini, unaweza ukahitaji wiki tatu, nne, tano, ndiyo maana tunasema tusijifunge kusema kwamba ni siku 20. Ila Mwenyekiti atakayekuwepo na Makamu watashauriana na Rais kuona muda unaofaa. Muda unaofaa inaweza ikawa siku tano, wala huhitaji siku 20 wala 30, lakini pia inaweza ikawa ni zaidi ya siku hizo.

Kwa hiyo, tukifunga, itabidi turudi Bungeni tuje turekebishe sheria. Maana tumeshafunga tena! Kama utasema siku 30, na ndani ya siku 30, yaani miezi mitatu hatujamaliza kazi, lazima tuitishe Bunge la Jamhuri ya Muungano tukarekebishe hicho kifungu cha Sheria

kutoa ruhusa kuongeza zaidi ya zile siku zilizoko kwenye sheria. Lakini ukiacha wazi, maana yake tuko huru kutumia siku mbili, siku tatu kadri itakavyoonekana inafaa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, naungana na mapendekezo aliyoleta Mheshimiwa Ndugulile kwamba tusifunge zile siku. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na kunakuwa na Kamati ya Uongozi kwa kujadiliana na kwa kushirikiana na Rais wataona ni siku ngapi zinafaa.

Pia alichosema Mheshimiwa Waziri, mimi nina *schedule of amendment,* haina siku 10. Naomba niungane na hii *schedule of amendment* ya Serikali, anasema: *"For such period as may be appropriate to accomplish the functions of the Constituent Assembly".* Naomba kushauri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile wewe ndio mtoa hoja, wala usiwe na haraka. Ngoja watu wachangie, watoa hoja wajibu halafu ndiyo tutakuja kwako kama unaridhia ama vipi. Tunapolihoji Bunge, hatukurudishii wewe *in between*.

Waheshimiwa Mawaziri wawili naona wamesimama. Mheshimiwa Mkuchika halafu tutamalizia na Mheshimiwa Chikawe ili turudi kwa mtoa hoja tufunge hoja yetu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTAWALA BORA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, marekebisho niliyonayo hapa hayazungumzi siku 10 wala 20, lakini mmeingiza hapa

hofu ya kwamba inaweza siku zikaongezeka sana ikawa gharama kwa Serikali. Imewekwa hapa kwamba siku zitaongezwa baada ya kushauriana na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar. Bila shaka watakapokwenda kuomba siku za nyongeza, watakuwa wamefahamu au wamekisia kwamba kazi iliyobaki tunahitaji siku 20 au siku saba.

Hofu ya kujifunga hapa ni kwamba mnaweza mkazitoa hizo siku 30, hawa watakwenda kuomba na wakikuta kwamba kazi iliyobaki inazidi zaidi ya siku 30; hatuna haja ya kujifunga kwa *assignment* ambayo hatujui kwamba inahitaji siku ngapi.

Kwa hiyo, ili mradi Marais wako pale watafuata wale wawili, watakapokwenda kuomba *extension,* wataeleza juu ya uzito wa kazi iliyopo. Kwa hiyo, nashawishika kusema kwamba haya marekebisho yaliyoletwa na Serikali bila ya kujifunga muda, yako sahihi kabisa. Naomba yaungwe mkono. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Chikawe.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya tulivyoyaleta ilikuwa ni *consensus* ya kwenye Kamati.

**MWENYEKITI:** Haya ambayo tunayo hapa Mezani?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Haya ambayo mimi nimeyaleta ilikuwa ni *consensus* ya Kamati na kweli yalifunguliwa. Nimeunga mkono mapendekezo ya

Mheshimiwa Ndugulile zaidi na nimeweka ukomo zaidi kwa sababu mbili. Moja kuongeza zile siku 10, ni kuwa na *definite period,* wala hatuna haja ya kurudi kwa Rais. Tukirudi kwa Rais tunali-*politicise* jambo hili na *in case of a stalemate;* sasa *stalemate* imetokea, mwamuzi anakuwa ni Rais, unaona! Watasema aah, ni Rais ndiye ameongeza siku tano! Ni Rais amekataa kutuongezea siku! Nasema tuiweke humu kwenye sheria siku 70, baada ya hapo siku 20, baada ya hapo Mwenyekiti na wenzake washauriane, lakini wasizidi siku 10, libaki ndani ya sheria hii liwe *very clear.* Tusimwingize Rais, mnatia siasa kwenye mambo ambayo pengine hayastahili.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Mheshimiwa Chikawe unachotaka kutuambia, unahama kwenye *amendment* yako ya Serikali?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA**: Ndiyo!

**MWENYEKITI:** Unakwenda sasa kwenye *amendment* ya Mheshimiwa Ndugulile?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Nimekwenda kwenye *amendment* ya Mheshimiwa Ndugulile na nime-*improve*.

**MWENYEKITI:** Eh! Kazi mpya sasa! Haya mtoa hoja. Ah, *AG*! Ngoja kwanza mtoa hoja.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na hoja zote hizo.

Lakini nataka tujue kwamba huu mchakato una *road map* kwamba ifikapo tarehe 26 Aprili, 2014 tuwe na Katiba mpya. Hayo ndiyo maagizo niliyopewa na sijapata maagizo mengine. Kwa hiyo, hii *amendment* ambayo ana-*propose* Mheshimiwa Ndugulile, haina kikomo. *Amendment* ambayo tumeleta sisi, kikomo chake cha muda kinawekwa na Mheshimiwa Rais baada ya kushauriana na Mwenyekiti wa Tume. *(Makofi)*

Sasa ni kweli kwamba muda wa kufanya hii kazi unajulikana, siku 70. Kama hazitoshi, itakuwaje? Kama Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Katiba hawakai Bungeni, wanatokatoka na hoja zinacheleweshwa, isipomalizika hizo siku 70 utafanyaje? Wakasema *Okay*. Tulipowasiliana na Zanzibar wakasema ongezeni siku 20. Lakini kwenye Kamati wanasema inawezekana hii *consultation* kwa sababu Katiba inapatikana kwa majadiliano, ni *consensus* na lazima mta-*negotiate* tu. Wanasema inawezekana nazo siku 20 hazitoshi. Sasa ndiyo tukasema, tukiweka siku 100, yaani unafuta kile kifungu, unaweka siku 100; tunasema kwa nini tusiweke *appropriate,* yaani Rais akiona mazingira yanaruhusu, basi waongeze siku, lakini kwa vyovyote vile tunafahamu kwamba Mheshimiwa Rais naye anajua hiyo *road map* ya tarehe 26 Aprili, 2014.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwamba tusijifunge sana kwenye siku na marekebisho yanayofanywa na Serikali ambayo yanaletwa kwenye jedwali, yanaweka ukomo kwa maneno "*appropriate*". *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunafikiri kwamba tumwachie Mheshimiwa Rais hiyo nafasi kutegemeana na hali itakavyokuwa na jinsi mtakavyokuwa mnafanya kazi kwenye Bunge la Katiba. Ukisema kwamba "*Such period of time that is necessary to complete the functions"* ndiyo mapendekezo tuliyonayo sisi. Hii *"as necessary"* ndiyo hii "*appropriate*" kama ukianza kuchambua maneno haya Kiingereza. Ukisema "*Such period of time that is necessary to complete the functions,*" ndiyo hiyo *"as appropriate"* ambayo iko kwenye mapendekezo ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile, tuhitimishe hoja sasa.

**MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Wabunge wote waliokuwa wamechangia hoja hii. Lengo letu hapa ni kutengeneza Katiba nzuri. Natambua kabisa kwamba tuna *roadmap* ambayo inatutaka itakapofika tarehe 26 Aprili, 2014 tuwe na Katiba mpya. Katiba hiyo mpya tutaipata kwa majadiliano ambayo yatakuwa yanaendelea katika Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina tatizo na siku 70 za mwanzo. Wasiwasi wangu ni kwamba tukijiwekea kikomo hapa, iwapo yale majadiliano hatutaweza kuyatimiza pale, itabidi sasa turudi tena huku tufanye marekebisho ya Sheria ili tuweze kuendelea na majadiliano, tutazidi kupoteza siku.

Mimi ninachokisema hapa ni kwamba siku 70 zile za mwanzo tukubaliane kimsingi, lakini tusiwabane Mwenyekiti pamoja na Mheshimiwa Rais na Rais wa Zanzibar kwa kuwapa kikomo cha siku za ziada thelathini. Tunaweza kuifanya hii ndani ya siku tano, tunaweza kuifanya ndani ya siku moja, ama tukaifanya ndani ya siku kumi au ikawa zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi hoja yangu bado iko pale pale. Tusiwape kikomo kipindi cha pili, tuwape muda ili kazi hii ifanyike kwa ufanisi ili kuleta hoja katika...

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, unakubaliana basi na hoja iliyoletwa na Serikali kwa sababu hoja iliyoletwa na Serikali ndiyo inabeba hayo unayoyazungumza wewe. Ukirudi kwenye hoja yako, unahamisha maana ya kile ambacho kimezungumzwa na Serikali. Sasa kwasababu hivyo ndivyo Mheshimiwa Ndugulile unavyo...

**MHE. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nifanye ufafanuzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndugulile, naomba tu uketi kwanza.

Ninachotaka kusema hapa, kama kweli tunakubaliana kwamba tusijifunge, tuache Mwenyekiti wa Bunge na Makamu wake wafanye *consultation* na viongozi wetu ili tusirudi tena kwenye Bunge hili kuongeza muda. *Amendment* hii ya Serikali ndiyo

inabeba dhana hiyo. Lakini tukiondoka, tukaja kwenye hii ya kwako, ndiyo sasa tunatengeneza ile mantiki ya kufunga siku. Tutakuwa tunatumia siku maalumu, na kama hatujamaliza inabidi sasa Sheria imekwishapitishwa turudi kwenye Bunge hili ili tuzifungue siku zile tena, halafu twende tena kuanza na hiyo kazi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri tufikie tu hatua tuhoji kifungu hiki.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nahoji wanaoafiki marekebisho haya ya Serikali ndiyo yanatoa ule mwanya wa kuwa *flexible* katika kufanya kazi hii na kuikamilisha.

Waheshimiwa Wabunge, walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi sana kwamba sikuwa makini wakati tunazungumzia ukurasa wa kwanza wa marekebisho ya Serikali kwenye Kifungu kipya 22 (a). Naomba radhi sana, kwa sababu tusipofanya hivi tutarudi tena kufanya marekebisho haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hicho kinahusu uchaguzi wa mtu atakayeendesha zile *proceedings* za mwanzo, yaani Mwenyekiti wa muda na kinasomeka kama ifuatavyo: "*Without prejudice to the provisions of section 23 after the convening of the Constituent Assembly, the Clerk of the National Assembly and the Clerk of the House of Representatives, shall manage and supervise the process of electing the in term chairman of the Constituent Assembly who shall be responsible for."* Sasa ukisoma yale maneno "*developing and adopting",* huyu hana mamlaka ya ku-*adopt.*

Kwa hiyo, nilikuwa napendekeza maneno "*be responsible for"* yafutwe na badala yake maneno "*who shall preside over the proceedings of the assembly for the purpose of (a) developing and adopting the standing orders and be conducting the elections of the..."* hayo yaendelee kama yalivyo. *(Makofi)*

Nilikuwa nasema kwamba, ukisoma yale maneno yalivyo sasa, Kiingereza haki-*flow* vizuri kwasababu unampa *in term chairman* mamlaka ya ku-*adopt standing orders,* siyo kazi yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG* tunakushukuru. Kwa hiyo, pale baada ya "*who shall"* ile *"be responsible"* ndiyo tunaiondoa pale?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unafuta maneno *"be responsible for" and then* unaweka nitaweka, kwenye *dictation speed. "preside over the proceedings of the assembly for the purpose of,"* unaweza kusema *"purposes of"* halafu (a) na (b) inaendelea kama kawaida.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na Marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa Mwaka 2013**
***(The Constitutional Review (Ammendment) Bill* 2013.**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 89 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la 2013, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2013, *(The Constitutional Review Amendment Act 2013),* Ibara kwa Ibara na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba wa mwaka 2013 *(The constitutional Review Amendment Act 2013)* kama ulivyorekebishwa katika Kamati ya Bunge Zima sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa kwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba kutamka kwamba Bunge sasa kwa hatua zote za Kikanuni limepitisha Muswada huu wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya wa mwaka 2013. Naomba kuwapongezeni sana kwa kazi hii nzito inayobeba dhamana na hatima ya Taifa la Tanzania na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Ninachoweza kusema kwenye Kiti hiki leo baada ya kupitisha Muswada huu, ni kuwaomba Watanzania wote waone umuhimu wa zaoezi hili muhimu sana la kuamua mustakabali wa Taifa letu la Tanzania na hasa kwa kuzingatia Utanzania wetu zaidi na siyo kitu kingine chochote. *(Makofi)*

Vile vile nichukue nafasi hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kushirikiana kwa kazi hii, lakini ninaamini kwamba Watanzania wote sasa tutumie nafasi ya kutosha kumwomba Mwenyezi Mungu ili mchakato huu wa Katiba ufike mahali unapotakiwa salama kwa amani na utulivu na kwa kweli nchi yetu iendelee kupata maendeleo kutokana na hayo yatakayoamuliwa katika hiyo Katiba mpya tunayokwenda kuitengeneza.

Waheshimiwa Wabunge, niliwasihi sana wale Waheshimiwa Wabunge waliokuwa wameniomba Miongozo asubuhi kwa kuona kwamba tunaendelea kupoteza sana muda kwa ajili ya Miongozo, niliwasihi sana. Nimeshawatambua wote kwenye orodha yangu, kwa hiyo, wanipe subira tumalize kazi hizi ambazo Watanzania walikuwa wanapenda kusikia tunahitimishaje, halafu tupeane nafasi ya kusikiliza Waheshimiwa Wabunge wanasema nini.

Sasa muda huo huo ninao angalu kama dakika kumi hivi, kabla ya saa 8.00, sasa kama wako ndani ya ukumbi wa Bunge, wale wanaoomba hiyo Miongozo nitawapa nafasi kwa dakika angalau moja moja tu.

Mheshimiwa Said Nkumba naona yupo, Mheshimiwa Ole-Sendeka yupo, Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla yupo, lakini wengine kama Mheshimiwa Mnyaa simwoni, Mheshimiwa Msigwa, simwoni; Mheshimiwa Machali, simwoni; Mheshimiwa Mkosamali; simwoni; Mheshimiwa Lissu na Mheshimiwa

Mnyika; hawako. Kwa hiyo, ngoja niwape nafasi niwasikilize. Kwa kweli nilisema hivyo na nilitumia Kanuni ambayo inanipa madaraka ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Said Nkumba, dakika moja tu tafadhali. Hatuna muda, tuna shughuli ya kusikiliza hotuba ya Waziri Mkuu jioni.

**MHE. JUMA S. NKUMBA** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nami nitajitahidi kusema kwa kifupi. Jana kulitokea mtafaruku hapa Bungeni kwa hoja kwamba...

**MWENYEKITI:** Kanuni ya ngapi Mheshimiwa Nkumba?

**MHE. JUMA S. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(7)

**MWENYEKITI:** Endelea.

**MHE. JUMA S. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jana kulitokea mtafaruku hapa Bungeni kwa hoja kwamba baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliodai kwamba Zanzibar haikushirikishwa katika majadiliano ya Muswada ambao tumeumaliza leo hii.

Sasa Mwenyekiti wa Kamati alithibitisha kwamba Zanzibar ilishirikishwa kwa Wadau, lakini vilevile Mwanasheria Mkuu alituthibitishia barua zilizotoka kwenye Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo zilisainiwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwasababu sisi hapa ni Waheshimiwa Wabunge na tuko hapa kuwawakilisha Watanzania wote na tungependa kujua ukweli wa jambo hili na Watanzania huko nje wajue ukweli wa jambo hili; na kwasababu Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar leo yuko hapa ndani, ningependa kupitia Mwongozo wako kama unaweza kumruhusu ili atupe maelezo ambayo yatathibitisha haya ambayo tulitolewa jana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Ole-Sendeka, dakika moja tu, muda tafadhali!

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelekezo yako nitatumia muda huo japo nilikuwa nimesimama mara mbili kwa hoja mbili tofauti kwa Miongozo miwili, Kanuni ya 68(7) na Kanuni ya (5); nilikuwa kwenye msiba, lakini nilifuatilia mwenendo mzima wa mambo yaliyokuwa yakiendelea Bungeni jana, lakini nikafuatilia na kugundua kwamba kulikuwa na uamuzi wa Spika au Naibu Spika aliyekuwa anakaa kwenye Kiti hicho ulichokalia na akatoa msamaha kwa kusema tuyapuuze yale. Lakini kulikuwa na kitendo kingine cha ziada kilichotokea nje ya jengo hili ambapo mmoja wa Wabunge waliotolewa nje alichukua hatua kinyume kabisa na matarajio ya Bunge lolote linalojiheshimu ya kumpiga Askari ngumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Mjini - Mheshimiwa Mbilinyi alifanya hatua moja ya fedhaha inayolifedhesha Bunge lako na siyo kwamba alipuuza maamuzi ya Kiti, lakini alichukua hatua ya kumpiga Askari.

Sasa kwa kuwa Katiba Ibara ya 100 inalinda uhuru wa majadiliano na mawazo na utaratibu ndani ya Bunge, lakini sijui ni kwa kiasi gani italinda heshima, utu na kwa kweli hadhi ya Askari ambao wanatii amri ya Kiti chako ili usalama wa maisha yao uweze kuwepo, lakini pia heshima ya Bunge hili iweze kulindwa. Je, hatua hiyo inalindwa ya Mbunge kuchukua hatua ya kufanya kosa la jinai la kumpiga Askari kwa kisingizio cha uhuru unaotolewa na Ibara ya 100?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Kiti chako kiweke bayana.

**MWENYEKITI:** Inatosha Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, tumekuelewa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ole-Sendeka nadhani kwa ajili ya muda inatosha.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Ni hoja tofauti.

**MWENYEKITI:** Ukiomba Mwongozo, utaomba kwa jambo moja mahususi. Mheshimiwa Dkt. Hamis Kigwangalla!

**MHE. DKT. HAMISI A. KIGWANGALLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naskushukuru na kukupongeza kwa kutunza ahadi yako kuwa ungetupa nafasi baadaye, lakini kwa faida ya muda, ni-*decline* kuomba mwongozo wako kwa sababu hoja zangu zinalandana na wenzangu wawili walionitangulia.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana kwa kujali muda.

Waheshimiwa Wabunge, kwanza niwashukuru Wabunge ambao waliendelea kuamini katika yale niliyoyaamua hapa kwenye Kiti kwamba kwa dhati nitawapa muda wa kuzungumza. Kwa hiyo, naomba niwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Zanzibar ndani ya Bunge hili yeye ni Mbunge, hakai ndani ya Bunge hili kama Makamu wa Rais.

Kwa Kanuni hizo hizo na hasa kwa kutumia Kanuni namba 2 (2) ambayo inaweza kumpa nguvu ama Kiti, au Spika, ama aliyekalia Kiti kina uwezo wa kufanya maamuzi yoyote kulingana na atavyoona inafaa kwa kuzingatia yalitokea ama anavyofikiri; basi labda nimpe dakika mbili Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Zanzibar kama ana neno lolote anaweza kusema, halafu nimalizie Mwongozo huo mwingine wa Mheshimiwa Ole-Sendeka. *(Makofi)*

Tafadhali sana Mheshimiwa Mbunge na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, dakika mbili halafu tutaendelea. *(Makofi)*

**MHE. BALOZI SEIF ALI IDD - MAKAMU WA PILI WA RAIS WA ZANZIBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kutoa ufafanuzi kuhusu yaliyotokea jana na natoa pole kwa Wabunge wetu humu ndani hasa Wabunge wa Chama cha Mapinduzi kwa yaliyotokea jana. Kwa sababu yalitokea jana kwakweli kidogo yametushushia hadhi kwa Bunge hili linaloheshimika kufika katika hali ile kwa sababu ambazo hazikuwa na msingi. Vile vile nimpe pole sana rafiki yangu Mheshimiwa Waziri Mkuu, najua alikuwa katika hali ngumu sana jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba naunga mkono barua iliyosomwa na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, ilikuwa ni barua sahihi na pia niseme kuwa ni barua ambayo niliandika mimi mwenyewe kwa mkono wangu, ilikuwa sahihi. Ukimwondoa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, mimi ndiye Msemaji Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa hiyo, maelezo yoyote yanayoweza kuja ndani ya Bunge hili kupitia njia za panya, yasikubalike yakaanza kutupotosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mbunge mwenzetu, lakini kwa wadhifa ule mkubwa ambao wenzetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wamekupa, Makamu wa Pili wa Rais, tunakushukuru kwa maelezo yako na maneno yako uliyowatamkia Watanzania kupitia Bunge hili. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo uliotolewa na Mheshimiwa Ole-Sendeka, naomba niuchukue, utafanyiwa kazi na Ofisi zetu kwasababu ni lazima kuutazama, ni tukio ambalo halijawahi kutokea na ni tukio la kwanza katika historia ya Bunge hili.

Kwa hiyo, nafikiri ninahitaji kufanya mashauriano ya kutosha na wataalamu wetu wa Sheria wa Bunge, lakini na vyombo vingine vinavyohusika. Baada ya hapo, basi tutalitolea mwongozo wa namna ya utekelezaji wa suala hili pale ambapo litakuwa limekamilika.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kujibu miongozi hiyo miwili, naomba nisitishe shughuli hizi mpaka saa 11.00 jioni.

Naomba niendelee kuwakumbusha kwamba muda huo wa saa 11.00 jioni utakuwa ni muda wa kusikiliza hotuba ya kuahirisha Bunge kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli hizi mpaka hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.57 mchana Bunge lilifungwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu!

**NDG. JOHN JOEL-KAIMU KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(2) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2013, naomba kutoa taarifa kwamba shughuli zote zilizowekwa kwenye Orodha ya Shughuli kwa ajili ya Mkutano wa Kumi na Mbili, sasa imemalizika.

## HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Katibu wetu kwa kutupatia taarifa hiyo, sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ajili ya kutoa hoja ya kuahirisha Bunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutekeleza na kukamilisha majukumu yetu katika muda uliopangwa. Katika Mkutano huu, Maswali 120 ya Msingi na 305 ya Nyongeza ya Waheshimiwa

Wabunge yalijibiwa na Serikali. Aidha, jumla ya Maswali 12 ya Msingi ya Papo kwa Papo na 11 ya Nyongeza yalijibiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu lilijadili na kupitisha Miswada Mitatu. Miswada hiyo ni:-

(i) Muswada wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji wa Mwaka 2013 *[The National Irrigation Bill, 2013*];

(ii) Muswada wa Sheria wa Vyama vya Ushirika wa Mwaka 2013 *[The Cooperative Societies Bill, 2013*]; na

(iii) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2013 *[The Constitutional Review (Amendment) Bill, 2013].*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitumie nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kujadili na kukubali kupitisha Miswada hiyo kwa umahiri mkubwa. Aidha, niwapongeze Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Wataalam wote waliohusika na maandalizi ya Miswada hiyo. Kipekee niwashukuru Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kupitia Miswada yote na kutoa maoni yao, ambayo sehemu kubwa yamezingatiwa na Serikali katika kuboresha Miswada hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, asubuhi ya leo Bunge lako Tukufu lilipokea Kauli za Mawaziri wa Fedha na Uchukuzi. Wote tunawashukuru kwa maelezo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Mfumo wa Matokeo Makubwa Sasa *(Big Result Now).* Katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge uliomalizika mwezi Juni, 2013, Serikali iliahidi kwamba, katika Bajeti ya mwaka 2013/2014, itaanza kutekeleza Mfumo Mpya wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambao unajulikana kwa dhana mpya ya 'Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa' (*Big Results Now-BRN*). Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mfumo huo mpya umeanza kutekelezwa kama ilivyokusudiwa. Utekelezaji wa Mfumo huu mpya umekuwa unatekelezwa katika mikondo (*streams*) mikuu miwili, inayoenda sambamba. Mkondo wa kwanza, ni kujenga na kuimarisha mfumo utakaohakikisha kuwa Matokeo Makubwa tarajiwa katika mikakati yetu ya kuleta maendeleo endelevu nchini yanapatikana (*Strengthening the Delivery System*). Mkondo wa pili, ni kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa mikakati iliyoainishwa katika Awamu ya Kwanza ya uchambuzi wa Kimaabara (*LABs*).

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Juni, 2013 maandalizi muhimu ya Awamu ya Kwanza ya uchambuzi wa kina wa kimaabara wa maeneo sita yaliyochaguliwa Kitaalam ulikuwa umekamilika. Napenda kuwakumbusha kuwa, maeneo hayo sita ni nishati ya umeme,

uchukuzi, kilimo, elimu, maji na ukusanyaji wa mapato. Kazi zilizotekelezwa katika kipindi hiki kifupi cha kuanzia Julai 2013 hadi sasa ni pamoja na zifuatazo:-

(a) Serikali imemteua Mtendaji Mkuu wa Taasisi Mpya ya *President's Delivery Bureau* (*PDB*) na amekwishaanza kazi tayari. Vilevile, Naibu Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo anayehusika na masuala ya Mageuzi ya Kilimo ameteuliwa hivi karibuni. *(Makofi)*

(b) Watendaji wa Wizara husika pamoja na Wakuu wa Mikoa wote, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya zote nchini wamepata mafunzo kuhusu Mfumo Mpya wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa.

(c) Mawaziri wa Wizara Sita zilizoanza kutekeleza Mfumo Mpya wa 'Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa' *(Big Results Now)* wameingia Mikataba ya Utendaji na Mheshimiwa Rais (*Performance Contract*) yenye Viashiria vya Utekelezaji (*Key Performance Indicators).* Aidha, Makatibu Wakuu wa Wizara sita pamoja na Watendaji wao, Wakuu wa Mikoa yote, Makatibu Tawala wa Mikoa, pamoja na Watendaji wao, wote wameingia Mikataba hiyo ya Utendaji Kazi ili kufikia malengo yaliyowekwa.

(d) Muundo wa Taasisi ya *President's Delivery Bureau* na ule wa Vitengo vya Kusimamia Utekelezaji katika Wizara (*Ministerial Delivery Units – (MDUs*)) umeidhinishwa tangu mwanzoni mwa mwezi Agosti, 2013. Aidha, tangu mwezi Julai 2013, Wizara

zinazohusika na matokeo ya awali zimeunda timu za muda za kusimamia na kufuatilia utekelezaji ili usimamizi stahiki wa utekelezaji uweze kuendelea wakati taratibu za kupatikana kwa watumishi wa kudumu zikiendelea.

(e) Wizara zote sita zenye Miradi ya Kipaumbele chini ya Mfumo wa 'Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa' *(Big Results Now)* ambazo ni nishati, kilimo, maji, elimu, pamoja na uchukuzi na fedha zimeanza utekelezaji wa miradi husika.

(f) Wizara zote sita zimeanza kuandaa ripoti za utekelezaji za kila wiki na kuziwasilisha kwenye *President's Delivery Bureau* kama mfumo unavyoainisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nyingine zilizofanyika ni kuundwa na kuanza kazi kwa Kamati Maalum za Kuratibu na Kusimamia Utekelezaji wa Miradi ya 'Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa' *(Big Results Now)* zinazojulikana kama *National Key Results Areas (NKRA) Steering Committees.* Kamati hizi zimeundwa na Wawakilishi wa Wadau muhimu katika kuhakikisha mikakati ya utekelezaji inatekelezwa na matokeo tarajiwa yanapatikana kwa wakati. Kamati hizi zinaongozwa na Mawaziri husika na zinakutana mara moja kila mwezi kujadili mwenendo wa utekelezaji, ili kutatua vikwazo na kushughulikia changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Mageuzi na Utekelezaji (*Transformation and Delivery Council – (TDC)*) imeundwa na kuanza kazi. Kamati hii ambayo Mwenyekiti wake ni Mheshimiwa Rais ndiyo yenye mamlaka ya kusimamia utekelezaji katika Mfumo wa 'Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa' *(Big Results Now).* Kamati hii itakuwa inakutana mara moja kila mwezi kutathmini maendeleo ya utekelezaji na vilevile kuzipatia ufumbuzi changamoto na vikwazo ambavyo vitakuwa vimeshindwa kupatiwa suluhisho stahiki katika ngazi za Wizara. Kamati hiyo itafanya kikao chake cha kwanza baadaye mwezi huu ambapo itapokea muhtasari wa taarifa ya utekelezaji wa 'Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa' *(Big Results Now)* na kisha kutoa maamuzi na muongozo stahiki wa hatua za utekelezaji zinazofuata pale itakapohitajika. Katika maandalizi ya kikao hicho, nilikutana na Mawaziri wote sita wanaohusika tarehe 21 Agosti, 2013 kujadili hatua za utekelezaji na changamoto zilizopo pamoja na mikakati ya kuzipatia ufumbuzi. Aidha, kuanzia tarehe 7 hadi 8 Septemba, 2013 hapa Dodoma, Ofisi yangu inatarajia kukutana na Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala wa Mikoa kupitia na kujadili Taarifa za Utekelezaji katika kipindi cha miezi miwili iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, muda ambao utekelezaji wa mfumo wa 'Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa' *(Big Results Now)* umeanza kutekelezwa rasmi ni mfupi mno, lakini dalili zinaonesha kuwa, matokeo mazuri yataanza kuonekana muda si mrefu kuanzia sasa na yatakuwa yakianishwa kadri

yanavyojitokeza. Serikali kwa ujumla imejipanga kuhakisha Miradi ya 'Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa' *(Big Results Now)* inatekelezwa kwa wakati na kwa ukamilifu kwa kuzingatia Viashiria vya Utekelezaji *(Key Performance Indicators - KPIs*) vilivyoainishwa wakati wa uchambuzi wa kimaabara kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya chakula. Tathmini ya awali ya uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa 2012/2013 iliyofanyika kati ya mwezi Julai na Agosti 2013 kwa Mikoa 25, imeonesha kuwa Mikoa minane ya Rukwa, Katavi, Mbeya, Ruvuma, Iringa, Kagera, Geita na Njombe itazalisha ziada ya chakula. Aidha, Mikoa minane ya Kigoma, Simiyu, Morogoro, Lindi, Mtwara, Pwani, Manyara na Tanga itajitosheleza kwa chakula. Aidha, Mikoa tisa ya Dar es Salaam, Dodoma, Tabora, Arusha, Mwanza, Shinyanga, Singida, Kilimanjaro na Mara itakuwa na uhaba wa chakula na kwamba Halmashauri 60 katika Mikoa 19 zitakuwa na maeneo tete yatakayokabiliwa na uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, hali ya uzalishaji na upatikanaji wa chakula nchini hadi kufikia mwezi Agosti 2013 ni ya kuridhisha katika maeneo mengi kufuatia mavuno ya msimu wa 2012/2013 kuanza kuingia sokoni. Bei za wastani za vyakula sasa hasa kwa mazao ya mahindi na mchele zimeanza na zinaendelea kushuka kufuatia uvunaji wa mazao hayo katika maeneo mbalimbali ya nchi. Uchambuzi unaonesha kuwa bei ya wastani ya mahindi Kitaifa imeshuka kutoka bei ya kilele ya Sh.774 kwa kilo mwezi

Februari, 2013 hadi Sh.513 kwa kilo mwezi Agosti, 2013. Aidha, bei ya wastani ya mchele Kitaifa imeendelea kushuka kutoka Sh.1,825 kwa kilo mwezi Februari, 2013 na kufikia Sh.1,215 kwa kilo mwezi Agosti, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Hifadhi ya Chakula ilianza kazi ya ununuzi wa nafaka (mahindi na mtama) mwezi Julai, 2013 katika Vijiji kwa Sh.450 kwa kilo na katika Miji kwa Sh.480 kwa kilo. Aidha, ili kuufanya Wakala kupata chakula cha kutosha kinyume na ilivyokuwa mwaka jana 2012/2013 na kuwawezesha kushindana na wafanyabiashara, Serikali iliamua kuongeza bei kidogo watakayotumia Wakala kununulia nafaka hiyo hadi kufikia Sh.500 kwa kilo katika vituo vyote vya ununuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ununuzi na akiba ya chakula kupitia Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*NFRA*) inaendelea vizuri na kwamba katika msimu wa mwaka 2013/2014, Wakala umepanga kununua tani 200,000 za nafaka kupitia kanda zake kama ifuatavyo: Makambako (tani 40,000); Sumbawanga (tani 50,000); Songea (tani 50,000); Dodoma (tani 15,000); Arusha (tani 20,000); Dar es Salaam (tani 10,000) na Shinyanga (tani 15,000). Hadi kufikia tarehe 03 Septemba, 2013 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula, umenunua kiasi cha tani 159,602 za nafaka ambapo tani 159,421 ni mahindi na tani 181 ni mtama. Akiba ya nafaka katika Maghala ya Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kwa sasa ni tani 182,587 zikiwemo tani 182,406 za mahindi na tani 181 za mtama. Kiasi hiki kinajumuisha tani 22,985 zilizokuwepo

katika maghala kabla ya kufanyika kwa manunuzi hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, katika ununuzi huu, *NFRA* ilichelewa kupata fedha kutoka Serikalini kwa ajili ya ununuzi wa kiasi chote cha mahindi kilichokwisha kununuliwa. Tayari wiki hii siku ya Jumatatu, Serikali imekwishatoa shilingi bilioni ishirini na tano kwa ajili hiyo. Jitihada zaidi zinafanywa na Serikali ili kupata fedha zaidi kwa ajili ya kuendelea na ununuzi wa mahindi na mtama.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwahakikishia wananchi wote kupitia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali imejipanga vizuri. Aidha, chakula cha kutosha kipo kwa maeneo yanayoelezwa kuwa na uhaba wa chakula na hakuna mwananchi atakayepoteza maisha yake kutokana na kukosa chakula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kuwaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya zenye chakula cha ziada, kuwahimiza wakulima kuhifadhi chakula cha kutosha kwa mahitaji ya Kaya zao. Aidha, Halmashauri za Wilaya ziweke mikakati madhubuti ya kuzuia ununuzi holela wa chakula kutoka katika mashamba ya Wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya pembejeo za kilimo kwa msimu wa 2013/2014. Tutakumbuka kuwa katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge lako Tukufu, nilieleza changamoto zilizoukumba Mfumo wa Kusambaza Pembejeo kwa

njia ya Vocha. Serikali iliamua kutafuta mfumo tofauti ili kuondokana na changamoto hizo. Moja ya hatua zilizochukuliwa ni kuweka utaratibu na uwiano wa asilimia 80 kwa vocha na asilimia 20 kwa mikopo. Aidha, Serikali imeidhinisha Bajeti ya shilingi bilioni 112.46 kati ya kiasi hicho shilingi bilioni 19.97 za ufadhili wa Benki ya Dunia na shilingi bilioni 92.49 za Serikali kwa ajili hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za zabuni za kuchapisha vocha kwa ajili ya mfumo huu wa ruzuku ya vocha zimekamilika na hadi kufikia tarehe 29 Agosti 2013, awamu ya kwanza ya vocha 300,000 kati ya vocha 523,000 zinazohitajika kwa ajili ya maeneo yanayowahi msimu zilishawasili nchini na zinaanza kusambazwa kwenda katika Mikoa ya Njombe, Mbeya, Katavi, Kigoma na Mwanza. Kiasi cha vocha zilizobaki zinategemewa kusambazwa mara zitakapowasili baadaye mwezi Septemba, 2013.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujiandaa na utekelezaji wa utaratibu huu mpya wa upatikanaji wa mikopo ya pembejeo kwa njia ya vikundi vya wakulima, Serikali imeteua Mikoa Saba (7) ya Ruvuma, Njombe, Mbeya, Iringa, Manyara, Geita na Shinyanga kuanza na Vyama vya Ushirika vya Mazao (*AMCOS*) na Ushirika wa Kifedha (*SACCOS*) ambavyo vina Mikataba na Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (*NFRA*). Aidha, Serikali imeona ni vyema kuvishirikisha pia vikundi vingine kama vya umwagiliaji maji ambavyo vina sifa ya kukopesheka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha mfumo huu mpya unasimamiwa na unatekelezwa kikamilifu na kuleta matokeo yaliyotarajiwa, Serikali katika kipindi cha mwezi Septemba 2013, itaendesha semina ya kutoa elimu ya mpango huu kwa Watendaji wa Kilimo na Ushirika katika ngazi za Mikoa na Wilaya na Wawakilishi wa Vyama vya Ushirika katika Mikoa husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulieleza Bunge lako Tukufu na wananchi wote kwa ujumla, kuwa Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu upatikanaji na usambazaji wa pembejeo na vocha za ruzuku kwa mfumo huu. Nitumie nafasi hii kuwaagiza Wakuu wa Mikoa na Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri, kusimamia kwa karibu upatikanaji na usambazaji wa vocha na pembejeo hizo ili kuwasaidia wakulima kuzipata mapema na kwa kiwango cha ubora unaotakiwa. Vilevile nataka kuwaomba Wabunge wenzangu tuliopo hapa na wale ambao wapo nje ya eneo la Bunge letu, wahakikishe wanasaidiana na Mikoa, Wilaya pamoja na Halmashauri katika kubainisha kasoro zozote zitakazojitokeza katika usambazaji wa vocha na kutoa taarifa katika vyombo na ofisi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia. Serikali inaendelea na utekelezaji wa miradi ya Kitaifa ya Kipaumbele katika Sekta ya Nishati katika Mfumo Mpya wa ‘Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa’ *(Big Results Now).* Miongoni mwa miradi hiyo ni ujenzi wa bomba la gesi asilia kutoka Mtwara na Lindi hadi Dar es Salaam pamoja na kujenga mitambo

miwili ya kusafisha gesi hiyo katika maeneo ya Mnazi Bay-Madimba (Mtwara) na Kisiwa cha Songo Songo (Lindi). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa, meli nne kati ya meli 12 zimewasili nchini zikiwa na shehena ya jumla ya vipande 16,623 vya mabomba ambayo yameanza kusambazwa katika maeneo husika. Mabomba hayo yatawezesha ujenzi wa bomba wa umbali wa Kilomita 194 kati ya Kilomita 532 za umbali wa mradi wote. Kazi ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi wa mradi inaendelea, mfereji wa mabomba yaani (Mkuza) umesafishwa kwa umbali upatao kilomita 293 na kazi ya kuunga bomba yaani (*welding*) imeanza tangu tarehe 26 Agosti, 2013. Kazi ya kulaza bomba kutoka Mtwara hadi Dar es Salaam inategemewa kukamilika ifikapo Juni, 2014 na kukamilika kwa mradi wote kunatarajiwa kuwa Desemba, 2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bomba hilo la gesi linatarajiwa kusambaza gesi katika maeneo ya Mtwara, Lindi, Kilwa, Somanga Fungu, Mkuranga, Dar es Salaam na maeneo mengine ya Tanzania kwa matumizi mbalimbali. Bomba litakuwa na uwezo wa kusafirisha gesi asilia yenye futi za ujazo milioni 784 kwa siku. Aidha, bomba hilo litakuwa na uwezo wa kusafirisha kiasi cha futi za ujazo milioni 1,002 baada ya kujenga vituo viwili vya kushindilia gesi asilia vitakavyojengwa maeneo ya Madimba (Mtwara) na Songo Songo (Lindi). Ni dhahiri kwamba kukamilika kwa mradi huu mkubwa wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia ni kichocheo kikubwa cha maendeleo kwa

wananchi wa maeneo hayo na kwa uchumi wa Taifa letu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imedhamiria kuendeleza miradi ya kusambaza umeme Vijijini kupitia Wakala wa Usambazaji Umeme Vijijini (*Rural Energy Agency – REA*). Tayari Miradi kumi ya usambazaji umeme ipo katika hatua mbalimbali. Zabuni za kutafuta Wakandarasi zimetangazwa, wakati miradi minne ipo katika hatua za utekelezaji (*Implementation Phase*). Miradi iliyoanza kuwaunganishia wateja umeme wa Gridi ya Taifa ni; "*Pending and New Application for Customer Connections*" ambao unatekelezwa na *TANESCO*. Mradi huu kwa kipindi cha mwezi Januari mpaka Agosti 2013, jumla ya wateja 91,199 waliunganishiwa umeme. Kati yao wateja wapatao 17,355, sawa na asilimia 19 waliunganishwa katika kipindi cha mwezi Julai mpaka Agosti, 2013 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mfumo mpya wa 'Tekeleza Sasa kwa Matokeo Makubwa' *(Big Results Now)*. Jitihada za kuendeleza vyanzo vya Nishati Jadidifu (*Renewable Energy*) bado zinaendelea kwa kasi kwani Mradi wa "*Sustainable Solar Market Packages (SSMP I)"* ambao unatekelezwa Wilayani Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa chini ya msaada wa Benki ya Dunia pamoja na Serikali ya Tanzania, tayari Taasisi za Umma 300 pamoja na Kaya 250 za watu binafsi zimefungiwa mifumo ya umeme-jua.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya umeme itokanayo na maporomoko madogo ya maji ya Mawengi (Njombe) utakaozalisha Megawati 0.3,

Mwenga, (Iringa) utakaozalisha Megawati 4.0 na Mbagamao (Ruvuma) utakaozalisha Megawati 1.0 nayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na uunganishaji wateja ambapo hadi kufikia tarehe 30 Agosti, 2013, jumla ya wateja 1,510 kati ya 4,922 wanaolengwa wameunganishiwa umeme. Aidha, uzinduzi wa utekelezaji wa Mradi wa "*Electricity V Package III*" ulifanyika tarehe 10 na 13 Julai, 2013, huko Ushirombo Bukombe. Mradi huo utatekelezwa kwenye Mikoa minne ya Kanda ya Ziwa ambayo ni: Geita, Mwanza, Simiyu na Shinyanga. Mradi utakapokamilika, unatarajiwa kufikisha umeme katika Vijiji na kuunga wateja wa awali wasiopungua 18,600. Mradi huu unagharimiwa kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika na Serikali ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu za kuwapata Wakandarasi kwa ajili ya kutekeleza Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini Awamu ya Pili kwa njia ya *Turnkey* katika Mikoa ya Tanzania Bara chini ya ufadhili wa Mfuko wa Wakala wa Nishati Vijijini (*Rural Energy Agency – REA*), umekamilika na tayari Mikataba ya kutekeleza Mafungu ya Kazi kwa ajili ya kupata Wazabuni yaani (*Lots)* 15 zilizopata Wakandarasi imesainiwa. Mikataba hiyo ni kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya kusambaza umeme vya misongo ya kilowati 11/33 vya Kigoma, Kasulu, Kibondo, Ngara, Mbinga na Tunduru; usambazaji umeme Vijijini katika Mikoa ya Katavi, Ruvuma, Mtwara, Njombe, Iringa, Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Tabora, Mwanza, Mara, Arusha na Kilimanjaro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Mafungu ya Kazi kwa ajili ya kupata Wazabuni (*Lots)* 10 hazikupata Wakandarasi, zimetangazwa upya tarehe 16 mwezi Agosti, 2013. Zabuni zitakazopokelewa, zinatarajiwa kufunguliwa tarehe 2 Oktoba, 2013. Mafungu ya Kazi kwa ajili ya kupata Wazabuni katika Mafungu au (*Lots)* hizo 10 ziligawanywa zaidi na kupata *Lots* ndogondogo 20 ili kuwezesha utekelezaji wa haraka na kwa muda mfupi. Mikoa ambayo inahusika katika Mafungu ya Kazi kwa ajili ya kupata Wazabuni (*Lots)* 10 ni Geita, Kigoma, Rukwa, Mbeya, Pwani, Kagera, Manyara, Tanga, Lindi na Morogoro. Utekelezaji wa miradi yote ya Mafungu ya Kazi kwa ajili ya kupata Wazabuni (*Lots) 25* unategemewa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wananchi wote na watekelezaji wa mradi huu kushirikiana kwa karibu kwa kazi katika kuhakikisha kwamba miradi hii yote inakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maji. Wizara ya Maji imekuwa ikipokea maoni na ushauri kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge na wadau mbalimbali kuhusu bajeti na utekelezaji wa Miradi na Programu mbalimbali za Sekta ya Maji. Serikali inaendelea na mchakato wa kuanzisha Mfuko wa Maji (*National Water Investment Fund*) ili kuongeza fedha za uwekezaji katika Sekta ya Maji kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Namba 12 ya mwaka 2009 kwenye kifungu cha 44.

Vyanzo vya mapato kwa utekelezaji huo ni fedha zilizoidhinishwa na Bunge na zitakazotolewa na Washirika wa Maendeleo. Hata hivyo, uanzishwaji wa Mfuko huo unahitaji pia maboresho kwenye Sheria za Maji zilizopo. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, jumla ya Shilingi Milioni 100 zimetengwa kama kianzio au (*seed money*) cha Mfuko wa Maji. Hata hivyo, kutokana na umuhimu na ukubwa wa uwekezaji unaohitajika kwenye Sekta ya Maji, Wizara imebaini kuwa vyanzo vya fedha vilivyobainishwa kwenye Sheria ya Maji havitoshelezi. Hivyo, Wizara itaanza mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria hii ili kuongeza wigo wa vyanzo vya mapato ya Mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, nyongeza ya bajeti ya Maji, Shilingi Bilioni 184.5. itakumbukwa kuwa, katika hatua za mwanzo za mchakato wa bajeti ya mwaka 2013/2014, Serikali ilikuwa imetenga fedha za miradi ya maendeleo yenye jumla ya Shilingi Bilioni 379.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya maji nchini. Miradi hiyo ililenga kuimarisha uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji Mijini na Vijijini, ikiwa ni pamoja na uendelezaji na usimamizi wa rasilimali za maji. Pamoja na fedha hizo za miradi, Serikali pia ilikuwa imetenga fedha za matumizi mengineyo Shilingi Bilioni 4.8 kwa ajili ya shughuli za uendeshaji ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo mchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kutokana na mahitaji makubwa ya huduma za maji nchini, fedha zilizotengwa awali zilikuwa hazitoshi kufikia malengo yaliyowekwa. Kwa kuzingatia hilo, Serikali iliongeza

Bajeti ya Wizara ya Maji kwa jumla ya Shilingi Bilioni 184.5 ambapo kati ya fedha hizo, Shilingi Bilioni 173.8 zilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo na Shilingi Bilioni 10.7 zilielekezwa kwenye shughuli za uendeshaji. Hivyo, baada ya nyongeza hiyo, fedha za maendeleo sasa ni shilingi bilioni 553.2. Utekelezaji wa miradi ya maji iliyopangwa mwaka 2013/2014 kwa kutumia bajeti hii mpya utawezesha kuwapatia wananchi wa Vijijini huduma ya maji hadi asilimia 60 ifikapo mwezi Juni 2014 kutoka asilimia 57.8 za sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kutoa huduma ya maji kulingana na malengo ya Milenia na Ilani ya Chama cha Mapinduzi inayoelekeza Serikali kuhakikisha kuwa wananchi waishio Vijijini wanapata huduma ya maji hadi kufikia asilimia 65 ifikapo mwaka 2015. Hivyo, kwa fedha hizi za nyongeza, Vijiji vitatu vimeongezwa kwa kila Halmashauri ili kukamilisha jumla ya Vijiji Vitano vya Awamu ya Pili. Fedha hizi za nyongeza zitatumika pia kugharamia baadhi ya miradi ya maji Vijijini inayoendelea kutekelezwa na Halmashauri kama ujenzi wa mabwawa, uchimbaji wa visima na kuendelea kugharamia Kampeni ya usafi wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa miradi ya maji baada ya nyongeza. Fedha za nyongeza kwenye miradi ya maendeleo shilingi bilioni 173.8 zitaelekezwa katika miradi kama ifuatavyo:-

(a) Shilingi bilioni 65 kwa ajili ya utekelezaji wa bradi wa Vijiji 10 kwa kila Halmashauri. *(Makofi)*

(b) Shilingi bilioni 65.6 kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji Vijijini itakayoleta matokeo ya haraka.

(c) Shilingi bilioni 18.7 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kusambaza maji katika mabwawa yaliyojengwa Iguluba, Sasajila, Habiya, Kirurumo, Sekeldidi, Matwiga, Kidete, Kawa, Mwanjoro na Wegero. *(Makofi)*

(d) Shilingi bilioni 11.7 kwa ajili ya kukarabati na kujenga miradi yenye kutoa huduma kwa wananchi wengi na Vijiji vingi zaidi.

(e) Shilingi bilioni 12.9 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kutoa maji kutoka Mto Ugala kwenda Miji ya Urambo na Kaliua na kugharamia uboreshaji wa huduma ya maji katika Miji Mikuu ya Mikoa mipya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Matumizi Mengineyo *(OC),* nyongeza ya shilingi bilioni 10.7 imefanya *OC* kufikia shilingi bilioni 15.5. Fedha hizo zitasaidia Wizara kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Programu ya Maji inayotekelezwa nchi nzima, kulipia umeme wa Mamlaka za daraja B, C na miradi ya Kitaifa, kulipia stahili za watumishi wa Wizara wanaofikia 1,541, kulipia huduma mbalimbali na sekta binafsi, kugharamia uendeshaji wa Chuo cha Maji kwa kulipia gharama za ufundishaji na chakula cha wanafunzi na kulipia ada za Taasisi za nje kulingana na mikataba na maridhiano na nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa watumishi wote watakaohusika katika utekelezaji wa miradi hii kutumia fedha hizi kulingana na mipango iliyowekwa ili wananchi wawe na imani na juhudi hizi za Serikali za kuongeza bajeti ya Maji. *(Maji)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maandalizi ya Katiba Mpya. Maendeleo ya Mchakato wa Mabadiliko ya Katiba. Kama sote tunavyofahamu, tarehe 3 Juni 2013, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal alizindua Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliyoandaliwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba katika hafla iliyofanyika katika Viwanja vya Karimjee jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzinduliwa kwa Rasimu hiyo ya Katiba, Tume ya Mabadiliko ya Katiba ilichapisha nakala za kutosha na kuzisambaza nchini kote katika Ofisi za Watendaji wa Vijiji, Mitaa, Kata, Vitongoji na Shehia kwa upande wa Zanzibar ili kuwawezesha wananchi kuisoma, kuijadili na kutoa maoni.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya uzinduzi wa Baraza, Tume ilianza mchakato wa kuandaa Mabaraza ya Katiba. Mabaraza hayo yamegawanyika katika makundi mawili: Kundi la Kwanza, ni Mabaraza ya Katiba ya Wilaya katika ngazi ya Serikali za Mitaa na Kundi la Pili ni Mabaraza ya Katiba ya Taasisi, Asasi, Taasisi na Makundi yenye Watu wenye malengo yanayofanana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mabaraza ya Katiba ya Wilaya yalisimamiwa na kuendeshwa na Tume kuanzia tarehe 12 Julai 2013 hadi tarehe 2 Septemba 2013. Jumla ya Wajumbe 10,932 wa Mabaraza wa Wilaya walipatikana. Vilevile, nakala za kutosha za Rasimu ya Katiba zilisambazwa kwa Asasi, Taasisi na Makundi ya watu wenye malengo yanayofanana. Pamoja na usambazaji huo, Rasimu ya Katiba iliwekwa katika tovuti ya Tume (www.katiba.go.tz) ili kuwawezesha wananchi wengi zaidi kupata Rasimu ya Katiba kwa urahisi na hivyo kushiriki katika mchakato huu muhimu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume kwa kushirikiana na Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA), kwa upande wa Tanzania Bara na Umoja wa Watu Wenye Ulemavu Zanzibar (UWZ), iliandaa na kuendesha mikutano miwili ya Mabaraza ya Katiba ya Watu Wenye Ulemavu Mjini Zanzibar tarehe 5 Agosti, 2013 na hapa Dodoma tarehe 15 Agosti, 2013. Mikutano hii ilitoa fursa kwa Wawakilishi wa Watu Wenye Ulemavu wa aina zote kushiriki na kutoa maoni yao kuhusu Rasimu ya Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sambamba na Mabaraza ya Katiba ya Wilaya, Tume iliruhusu Asasi, Taasisi na Makundi ya watu wenye malengo yanayofanana kuunda na kuendesha Mabaraza ya Katiba kwa lengo la kuijadili na kuitolea maoni Rasimu ya Katiba na kisha kuwasilisha maoni yao kwenye Tume. Mabaraza haya yalikuwa na uhuru wa kuanza

kuijadili Rasimu ya Katiba mwezi Juni, 2013 na yalipaswa kuwasilishwa maoni na mapendekezo yao kwenye Tume kabla au ifikapo tarehe 31 Agosti, 2013. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Tume inachambua maoni yaliyotolewa na Mabaraza ya Katiba ya Wilaya, Asasi, Taasisi na Makundi ya watu wenye malengo yanayofanana. Baada ya uchambuzi huu kukamilika, Tume itandaa Ripoti ambayo itaambatisha Toleo la Pili la Rasimu ya Katiba iliyoboreshwa kutokana na maoni ya Mabaraza ya Katiba na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Zanzibar kama Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inavyoelekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Serikali, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza Wananchi wote, Asasi, Taasisi na Makundi yote ya Watu wenye malengo yanayofanana kwa namna walivyoshiriki katika Mabaraza ya Katiba na kutoa maoni yao. Ni matumaini yangu kuwa maoni yao yataisaidia katika kuiwezesha Tume kuboresha Rasimu ya Katiba kwa masilahi ya Taifa letu. Wito wangu kwa wananchi wote ni kuendelea kushirikiana na Tume ili kukamilisha zoezi hili kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira kwa vijana na wasomi. Miradi ya Vijana Wilayani Sikonge. Mwishoni mwa mwezi Agosti 2013, nilipata fursa ya kuhudhuria Mahafali katika Chuo cha Nyuki Mkoani Tabora.

Nikiwa Mkoani hapa nilipata pia fursa ya kutembelea miradi kadhaa inayoendeshwa na vijana; wengi wao wakiwa ni wahitimu wa Vyuo Vikuu hapa nchini. Chimbuko la Miradi hii ya Vijana ni agizo la Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alilolitoa mwaka 2012 kwa Wakuu wa Mikoa na Wilaya zote nchini kutenga maeneo ya ardhi kwa ajili ya kuwasaidia vijana wanaohitimu kutoka katika vyuo mbalimbali. Lengo likiwa ni kuanzisha miradi ya kilimo ili waweze kujiajiri na baadaye kuwaajiri wenzao katika shughuli za kuzalisha mali. Aidha, vikundi hivi vinalenga kuwapatia vijana nguvu ya pamoja, kubadilishana uzoefu na kuwafanya kuwa na moyo wa kujiendeleza na kuwa chachu ya mabadiliko kwa vijana wengine na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa Wilayani Sikonge nilitembelea mradi wa kilimo chini ya kikundi cha vijana wapatao 86 wa Kijiji cha *“Pathfinders Green City”* katika Vijiji vya Tumbili na Lufwisi Wilayani Sikonge. Mradi huu unalenga kutekeleza miradi midogo takribani tisa ikiwemo ya ufugaji nyuki, kilimo cha bustani na mbogamboga kwa kutumia umwagiliaji kwa njia ya matone, ufyatuaji tofali, uhifadhi wa mazingira na kadhalika. Tayari miradi mitano imeanza na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji na minne itaanza baada ya kukamilika kwa miundombinu ya jengo la utawala, karakana ya ufundi, mabanda ya mifugo na nyumba 12 za kuishi Vijana hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Vijana – Igunga. Nilipata pia fursa ya kutembelea vikundi vya vijana katika Wilaya ya Igunga. Nilielezwa kuwa kwa kipindi cha mwaka 2009 hadi Julai, 2013, Wilaya ya Igunga imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi 92.5 kwa vikundi 56 vya vijana. Mojawapo ya vikundi hivyo ni kikundi cha *Graduates Integrated Youth Association* (*GIYA*) ambacho kimepatiwa ekari 300 na Wilaya kwa ajili ya kilimo cha alizeti na vitunguu. Vijana hawa wameshalima mashamba matatu yenye jumla ya ekari 150 za alizeti na ekari nne za vitunguu na wamekwishavuna tani 30 za alizeti ya thamani ya shilingi milioni 36.0. Wanatarajia kuuza mashudu tani 18 ya thamani ya shilingi milioni 5.4, wanatarajia mauzo kuwa shilingi milioni 41.4 na kwa vile gharama ya uzalishaji zilikuwa shilingi 14.5, wanatarajia kupata faida ya shilingi milioni 26.9. Ni dhahiri kuwa matarajio yao ni kufanya vizuri zaidi kwa miaka inayofuata kwa kuwa gharama za uzalishaji zitakuwa zimepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipata pia fursa ya kutembelea shamba la kikundi cha vijana 30 cha Elibariki Kilimo lenye ukubwa wa ekari 14 la kilimo cha mahindi, vitunguu, matikiti maji na mboga za majani katika Kijiji cha Mwanzugi. Walinieleza kuwa kwa ekari nane walizolima vitunguu wanatarajia kuvuna tani 11 zenye thamani ya shilingi milioni 27.5 kwa bei ya sasa ya shilingi 2,500/= kwa kilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, nimevutiwa sana na mfumo wa maisha ya vijana hawa ya kuishi katika Makambi, kwa Mfumo wa *Maisha Plus*. Niliona

juhudi za Mkoa za kuwaletea watu watakaowapa vijana hawa stadi za maisha ambapo walimwalika Mwanzilishi wa *Maisha Plus* Bwana Masoud Ally (maarufu kwa jina la Masoud Kipanya) ili akae na vijana hawa kwa muda. Nimemwambia Bwana Masoud kuwa sasa wananchi wanataka kuona *Maisha Plus* ya kweli na si ya kuigiza itakayowafanya vijana wengi kuvutiwa na kujiingiza katika vikundi vya uzalishaji. Aidha, nilimwomba Mkuu wa Mkoa wa Tabora apeleke watu wa kuwatia moyo vijana hawa ili wasikate tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuupongeza sana Uongozi wa Mkoa wa Tabora pamoja na Wilaya zake kwa juhudi kubwa za kuwawezesha vijana kujitambua na kuthubutu kuanza miradi hii na kuwasaidia kuondoa dhana kuwa wasomi ni lazima wapate kazi za kuajiriwa. Niupongeze pia Uongozi wa Mkoa wa Tabora kwa kutumia vyema Ushuru wa Mazao yaani *Crop Cess* katika kuwa chachu ya kuleta mabadiliko kwa vijana wetu. Niliambiwa kuwa asilimia 20 ya *Crop Cess* katika Halmashauri za Wilaya Mkoani Tabora zinarudishwa Vijiji na asilimia 80 inatumika kwa shughuli za maendeleo kama vile kusaidia vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliambiwa kuwa, Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge ilitumia Ushuru wa Mazao yaani *Crop Cess* kuwapatia Vijana wa *Pathfinders* jumla ya Sh.488,230,500/= katika msimu wa mwaka 2012/2013 na Sh.300,000,000/= zimetengwa katika bajeti ya mwaka 2013/2014. Wilaya ya Igunga

kwa kipindi cha mwaka 2009 hadi Julai, 2013 imefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya karibu shilingi Sh.93,000,000/= kwa vikundi 56 vya vijana. Naomba kutumia nafasi hii kuwapongeza sana Viongozi, Waheshimiwa Wabunge, Halmashauri zetu pamoja na vijana wote ambao wameamua kuingia katika shughuli hizi za uzalishaji mali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kazi hiyo nzuri katika Mkoa wa Tabora, nichukue fursa hii kuiagiza Mikoa pamoja na Wilaya ambazo haijatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais wafanye hivyo mapema kwa kutumia rasilimali na fursa zilizopo katika maeneo yao. Nitapenda kupata taarifa kutoka katika kila Mkoa kuhusu utekelezaji wa agizo hili muhimu sana kwa ajili ya vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutumia Vijana Wasomi kuanzisha Miradi (*Sokoine University Graduates Entrepreneurs Cooperative - SUGECO*). Mwaka 2008 nilipokuwa katika Chuo Kikuu cha Sokoine kama mgeni Rasmi katika siku ya Maadhimisho ya Kifo cha Hayati Edward Moringe Sokoine, nilipata nafasi ya kuzungumza na Wakufunzi na Wanafunzi kuhusu Maendeleo ya Kilimo nchini na changamoto zake. Nilitoa changamoto kwa Jumuiya ya Wanafunzi na Wahadhiri wa Chuo Kikuu cha Sokoine kwamba Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine wanaotaka kuonyesha kwa vitendo namna ya kutumia vizuri elimu waliyoipata, kujitokeza na kuchangamkia shughuli na fursa nyingi zilizopo kwenye kilimo/mifugo ili wawe mfano bora wa kuigwa na wakulima Vijijini

katika kuleta mabadiliko chanya ya kuongeza tija na uzalishaji katika kilimo, ufugaji nyuki, mifugo na uvuvi. Niliwaahidi kuwa iwapo watajitokeza, Serikali ipo tayari kuwasaidia. Aidha, nilishauri waandae Maandiko ya Miradi mizuri wanayopenda kuanzisha na kuiwasilisha Serikalini ili miradi hiyo itafutiwe fedha kutoka kwenye vyombo vya fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 17 Julai, 2013, nilipata fursa ya kukutana na Wawakilishi wa Ushirika wa Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (*Sokoine University Graduates Entrepreneurs Cooperative - SUGECO*) ambao wanaendesha takriban miradi ya kilimo 11 nchini ikiwemo ya ufugaji wa samaki, kuku, nguruwe na nyuki. Ipo pia miradi ya kukausha mbogagamboga na matunda na kukamua mafuta ya alizeti. Changamoto kubwa wanazokabiliana nazo vijana hawa ni pamoja na kutopata mitaji, kushindwa kumiliki ardhi, kukosa masoko ya uhakika na hata kushindwa kupata nembo za ubora kwa bidhaa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niliwaalika baadhi ya Mawaziri wakiwemo wa Wizara za Uwezeshaji na Uwekezaji, Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Kazi na Vijana, Kilimo, Chakula na Ushirika, Viwanda na Biashara, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Fedha ili kupata fursa ya kuwasikiliza vijana hao. Kwa pamoja tulishirikiana na kuweka mikakati ya kuwawezesha Vijana hawa wa (*Sokoine University Graduates Entrepreneurs Cooperative - SUGECO*) kupata ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili.

Nimewaelekeza Waheshimiwa Mawaziri kuweka mikakati ya kuwawezesha (*Sokoine University Graduates Entrepreneurs Cooperative - SUGECO*) kupata ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili ili kuweza kufikia malengo waliyojiwekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na mifano hiyo mizuri niliyoiona katika Mkoa wa Tabora na kutoka kwa Vijana wa (*Sokoine University Graduates Entrepreneurs Cooperative - SUGECO*), nimeona kuna umuhimu wa kuwasaidia vijana wanaohitimu vyuo vikuu na wengineo wanaopenda kujiingiza katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi na kadhalika ili wawe chachu ya maendeleo Vijijini. Ni dhahiri kwamba, tukiamua kwa dhati na kujipanga vizuri tunaweza kuwasaidia Vijana hao kuleta mabadiliko makubwa katika Kilimo Nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wito wangu sasa ni kama ifuatavyo:-

(1) Watanzania wote tuweke nguvu zetu katika kuwasaidia vijana ambao tayari wamejiajiri kwa kuwawezesha kupata huduma muhimu zikiwepo chakula na miundombinu muhimu ikiwemo umeme na maji. Aidha, Wizara na Taasisi zenye dhamana ya kilimo wawasaidie kupata pembejeo na zana bora za uzalishaji ili miradi hii iweze kuongeza uzalishaji na hatimaye kufikia kiwango cha kujitegemea.

(2) Viongozi wa Halmashauri kuwajibika ipasavyo na kutumia fedha za umma kwa manufaa ya Taifa letu.

(3) Viongozi wanaohusika na Ushirika wawasaidie na kuwaongoza vijana hawa waliojiunga pamoja kujisajili Kisheria ili waweze kukopesheka.

(4) Uongozi wa Wilaya na Mkoa kuwashirikisha makundi yote ya Taasisi mbalimbali zikiwemo Vyama vya Siasa, Madhehebu ya Dini na Watendaji wengine katika kuwasaidia vijana na kuhakikisha kuwa wananchi wanaozunguka maeneo yenye miradi ya vijana wananufaika na ujuzi wa Vijana na hatimaye kubadilisha maisha yao kwa ujumla.

(5) Viongozi wa Mikoa na Halmashauri katika ngazi zote kutambua kuwa vijana hawa bado wanahitaji kulelewa kimaadili, hivyo wawe karibu na vijana kwa kuwapatia semina za malezi ikiwemo michezo na burudani.

(6) Vyuo vingine vya Elimu ya Juu viweke mipango madhubuti ya kuwasaidia wahitimu wa fani zilizopo katika vyuo hivyo kuanza Ushirika kama wa (*Sokoine University Graduates Entrepreneurs Cooperative - SUGECO*).

Mheshimiwa Naibu Spika, mahusiano ya Tanzania na nchi za nje. Ujio wa Viongozi na faida zilizopatikana. Tangu mwezi Machi 2013, nchi yetu ilipata heshima

kubwa ya kutembelewa na viongozi mashuhuri Duniani. Ujio wa viongozi hao ni uthibitisho wa kuimarika kwa mahusiano na ushirikiano baina ya Serikali yetu na nchi za nje. Viongozi waliotutembelea ni pamoja na kwanza Rais wa China Mheshimiwa Xi Jinping. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Jamhuri ya Watu wa China, Mheshimiwa Xi Jin Ping, alifanya ziara nchini kuanzia tarehe 24 - 25 Machi, 2013. Ujio wa Rais Xi Jinping uliwezesha kusainiwa mikataba na makubaliano 17 kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Baadhi ya Makubaliano hayo ni ujenzi wa bandari ya Bagamoyo, itakayojengwa na Kampuni ya *Merchants Holding* ya China. Mkataba mwingine ni ule wa kujenga barabara itakayounganisha bandari hiyo na Reli ya Kati na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zanzibar. Mkataba mwingine ni kuendeleza Shirika la Utangazaji la Taifa *(TBC)*. Rais Xi Jin Ping pia alizindua na kukabidhi rasmi Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Kituo hicho kimejengwa mahsusi ili kumuenzi Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Ziara hiyo ilikuwa muhimu kwani imeimarisha uhusiano wetu na nchi ya Watu wa China. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Rais wa Marekani, Mheshimiwa Barack Obama. Tarehe 1–2 Julai 2013, nchi yetu ilipata heshima ya kumkaribisha Rais wa Marekani Mheshimiwa Barack Obama. Lengo la ziara

ya Mheshimiwa Barack Obama lilikuwa kuimarisha uhusiano katika nchi hizi mbili katika nyanja za Ushirikiano wa Kidiplomasia, Kiuchumi na Kibiashara na kadhalika. Manufaa yanayotarajiwa kutokana na ujio wa Rais wa Marekani ni pamoja na:-

(a) Kuimarika zaidi uhusiano wa ushirikiano kati ya Tanzania na Marekani katika nyanja za kibiashara na uwekezaji;

(b) Kuongezeka kiasi cha misaada ya maendeleo na ufundi kitakachotolewa katika nyanja za afya, elimu, kilimo, barabara, nishati na maendeleo ya vijana;

(c) Katika kuhakikisha Sekta ya Umeme inaimarishwa, Mheshimiwa Obama alizindua Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Umeme unaojulikana kama "*Power Africa Initiative*". Chini ya Mpango huu, Serikali ya Marekani itatoa jumla ya Dola za Kimarekani Bilioni saba na Makampuni Binafsi yatawekeza Dola Bilioni tisa. Lengo la Mpango huu ni kuimarisha upatikanaji wa umeme Barani Afrika. Kwa kuanzia mpango huu utatekelezwa katika nchi sita za Bara la Afrika, Tanzania ikiwa mojawapo. Nchi nyingine ni Ethiopia, Ghana, Nigeria, Liberia na Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, Rais Mstaafu wa Marekani, Mheshimiwa George W. Bush. Vilevile, tulipata fursa ya kumpokea Rais Mstaafu wa Marekani Mheshimiwa George W. Bush, aliyefanya ziara kuanzia tarehe 1 hadi 3 Julai 2013. Kupitia Asasi yake ya

*George Bush Foundation* waliandaa Mkutano wa Kimataifa wa Wake wa Marais wa Afrika. Aidha, katika Mkutano huo, ulizinduliwa Mpango wa Kuimarisha Mapambano Dhidi ya Kansa ya Shingo ya Kizazi na Matiti. Aidha, kupitia Mpango huo, Serikali ya Marekani ilitoa Dola Milioni tatu na mashine 16 za *CryoTherapy* zinazotumia baridi kali kuua chembechembe za Kansa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Waziri Mkuu Mstaafu wa Uingereza, Mheshimiwa Tony Blair. Tarehe 23 mwezi Julai, 2013 Waziri Mkuu Mstaafu wa Uingereza, Mheshimiwa Tony Blair alitembelea nchini mwetu. Kupitia Taasisi yake ya *Africa Governance Initiative* aliahidi kusaidia kusambaza umeme wa jua katika Shule za Sekondari Vijijini, kuboresha Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* na kusaidia uanzishaji na uimarishaji wa Kitengo cha Rais cha Ufuatiliaji na Utekelezaji wa Programu za Maendeleo (*President's Delivery Bureau - PDB*). *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tano, Waziri Mkuu wa Nchi ya Thailand, Mheshimiwa Yingluck Shinawatra. Waziri Mkuu wa Thailand, Mheshimiwa Yingluck Shinawatra alifanya ziara ya siku tatu nchini kuanzia tarehe 30 Julai, 2013. Lengo la ziara hiyo ilikuwa kuimarisha uhusiano wa Kidiplomasia, Kiuchumi na Kibiashara kati ya Thailand na Tanzania. Serikali pia ilitiliana saini mikataba mitano ya Ushirikiano katika nyanja za kukuza na kulinda vitega uchumi; kubadilishana wafungwa; kukuza ushirikiano wa kiufundi na ushirikiano kwa masuala ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Thailand kupitia Mheshimiwa Waziri Mkuu huyo, imeahidi kutoa ufadhili kwa vijana 10 kusoma Shahada ya Uzamili nchini humo. Vilevile, nchi hiyo itaanza kuleta wataalamu wa afya wa kujitolea kuja kushirikiana na wataalam wetu kuimarisha huduma ya afya nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, Rais Mstaafu wa Marekani, Mheshimiwa Bill Clinton. Rais wa 42 wa Marekani, Mheshimiwa Bill Clinton, alifika nchini tarehe 3 Agosti 2013. Kupitia Taasisi yake ya *Clinton Foundation* na Mradi wa Maendeleo wa *Clinton Development Initiative (CDI)*, alisaini makubaliano na Serikali ya kuendeleza Sekta ya Kilimo na kuwasaidia wakulima wadogo wadogo kuboresha kilimo na kiwango bora cha uzalishaji wa mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi, ujio wa Viongozi hao Mashuhuri katika kipindi kifupi, pamoja na wengine wengi kutoka nchi za Afrika na sehemu nyingine ni uthibitisho thabiti wa kuimarika kwa demokrasia ya ndani, kuwepo kwa amani na utulivu, kuimarika kwa utawala bora na kuwepo kwa mazingira bora ya uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, mafanikio yanayotarajiwa kupatikana kutokana na ujio wa viongozi ni mengi lakini kwa kutaja machache ya jumla ni pamoja na:-

(i) Kuimarika kwa ushirikiano wa Kimataifa wa Tanzania na nchi hizo na nchi nyingine;

(ii) Tanzania kufaidika na mitaji ya maendeleo kutoka nchi hizo kwa ajili ya kujenga miundombinu;

(iii) Kufunguka milango ya uwekezaji katika sekta mbalimbali. Ziara za Viongozi hao zimetoa fursa kwa wawekezaji kote duniani kuona mazingira mazuri na fursa za uwekezaji zinazopatikana nchini; na

(iv) Faraja tuliyoipata ni kuitangaza Tanzania kama nchi ambayo unaweza ukaenda ukiwa mtalii au mwekezaji kwa kadri utakavyoona inakupendeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkutano wa Kimataifa wa Majadiliano ya Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote (*Global 2013 Smart Partnership*). Kwa upande mwingine na kama nilivyogusia wakati nafunga Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge lako Tukufu, tarehe 28 Juni hadi tarehe 1 Julai 2013, nchi yetu ilipata heshima ya kuwa Mwenyeji wa Mkutano wa Kimataifa wa Majadiliano ya Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote mwaka 2013 (*Global 2013 Smart Patnership Dialogue*). Mkutano huo wa Kimataifa ambao Agenda yake kuu ilikuwa ni “Matumizi ya Teknolojia kama Nyenzo ya Kuleta Maendeleo ya Kijamii na Kiuchumi Barani Afrika” (*Leveraging Technology for Africa’s Social Economic Transformation. The Smart Partnership way*), ulihudhuriwa na washiriki zaidi ya 800 kutoka Mabara yote duniani. Idadi hiyo ilijumuisha

Wakuu wa Nchi, Serikali, Wanadiplomasia, Wawakilishi wa Makampuni ya Ndani na Nje ya Nchi, Wasomi, Wafanyabiashara na makundi mengine mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, manufaa yaliyopatikana kutokana na Mkutano huo ni pamoja na:-

(i) Kuhimiza matumizi ya Sayansi na Teknolojia pamoja na kujenga uwezo wa ndani katika uvumbuzi, ubunifu, umiliki na uendelezaji katika maendeleo endelevu ya Kijamii na Kiuchumi kwa njia shirikishi;

(ii) Mkutano huo pia umetoa fursa kwa nchi yetu kujifunza na kupata uzoefu wa dhana ya ushirikiano kwa manufaa kwa wote (*Smart Partnership*) na kuweza kusaidia kuibua fursa zilizopo za kukuza uchumi na kuondoa umaskini; na

(iii) Kutokana na idadi kubwa ya Washiriki waliohudhuria kutoka nchi mbalimbali duniani, nchi yetu iliweza kutangaza fursa za uwekezaji na utalii zilizopo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niungane na Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwashukuru Wananchi wote, hususan wa Mkoa wa Dar-es-Salaam kwa kushiriki kikamilifu katika mapokezi ya viongozi wote waliotembelea nchi yetu na kuhakikisha kwamba inadumu katika hali ya amani na utulivu. Nawasihi wananchi wote tuendelee kudumisha amani na utulivu

pamoja na mshikamano tuliouonesha. Hiyo ni tunu yetu lazima wote tuienzi na kuilinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, udhibiti wa dawa za kulevya. Vita dhidi ya dawa za kulevya nchini vilianza siku nyingi. Kwa kutambua uzito wa vita hii, mwaka 2006, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete aliunda Kikosi Kazi cha Taifa cha kushughulikia Udhibiti wa Dawa za Kulevya Nchini. Kikosi hiki kinaundwa na Vyombo vya Ulinzi na Usalama kikijumuisha Maafisa kutoka Jeshi la Polisi, Idara ya Uchumi na Forodha, Idara ya Uhamiaji, Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Idara ya Usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi karibuni kumetokea matukio ya usafirishaji wa dawa za kulevya nchini, hasa kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Kambarage Nyerere. Kwa upande wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa, kazi za kudhibiti dawa za kulevya hufanywa kwa utaratibu wa Kikosi Kazi (*Task Force*) kwa Polisi wa Kudhibiti Dawa za Kulevya, Polisi wa Viwanja vya Ndege, Uhamiaji, Idara ya Ushuru wa Forodha na Idara ya Usalama wa Taifa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kikosi Kazi cha Taifa cha kushughulikia Dawa za Kulevya pamoja na Vyombo mbalimbali vya kudhibiti usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya licha ya changamoto zilizopo, vimefanya kazi kubwa kudhibiti dawa za kulevya

nchini. Kwa mfano, Kikosi cha Kudhibiti Dawa za Kulevya Nchini tarehe 8 Machi, 2010 huko Kabuku – Mkoa wa Tanga, watuhumiwa watano walikamatwa wakiwa na kilo 95 za dawa za kulevya aina ya *heroin*. Watuhumiwa hao wamefungwa miaka 25 na kulipa faini ya shilingi Bilioni 1.5 kila mmoja. Tarehe 19 Desemba, 2010 hukohuko maeneo ya Kabuku tena Mkoa wa Tanga, watuhumiwa wawili walikamatwa wakiwa na kilo 50 za dawa za kulevya aina ya *heroin* zilizokuwa zinasafirishwa kutoka Dar es Salaam kwenda Sudan kupitia Kenya. Tarehe 21 Februari, 2011 huko Mbezi Jogoo, Wilaya ya Kinondoni, watuhumiwa wanne walikamatwa wakiwa na kilo 179 za *heroin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 4 Machi, 2011 huko Kawe, Wilaya ya Kinondoni, walikamatwa watuhumiwa wanne wakiwa na kilo 81 za *heroin*. Tarehe 7 Septemba, 2011 huko Mbuyuni, Kinondoni watuhumiwa wanne walikamatwa wakiwa na kilo 97 za *heroin* na tarehe 12 Januari, 2012 huko Mchinga Mbili, Mkoa wa Lindi, watuhumiwa wanne walikamatwa wakiwa na kilo 211 za *heroin*. Haya ni baadhi tu ya mashauri yaliyopo katika Mahakama mbalimbali nchini. Upelelezi wa mashauri hayo yote umekamilika na yapo katika Mahakama Kuu kwa hatua ya kusikilizwa. Mashauri haya ni kielelezo tosha cha kutoa picha kwamba, Kikosi Kazi cha Kudhibiti Dawa za Kulevya hufanya kazi kwa uadilifu mkubwa kwa kushirikiana na Vyombo vingine kutoka Taasisi na Idara mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya mwaka 2010 hadi Julai, 2013, mashauri 368 yanayohusu dawa za kulevya yalipelekwa Mahakamani na mashauri 91 kumalizika kwa mafanikio kwa watuhumiwa kufungwa na wengine kutozwa faini. Kwa sasa kuna takriban mashauri 245 ambayo bado yako Mahakamani. Changamoto inayotukabili katika Vyombo vyetu vya Mahakama na Jeshi la Polisi ni katika kuharakisha mashauri hayo. Pamoja na changamoto hiyo, ni maoni yangu kuwa *"Task Force"* iliyoundwa na Mheshimiwa Rais, Tume ya Kuratibu Udhibiti wa Dawa za Kulevya na Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama vinafanya kazi nzuri sana katika vita hii. Tunachotakiwa ni kuwapa Moyo wale wote waliohusika katika kuwakamata watuhumiwa wote wa dawa za kulevya, ili waweze kufanya kazi kwa bidii zaidi. Aidha, ni vizuri ikibidi kuwapandisha vyeo Maafisa kadhaa kutokana na juhudi hizo nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukio la Uwanja wa Ndege wa JNIA la tarehe 5 Julai, 2013 ambapo wako watu waliokamatwa na dawa za kulevya, mara baada ya taarifa hizo kupatikana, Kamati Ndogo ya Ulinzi na Usalama ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ilikutana tarehe 9 Julai, 2013 na kuagiza uchunguzi uanze mara moja. Kwa utaratibu, jalada lilifunguliwa, watuhumiwa kuhojiwa na hatimaye jalada hilo kupelekwa kwa Mwanasheria wa Kanda ya Dar es Salaam tarehe 29 Julai, 2013 kwa ajili ya maamuzi ya kisheria. Taratibu za kukamilisha uchunguzi wa tukio hili zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, changamoto kubwa tuliyonayo ni uharakishaji wa mashauri ya dawa za kulevya ambayo nina imani tukijipanga vizuri inawezekana. Iko hoja kwamba, labda tutafika mahala tufikirie kuwepo na Mahakama Maalum ya Dawa za Kulevya ambayo itakuwa na kazi moja tu ya kusimamia mashauri yanayohusu dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, vita vya dawa za kulevya ni shirikishi kwa kushirikiana na nchi mbalimbali duniani. Jitihada hizi hufanywa kwa kufanya mikutano ya pamoja ambapo mikakati mikubwa ya kufanya misako ya pamoja, mafunzo ya pamoja na matumizi ya vifaa mbalimbali hupangwa. Vilevile, kuhamasisha kutunga Sheria Kali zinazofanana ili kutotoa mwanya kwa watuhumiwa kupenya na kufikisha dawa za kulevya kwa watumiaji. Ni kweli kwamba, vita vya dawa za kulevya haiwezi kukomeshwa na nchi moja, kwa hiyo mapambano dhidi ya Wafanyabiashara Haramu wa Dawa za Kulevya yatafanikiwa tu, kwa nchi zote duniani kuungana katika kudhibiti biashara hii. Wauzaji, Wasafirishaji na Watumiaji wa dawa hizi tunao katika jamii zetu na baadhi yao tunawafahamu. Nitoe wito kwa wananchi wote kushirikiana na Vyombo vya Ulinzi na Usalama katika kuwafichua na kutoa taarifa za wale wote wanaojihusisha na Biashara ya Dawa za Kulevya. Serikali itaendelea kuchukua hatua stahiki kwa wale wote watakaobainika kuhusika na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze sana Wizara zote ambazo zinahusika na watumishi hawa ambao wameunda hicho Kikosi Kazi Maalum kwa kazi nzuri wanayoifanya ikiwemo Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Uchukuzi, Watu wa Usalama wa Taifa na Wizara nyingine zote ambazo kwa namna moja au nyingine zinahusika katika kusaidia kupambana na tatizo hili la dawa za kulevya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, napenda nimalizie kwa kuwashukuru wote waliosaidia kufanikisha Mkutano huu. Kipekee nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika kwa kutuongoza vizuri. Niwashukuru Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri. Aidha, niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri na kwa michango yenu mbalimbali wakati wa Mkutano huu. Namshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake pamoja na Wataalamu wote wa Serikali na Taasisi zake kwa misaada ya kitaalam na huduma mbalimbali za kufanikisha Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kumalizia, naomba niendelee kuonyesha masikitiko yangu kwamba bado hata katika Bunge lako hili katika kuhitimisha Mkutano huu bado tunao wenzetu kutoka Vyama vya Upinzani ambao wameona hakuna umuhimu wa kuja hapa Bungeni licha ya kwamba asubuhi tulikuwa nao lakini jioni hii bado wameendelea na mgomo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuwaomba na kuwasihi sana, chombo hiki ni chombo muhimu, chombo cha heshima, Bunge ni eneo Tukufu sana, hatuna budi wote kufanya kazi kwa ushirikiano wa karibu, kwa kuheshimiana na kupendana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya Bunge hili ni kutunga sheria. Utaratibu wa kutunga Sheria umeelezwa Kikanuni na wajibu wetu ni kufuata huo utaratibu. Matumaini yangu ni kwamba Mwenyezi Mungu atawajaza busara na hekima wenzetu hawa waweze kutambua dhamana waliyobebeshwa na jamii na waweze kurejea na kutoa huduma kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimalizie kwa kuwatakia wote safari njema wakati mnaporejea kwenye maeneo yenu ya kazi. Kwa maana hiyo, naomba sasa kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe hadi tarehe 29 Oktoba, 2013, Saa Tatu Asubuhi litakapokutana katika Ukumbi huu hapa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

## WIMBO WA TAIFA

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba niwashukuru sana kwa kazi kubwa ambayo mmeifanya katika kipindi chote tangu mkiwa katika Kamati Dar es Salaam na mlipokuwa hapa Dodoma kwa wiki mbili, mmefanya kazi kubwa sana, naomba niwapongezeni sana wote. Kazi hii mnayoifanya kwa niaba ya Wananchi wa Tanzania, ni kazi kubwa na ni matumaini yetu mtaendelea kuifanya kazi hii kwa juhudi zaidi. *(Makofi)*

Kama Uongozi, tumekuwa tunapata matatizo kidogo kwenye Mikutano ya Kamati, mahudhurio baadhi ya Kamati yamekuwa si mazuri sana. Baadhi ya Kamati imekuwa tabu kupata hata nusu ya Wajumbe kwa kikao na baadhi wakishafika wakisaini tu asubuhi basi wanaondoka *immediately*. Mtindo huo umeonekana hata Bungeni, watu wanasaini asubuhi halafu jioni hawapo lakini kwenye vitabu vyetu vya mahudhurio ni kwamba kwa tarehe ya leo kwa kumbukumbu zetu za *Hansard* kwa miaka yote ijayo ni kwamba wamehudhuria. Kwa hiyo, unapofika saa fulani halafu saa fulani haupo, ukasema umesusia, kwa kweli ni kitu ambacho hakisomeki hivi, ni usanii wa hali fulani hivi ambao siyo sawasawa. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge, kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu, tufanye kazi ya wananchi tuliyotumwa, tusiifanyie mzaha. *(Makofi)*

Mwisho, niwape salamu za Mheshimiwa Spika, hakuwa nasi katika muda wa wiki hii moja kwa sababu yuko nchini Afrika Kusini kwenye Mkutano wa *CPA* Afrika, wa Jumuiya ya Mabunge ya Jumuiya ya Madola ya Afrika ambapo yeye ni Rais wa Jumuiya hiyo. Ametuma salamu zake za upendo kwenu. *(Makofi)*

Nimalizie tu kwa kutoa Mwongozo mdogo aliokuwa ameuliza Mheshimiwa Ole-Sendeka asubuhi ya leo kuhusiana na vitendo vya jinai vilivyofanywa na Mbunge wa Mbeya Mjini kwa kumpiga Askari hapo nje. Tunaendelea kuwasiliana kuona ile Ibara inayotukinga Bungeni, ina kinga kiasi gani na tunaendelea kupata ushauri toka kwa wataalamu lakini kilichotokea ni sawasawa tu na pale Mahakamani Mheshimiwa Jaji yeyote ana kinga pale lakini ikitokea pale Mahakamani Jaji akampiga ngumi mtu yeyote pale Mahakamani au Mtuhumiwa sijui kinga ile kama itakuwa bado inamlinda! Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge na sisi ni vilevile, kinga hii haitulindi dhidi ya jinai zozote zile, inatulinda kuwa na uhuru wa mawazo, uhuru wa mijadala na siyo zaidi ya hapo. Mengine tuviachie vyombo vya dola vitaangalia kama kuna hoja ya kujibu. *(Makofi)*

Mwaisho kabisa, naomba niwatakie kila la kheri mnapoenda Majimboni, Mwenyezi Mungu awatangulie.

**WABUNGE FULANI:** Ameen!

**NAIBU SPIKA:** Naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi tarehe 29 Oktoba, 2013, Siku ya Jumanne, Saa Tatu Asubuhi hapa Dodoma.

*(Saa 12.40 jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 29 Oktoba, 2013, Saa Tatu Asubuhi)*